Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Books on Islam and Muslims* | *Al-Islam.org* (http://www.al-islam.org)

Kuanzia Ndoa Hadi Kuwa Wazazi

Log in [1] or register [2] to post comments

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho From Marriage to Parenthood. Sisi tumekiita, Kuanzia Ndoa Hadi Kuwa Wazazi.

Kitabu hiki kinazungumzia masuala yote yanayohusu wanandoa: kuanzia kufunga kwao ndoa - waishi vipi, mpaka watakapopata watoto - wawalee vipi - kwa mujibu wa mafundisho ya Kiislamu. Kama ambavyo inafahamika kwamba Uislamu ni dini na ni mfumo wa maisha, basi kwa hakika haukuacha hata kitu kimoja kinachohusu maisha ya mwanadamu, pamoja na kumhudumia kiroho. Ndoa ni taasisi ambayo iliasisiwa na Allah ‘Azza wa Jallah Mwenyewe pale alipowaunganisha baba yetu Adam na mama yetu Hawa kuishi pamoja kama mume na mke.

Author(s):

- Abbas na Shaheen Merali [3]

Translator(s):

- Ramadhani Kanju Shemahimbo [4]

Publisher(s):

- Alitrah Foundation [5]

Category:

- Marriage [6]

Topic Tags:

- Ndoa [7]
- Watoto [8]
- Wazazi [9]
- Familia [10]

Old url:

http://www.al-islam.org/kiswahili/pdf/ndoawazazi.pdf

Person Tags:

- Imam Ali (as) [11]
- Bibi Fatimah (as) [12]
- Imam Zainul-Abideen (as) [13]

Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho *From Marriage to Parenthood.* Sisi tumekiita, *Kuanzia Ndoa Hadi Kuwa Wazazi.*

Kitabu hiki kinazungumzia masuala yote yanayohusu wanandoa: kuanzia kufunga kwao ndoa - waishi vipi, mpaka watakapopata watoto - wawalee vipi - kwa mujibu wa mafundisho ya Kiislamu. Kama ambavyo inafahamika kwamba Uislamu ni dini na ni mfumo wa maisha, basi kwa hakika haukuacha hata kitu kimoja kinachohusu maisha ya mwanadamu, pamoja na kumhudumia kiroho. Ndoa ni taasisi ambayo iliasisiwa na Allah '*Azza wa Jallah* Mwenyewe pale alipowaunganisha baba yetu Adam na mama yetu Hawa kuishi pamoja kama mume na mke.

Kwa hiyo, Uislamu kama dini na mfumo wa maisha, umeweka kanuni, sheria na hukumu za kufuatwa ndani ya taasisi hii tukufu (ya ndoa). Waandishi wa kitabu hiki wamefanya juhudi kubwa ya kukusanya mafundisho yote muhimu yenye kuhusu taasisi hii kutoka katika vyanzo vikubwa na chimbuko la sheria na mafundisho ya Uislamu, ambavyo ni Qur'ani na Sunna

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, Ramadhani Kanju Shemahimbo kwa kukubali kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar-es-Salaam, Tanzania.

Utangulizi

Ni pale tu tunapofikiri na kutafakari juu ya mwongozo na hadithi zilizosimuliwa na Mtume (s.a.w.w.) na Ahlul-Bayt wake (a.s.) tunapoweza kutambua zile hazina walizoacha kwa ajili yetu sisi. Johari hizi za hekima zinaangaza njia kuelekea Mbinguni kwa kutupatia ushauri na maarifa katika kila hatua kwenye maisha yetu.

Kwa bahati mbaya, nyingi ya johari hizi zinapatikana kwa Kiarabu na Kifursi tu, na kuwaacha wasomaji wa Kiingereza (na lugha nyingine) kijisehemu tu cha kile kinachopatikana, hivyo kuwalazimisha kutegemea moja kwa moja juu ya taarifa za kilimwengu ili kuziba pengo hili.

Mbili ya johari hizi ni mafundisho ya kiislam ya mahusiano ya kijinsia baina ya mwanaume na mwanamke, na upatikanaji wa mtoto halali wa 'kiungu.'

Taarifa hizi kwa hiyo, zimetafsiriwa kutoka kwenye vitabu mbalimbali vya Kifursi na kukusanywa katika kitabu hiki cha mwongozo. Ni matumaini yetu kwamba hiki kitawapatia wasomaji wa Kiingereza mwon- gozo wa Kiislam utakaounganishwa na kutumika sambamba na taarifa nyingine zote zinazopatikana, kumuwezesha mtu sio tu kupata manufaa yake katika dunia hii, bali kumsogeza mtu karibu na Mwenyezi Mungu (s.w.t.) na Pepo.

Taarifa za ndani ya kitabu hiki cha mwongozo zimeegemea kwenye vyanzo sahihi na vya asili vya mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Ahlul-Bayt wake (a.s.). Mahali ilipowezekana, hadithi kutoka kwa watu hawa watukufu zimejumuishwa ili kuupa umuhimu ule msingi imara wa Kiislam unaounga mkono yale mapendekezo yaliyotolewa, na vilevile kumtia moyo msomaji katika kuwa mzoefu na maneno ya viongozi wetu katika Uislam. Kwa nyongeza, uingizwaji wa hadithi hizi unatia msisitizo umuhimu unaowekwa na Uislam katika kila kipengele cha maisha, kamwe bila kutuacha sisi tukikosa mwongozo katika hatua yoyote ile.

Katika hatua hii ni muhimu sana kueleza kwamba inawezekana kuwa hao Ahlul-Bayt (a.s.) wamezisimulia hadithi hizi katika muda mahususi, mahali au hali, ambayo taarifa kwa bahati mbaya hazijatufikia sisi. Tumejaribu kiasi cha uwezo wetu kuwaletea hadithi kama zilivyosimuliwa katika vyanzo, ili kwamba ziweze kuwa na manufaa na mafanikio.

Kitabu hiki kinaanza na mjadala kuhusu ule usiku wa harusi, pamoja na amali ambazo zimependekezwa kwa ajili ya usiku huu, kuwawezesha Bwana na Bibi harusi kuanza hatua hii mpya ya maisha yao katika njia nzuri zaidi iwezekanavyo. Kisha hii inafuatiwa na mahusiano ya kijinsia na umuhimu wake katika Uislam, na vilevile mapendekezo kwa ajili ya matendo hayo na nyakati ambazo muungano wa kijisia haswa unaoshauri- wa au usiporuhusiwa.

Mlango juu ya kanuni za kifiqhi zinazotoa taarifa muhimu katika namna rahisi unafuata. Kanuni zote za kifiqhi ni kwa mujibu wa Ayatullah al-Udhma Sayyid Ali Hasan as-Sistaniy. Muqallidin (wafuasi) wa mujtahid wengine wanashauriwa kurejea kwenye risala zao wenyewe juu ya milango hii.

Kuhusu mahusiano ya kijinsia, upangaji wa familia na kipindi cha kushika mimba, mapendekezo ya kiislam yamepewa umuhimu sana kuhusiana na vyakula, matendo na nyakati zake, ili kuandaa mazingira kwa ajili ya kutengeneza mtoto wa halali na mzuri, insha'allah.

Mara tu unapopatikana ujauzito, wote mama na baba wanahitaji kutambua majukumu wa wajibu wao, ili kuwawezesha kuyatimiza haya katika namna nzuri iwezekanavyo. Kwa mara nyingine tena, mapendekezo kwa ajili ya vyakula, matendo na madua vimeainishwa, ili kuanza kumrutubisha na kumlea mtoto huyo kuanzia kwenye hatua hizi za mapema akiwa ndani ya tumbo la mama yake.

Vitendo vinavyopendekezwa kwa ajili ya kujifungua kuliko salama na kwepesi na kwa ajili

ya kile kipindi cha mara tu baada ya kujifungua hapo tena vinajadiliwa, kuendelea hadi wakati wa kunyonyesha, ambako kunajulikana kama moja ya haki za mtoto. Hili, halafu linafuatiwa na kanuni muhimu za ziada ya kifiqhi juu ya mama, zikishughulika hasa na suala la *nifaas* (ile damu anayoona mama baada ya kujifungua).

Mwisho lakini sio kwa umuhimu wake, kitabu hiki kinamalizia na mlango juu ya malezi ya watoto, pamoja na nukta arobaini juu ya namna ya kutendeana na mtoto wako, kudukiza au kuingiza kidogo kidogo mapenzi kwa Ahlul-Bayt (a.s.) ndani yao na vidokezo na ushauri wa kuhifadhi Qur'ani kwa wazazi na watoto.

Sehemu hii taarifa muhimu na za kuvutia ambazo kama zitashikwa kikamilifu, zinaweza kutumika ili kupata matokeo chanya na yenye manufaa kwa mtoto.

Ni muhimu kutaja nukta fulani fulani ambazo zinaweza zikazuka katika akili ya msomaji pale anapopitia kile kiwango kikubwa cha taarifa kilichokuwepo.
Kwanza, mapendekezo fulani yanaweza kuonekana kuwa maalum sana na mafinyu, kama yale ya nyakati ambazo mtu anapaswa na pale ambapo hapaswi kushika mamba, hata hivyo, ni lazima ikumbukwe kwamba Uislam sio dini ngumu, na mapendekezo haya hayapo ili kuweka vizuizi visivyo na lazima juu yetu. Bali kwa usahihi zaidi, mapendekezo haya yanawekwa pale kwa faida yetu, na Muumba ambaye anatujua vizuri sana kuliko tunavyojijua sisi wenyewe.

Juhudi ndogo kutoka upande wetu sisi zitakuwa zichukue matokeo ya muda mrefu ambayo tunaweza hata pia tusiyatambue. Kwa kweli ni muhimu kuona kwamba mengi ya mapendekezo yamebaki hivyo, ni mapendekezo tu. Tunayotakiwa kufanya sisi ni kuyaendea haya kwa nia sahihi, kuhakikisha kwamba vitendo vya wajibu vinafanyika na kujaribu kwa uwezo wetu wote na hayo mengine, na insha'allah Yeye atakuongoza katika njia iliyobakia.

Pili, wanawake wa Kiislam hususan hasa wanao wajibu wa nyongeza wakati wa ujauzito na baada, kwamba wasifanye yale mambo ya kiafya tu na ushauri unaopaswa kushikwa, bali na mambo ya kiroho pia. Hili zaidi hasa ni gumu kama mimba yenyewe ni ya matatizo. Kwa mara nyingine tena, mtu ni lazima azingatie akilini kwamba manufaa yanazidi gharama zenyewe.

Kwa nyongeza, sio lazima kwamba kila tendo moja lililopendekezwa laz- ima litekelezwe; bali mama mwenyewe lazima aone ni kipi kinachofaa zaidi kwake na kutekeleza kile anachoweza kukifanya kwa ubora wa uwezo wake wote na kuyaacha mengine mikononi mwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye ni Mjuzi wa yote. Hili hasa linafungamana vizuri kwa kuchukulia kwamba mapendekezo yenyewe yatakuwa na matokeo yanayotakiwa tu kama yakitendwa kwa moyo uliotulia na wenye amani, kuliko wenye wasiwasi na mfadhaiko.

Kweli, katika vipengele vyote vya maisha, Uislam umetoa umuhimu kwenye 'njia ya kati' na kukataza mambo ya kuzidi kiasi. Kadhalika, ni jambo la busara kukumbuka kwamba mapendekezo yaliyomo katika kitabu hiki, kila moja lina wakati wake na mahali pake, na hayapaswi kuingiliwa kwa nguvu kupita kiasi, wala kupuuzwa moja kwa moja.

Kwa mfano, moja ya mapendekezo kwa ajili ya mtoto mzuri ni kwamba baba anapaswa kula komamanga; hata hivyo, hii haina maana kwamba baba huyo afanye komamanga kuwa ndio tunda lake peke yake, na hata kulibadilisha kwa ajili ya milo yake mikuu kwani jambo hilo lina madhara na ni hatari. Ni pale tu ambapo njia ya wastani au ya kati na kati

itakapofuatwa ambapo manufaa ya kina ya kiroho ya mapendekezo haya yanapokuja kufanya kazi na kuathiri maisha yetu.

Kwa kumalizia, kwa ajili ya mtazamo mpana kwenye maeneo haya, tungependa kupendekeza kwamba kitabu hiki kisomwe kwa kushirikiana sambamba na dua zilizomo kwenye kitabu 'A mother's Prayer'* (Dua za Mama) kilichotungwa na Saleem Bhimji na Arifa Hudda.

Tungependa kuwashukuru wale wote ambao wamechangia kwenye kitabu hiki kwa njia moja au nyingine, na kukisaidia wakati wote. Mwenyezi Mungu Mtukufu awalipe kwa ajili ya kila kitu..

Mwisho, tunaomba msamaha kwenu endapo kuna mapungufu yoyote au makosa ndani ya kitabu hiki; tafadhali tujulisheni na insha'allah, sisi tutajaribu kukiboresha kwa ajili ya wasomaji wa baadae. Maoni au ushauri mwingine wowote unakaribishwa pia. Wakati unapotumia kitabu hiki, tafadhali kumbuka familia zetu katika du'a zako, na pia Marehemu wote kwa kusoma Suratul-Fatihah.

Tunaomba kwa unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu atukubalie juhudi zetu hizi, na kama atatukubalia, basi tunaziwasilisha kwa Hadharat Ma'sumah (a.s.) ambao katika ujirani wao tumeikamilisha kazi hii, na Mtukufu Imam wetu wa zama, Imam Mahdi (a.s.).

"Sifa zote njema ni Zake Allah (s.w.t.). Mola wa walimwengu wote."

*Kitabu hiki kinaweza kununuliwa kutoka **Islamic Humanitarian Service** kwenye Mtandao kupitia www.al-haqq.com [14]. Ili kuwasiliana na mwandishi unaweza kutuma baruapepe kwa anuani tph@tph.ca [15].

Abbas na Shaheen Merali
1 Julai, 2005
Qum Shariif.

Mlango 1: Usiku Wa Harusi (Ndoa)

A'mali Za Usiku Wa Harusi

Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba: "Milango ya Peponi kwa ajili ya rehema itafunguliwa katika hali nne: Wakati inaponyesha mvua; wakati mtoto anapoangalia kwa huruma usoni kwa mzazi wake; pale mlango wa Ka'ba unapokuwa wazi, na wakati wa (kutokea) harusi."1

Kama inavyoonyeshwa na hadithi hiyo hapo juu, dhana ya harusi katika Uislam ni tukufu mno na yenye kuthaminiwa, kiasi kwamba milango ya rehema ya Mwenyezi Mungu inafunguliwa katika tukio hili.

Naam, hili halishangazi pale mtu anapochukulia kwamba ndoa inahifadhi sehemu kubwa ya imani ya mtu na kuilinda na uovu wa Shetani, kama ilivyosimuliwa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.): "Hakuna kijana yeyote atakayefunga ndoa katika ujana wake, isipokuwa kwamba shetani wake anapiga makelele akisema: 'Ole wake, ole wake, amezikinga sehemu

mbili ya tatu ya imani yake kutokana na mimi;' kwa hiyo mwanadamu lazima awe na taqwa (mwenye kumcha Mungu) kwa Mwenyezi Mungu ili kulinda sehemu moja ya tatu ya imani yake iliyobakia.2

Ni muhimu kwa hiyo, kwamba wawili hao, pale wanapoingia kwenye hatua hii, wachukue hadhari ya hali ya juu kulinda usafi wa muungano huu mtukufu na wala wasiutie doa tangu mwanzoni mwake kwa kuruhusu lile tukio la sherehe ya harusi kuwa ni chanzo cha madhambi na israaf.

Hususan ule usiku wa harusi ndio usiku wa kwanza ambao mwanaume na mwanamke wanakuja pamoja kama mume na mke, na imekokotezwa sana kwamba wanaunda muungano huo kwa nia ya kupata ukaribu na radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu na kufanya zile A'amali zilizopendekezwa kwa ajili ya usiku huo.

Wakati huu ni muhimu kuangalia ni hali gani yule 'Bibi wa wanawake wote wa ulimwengu,' Hadhrat Fatimah (a.s.) aliyokuwa nayo ule usiku wa harusi yake, na ni vipi alianza maisha yake na mume wake, Imam Ali (a.s.): Katika ule usiku wa harusi Imam Ali (a.s.) alimuona Hadhrat Fatimah (a.s.) alikuwa amefadhaika na akitokwa na machozi, na akamuuliza kwa nini alikuwa kwenye hali ile.

Yeye alijibu akasema: "Nilifikiria kuhusu hali yangu na vitendo na nikakumbuka mwisho wa uhai na kaburi langu; kwamba leo nimeondoka nyumbani kwa baba yangu kuja nyumbani kwako, na siku nyingine nitaondoka hapa kwenda kaburini na Siku ya Kiyama.

Kwa hiyo, namuapia Mungu juu yako; njoo tusimame kwa ajili ya swala ili kwamba tuweze kumuabudu Mwenyezi Mungu pamoja katika usiku huu."3

A'amali Zifuatazo Zinapendekezwa Kwa Ajili Ya Usiku Huu

A'amali Zifuatazo Zinapendekezwa Kwa Ajili Ya Usiku Huu4

1. Jaribu kuwa katika Udhuu kwa kiasi kirefu kinachowezekana cha usiku huo, na hususan wakati wa A'amal zifuatazo hapa chini.

2. Anza kwa kumtukuza Mwenyezi Mungu Mtukufu halafu useme "**Allahu Akbar**," ikifuatiwa na Swala ya Mtume – *Allahumma swali 'alaa Muhammadin wa aali Muhammad*).

3. Swali rakaa mbili, kwa nia ya '*Mustahab Qurbatan ilallah*' – kujisogeza karibu na Allah (s.w.t.). (Swala inayopendekezwa kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu) ikufuatiwa na Swala
ya Mtume.

4. Soma Dua ifuatayo, ikifuatiwa na Swala ya Mtume. Kwanza bwana harusi aanze kuisoma, baada yake ambapo bibi harusi atapaswa kusema: Ilahi Amin (Mwenyezi Mungu aitakabalie Dua hii).

"Allahumma rzuqniy ilfahaa wa wudhahaa wa ridhwaahaa wa radhwiniy bihaa thumma j'ma'u bayinanaa bi-ahsani j'timaa'in wa asarri itilaafin fainnaka tuhibbul-halaala wa takrahul-haraam."

"Ewe Allah! Nijaalie na upendo wake, mapenzi na kunikubali kwake mimi; na nifanye mimi niridhike naye, na tuweke pamoja katika namna bora ya muungano na katika muafaka kamilifu, hakika Wewe unapenda mambo ya halali na unachukia yale ya haram."5

5. Hata kama wawili hao hawadhamirii ushika mimba katika usiku huo wa harusi, inapendekezwa kwamba Dua zifuatazo zisomwe kwa ajili ya watoto wazuri (wakati wowote itakapotunga mimba):

a. Bwana harusi anapaswa aweke kiganja cha mkono wake wa kulia kwenye paji la uso la bibi harusi kwa kuelekea Qibla na asome:

"Allahumma bi-amaanatika akhadhtuhaa wa bikalimaatika stahlaltuhaa fain qadhwayta liy minhaa waladaan faaj'alhu mubaarakaan taqiyyan min shiy'ati aali Muhammad wa laa taj'al lil-shaytwaani fiyhi shirkaan wa laa naswiybaan.

"Ewe Allah! Nimemchukua (binti) huyu kama amana Yako na nimemfanya halali juu yangu mwenyewe kwa maneno Yako. Kwa hiyo, kama umenikadiria mtoto kutokana naye, basi mfanye mbarikiwa na mchamungu kutoka miongoni mwa wafusi wa familia ya Muhammad; na usimfanye Shetani kuwa na sehemu yoyote ndani yake."6

b. Dua ifuatayo pia inapaswa kusomwa:

"Allahumma bi-kalimaatika stahlaltuhaa wa bi-amaanatika akhadhtuhaa. Allahumma-j'alhaa waluwdaan waduwdaan laa tafraku taakulu mimmaa raaha wa laa tas-alu 'ammaa saraha."

"Ewe Allah! Nimemfanya awe halali juu yangu kwa maneno Yako, na nimemchukua katika amana Yako. Ewe Allah! Mjaalie awe mwenye kuzaa na mwenye upendo."7

6. Bwana harusi aioshe miguu ya bibi harusi na anyunyize maji hayo katika pembe zote nne za chumba na nyumba. Mwenyezi Mungu Mtukufu ataondoa aina 70,000 za umasikini, aina 70,000 za neema zitaingia ndani ya nyumba hiyo na neema 70,000 zitakuja juu ya bibi na bwana harusi. Bibi harusi atakuwa salama kutokana na wendawazimu, vidonda vya tumbo na ukoma.8

Mambo Kadhaa Kuhusu 'Aqd Na Ndoa

Mambo Kadhaa Kuhusu 'Aqd Na Ndoa 9

1. Mtu anapaswa kujiepusha na kufanya Aqd au ndoa wakati wa *Qamar dar Akrab* – pale mwezi unapopita kwenye eneo la ng'e (*scorpio*). **
**Kanuni hii haiungwi mkono na Shi'a wote – Mtarjuma.
2. Mtu sharti ajiepushe kutokana na kufanya Aqd au ndoa nje chini ya mwanga wa jua.
3. Inapendekezwa kwamba Aqd na ndoa zifanywe wakati wa usiku.

Dokezo: Ni muhimu kukumbuka kwamba lengo kuu la ndoa ni kumuun- ganisha mwanaume na mwanamke. Mara nyingi sana harusi zinazofanyi- ka leo hii huwa ni ndefu sana na zenye kuchosha kwa bibi na bwana harusi; wanafika chumbani kwao usiku sana wakiwa hawana nguvu za kufaa kwa ajili ya A'amali zilizopendekezwa kwa ajili ya usiku huu mtukufu, wala nyingine zaidi. Kwa hiyo, inapendekezwa kwamba taratibu za usiku huu zinawekwa rahisi na kwa kiwango kidogo kabisa. Kama sherehe nyingine zinahitajika, basi zipaswe kufanyika katika usiku uliotangulia au unaofuata ule wa harusi.

Baadhi Ya Mambo Kwa Ajili Ya Bibi Na Bwana Harusi

1. Sio lazima kwamba kujamiiana kwa kutimiza ndoa kufanyike katika ule usiku wa harusi; bali unaweza kuchukua siku chache au hata majuma machache.

2. Uchovu, wasiwasi na fadhaa vinaweza kufanya hilo liwe gumu zaidi; hivyo ni muhimu kwamba mume na mke wachukue muda wa kutosha kuweza kuwa wametulizana na kuzoeana na kwenda kwa mwendo wao wenyewe.

3. Mafuta ya kulainishia yanaweza yakahitajika kwa siku zile chache za mwanzo au majuma ili kufanya kule kujamiiana kuwa rahisi zaidi na kwenye starehe zaidi.10

4. Kumaliza mapema au kusikotarajiwa kunaweza kuwa ni tatizo kwa mara chache za mwanzoni; hata hivyo, hili linapaswa kutatuliwa baada ya kupita muda na kupatikana uzoefu.

5. Kizinda (cha bikra) kinaweza kivuje au kisivuje damu. Unyegereshano, upole na kuingiliana tena mara tu baada ya hapo kunaweza kupunguza maumivu ya uchanikaji wa hicho kizinda.

6. Baada ya kujamiiana (wakati wowote itakapokuwa), bibi harusi asije akatumia maziwa, siki, giligilani, tuhafa chungu au tikitimaji kwa kiasi cha juma moja, kwani vinasababisha tumbo la uzazi kukauka na kuwa la baridi na gumba. Kula siki wakati huu vilevile kunatokezea kwa mwanamke kutokuwa msafi (tohara) kutokana na damu ya hedhi, giligilani (na tikitimaji) kunasababisha matatizo ya wakati wa uchungu na tuhafa linasababisha kusimamisha ukawaida wa hedhi, na yote haya yanaishia kwenye kuleta maradhi.11

7. Watu wanaweza wakatoa maoni fulani juu ya siku chache zinazofuatia. Ni muhimu sana kufanya hilo lisikuathiri wewe, na usivutike kwenye mazungumzo yao.

8. Usizungumze kuhusu mambo yako ya ndani kwa watu wa nje, chunga heshima kwa mwenza wako na kwenye uhusiano wenu.

Harusi Ya Imam Ali (A.S.) Na Hadhrat Fatimah (A.S.)

‘Aqd (Mkataba Wa Ndoa)

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipenda hotuba ya ndoa isomwe msikitini na mbele ya mahudhurio ya watu. Imam Ali (a.s.) alikwenda pale msikitini kwa furaha sana, na Bwana Mtume (s.a.w.w.) vilevile akaingia msikitini mle. Muhajirina na Ansari wakakusanyika kuwazunguka. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akenda juu ya mimbari na baada ya kumtukuza na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema:

“Enyi watu! Jueni kwamba Jibril amenishukia mimi na kuniletea ujumbe kutoka kwa Allah (s.w.t.). kwamba sherehe za ndoa ya Ali (a.s.) zimefanyika mbele ya Malaika huko ‘Bait al-Ma’mur.’

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameamuru kwamba mimi nifanye sherehe hizi hapa duniani na niwafanye nyote nyie kuwa mashahidi.” Kufikia hapa, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasoma hotuba ya ndoa (‘*Aqd*).

Halafu Mtume (s.a.w.w.) akamwambia Imam Ali: “Simama na utoe hotuba.” Imam Ali (a.s.) aliianza hotuba yake na akaonyesha kufurahi na kuridhika kwake kwa ndoa yake na Hadhrat Fatimah (a.s.).

Watu wakamuombea yeye na wakasema: “Mwenyezi Mungu Mtukufu aibariki ndoa hii, na

aweke mapenzi na usuhuba ndani ya nyoyo zenu.”12

Harusi Yenyewe

Sherehe za harusi zilifanyika mnamo mwezi mosi Dhul Hijjah, mwaka wa pili Hijiria13 (au tarehe 6 ya Dhul Hijjah, 2 A.H.)14 mwezi mmoja baada ya hotuba ya ndoa.

Muda kati ya hotuba ya ndoa na sherehe za harusi, Imam Ali (a.s.) alikuwa ana haya ya kuongea kuhusu mke wake kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Siku moja, kaka yake, Aqiil, alimuuliza: “Kwa nini humleti mke wako nyumbani ili tuweze kukupongeza kwa ajili ya shughuli ya kufunga ndoa kwako?” Jambo hili lilimfikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambaye alimwita Imam Ali (a.s.) na kumuuliza: “Je, uko tayari kwa kufunga ndoa (kuoa)?”

Imam Ali (a.s.) alitoa jibu la kukubali. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Insha’allah, leo usiku au kesho usiku, mimi nitafanya maandalizi kwa ajili ya harusi.” Wakati huo, yeye Mtume (s.a.w.w.) akawaambia wake zake wamvalishe Hadhrat Fatimah (a.s.) na kumtia manukato na kuweka mazulia kwenye chumba chake ili kujiandaa kwa ajili ya sherehe za harusi.15

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akamwambia Imam Ali (a.s.): “Hapawezi kuwa na harusi bila ya wageni.” Mmoja wa viongozi wa Ansari aliyeitwa Sa’ad akasema: “Mimi nakuzawadia kondoo mmoja,” na kikundi cha Ansari nao vilevile wakaleta kiasi16 cha nafaka,17 na maji ya maziwa yaliyoganda, mafuta na tende pia vililetwa kutoka masokoni. Nyama hiyo ilipikwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pamoja na usafi wake alichukua jukumu la kupika kwa ajili ya harusi hiyo, na kwa mikono yake iliyobarikiwa, akavichanganya (viungo) na akaanza kutengeneza aina ya chakula cha kiarabu kinachoitwa Habis au Hais.18

Hata hivyo, ingawa chakula kilitayarishwa, mwaliko ulikuwa wa jumla. Idadi kubwa ya watu ilishiriki na kwa baraka za mikono ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kila mmoja alikula na akashiba kutokana na chakula hicho, na kulikuwa na kingine kamwe kilichobakia kwa ajili ya masikini na wenye shida; sinia la chakula vile vile liliwekwa kwa ajili ya bibi na bwana harusi.19

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwaambia wake zake waandae sherehe kwa ajili ya Hadhrat Fatimah (a.s.). Baada ya chakula, wanawake hao walijiku- sanya karibu na Hadhrat Fatimah (a.s.) na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akamsaidia kupanda juu ya farasi wake Mtume mwenyewe.

Salman al- Farsi alizikamata hatamu za farasi huyo na kwa sherehe hiyo maalum, wanaume majasiri kama vile Hamza na idadi kadhaa ya wana familia na maharimu wa Hadhrat Fatimah (a.s.) wakajikusanya karibu ya farasi huyo wakiwa na panga zilizochomolewa. Wanawake wengi walisubiri nyuma ya bibi harusi na wakasoma Takbira.

Farasi akaanza kutembea, na wale wanawake wakaanza kusoma Takbira na sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu Kwa wakati ule, mmoja baada ya mwingine, walisoma qaswidah nzuri na, tamu ambazo zilikuwa zimetung- wa kwa utukufu na shangwe, wakampeleka bibi harusi nyumbani kwa bwana harusi. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) vilevile alilikuta kundi hilo na akaingia chumbani kwa maharusi.

Aliitisha karai la maji, na wakati lilipo- letwa, yeye akanyunyiza kiasi juu ya kifua cha Hadhrat Fatimah (a.s.) na akamwambia atawadhe na kuosha kinywa chake kwa yale maji yaliyobakia. Alinyunyiza kiasi juu ya Imam Ali (a.s.) pia na akamwambia atawadhe na

kuosha kinywa chake.

Kisha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akachukua mkono wa Hadhrat Fatimah (a.s.) na akauweka kwenye mkono wa Imam Ali (a.s.) na akasema: “Oh, Ali! Ubarikiwe wewe; Allah (s.w.t.). amemuweka juu yako binti ya Mtume wa Allah, ambaye ndiye mbora wa wanawake (wa ulimwengu).”

Kisha akaongea na Hadhrat Fatimah (a.s.) na akasema: “Oh, Fatimah! Ali ni kutoka kwa wabora wa waume.”20

Kisha akawaombea Dua juu yao: “Ewe Allah, wafanye wazoeane (wakaribiane) na kila mmoja wao! Ee Allah, wabariki hawa! Na weka neema kwa ajili yao katika maisha yao.”

Wakati alipokaribia kuondoka, yeye akasema: “Mwenyezi Mungu Mtukufu amekufanyeni ninyi na kizazi chenu kuwa tohara. Mimi ni rafiki wa marafiki zenu, na ni adui wa maadui zenu. Sasa nakupeni mkono wa kwaheri na kukukabidhini kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu”21

Asubuhi iliyofuata, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikwenda kumuona binti yake. Baada ya kuwatembelea huku, yeye hakwenda tena nyumbani kwao kwa muda wa siku tatu, bali akaenda katika siku ya nne.22

Matakwa Ya Hadhrat Khadija (A.S.)

Katika ule usiku wa harusi ya Hadhrat Fatimah (a.s.), Asma bint Umais (au Umm Salama) ambaye alikuwa miongoni mwa wanawake hao, aliomba ruhusa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama angeweza kukaa karibu na Hadhrat Fatimah ili aweze kutekeleza mahitaji yoyote atakay- oweza kuwa nayo. Alimwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Wakati wa kifo cha Hadhrat Khadija ulipofika hapo Makkah, mimi nilikuwa karibu naye na niliona kwamba Khadija alikuwa analia.

Nilimuuliza: “Wewe ni ‘Bibi wa wanawake dunia zote’ na mke wa Mtume (s.a.w.w.) na licha ya yote hayo bado unalia ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu amekupa habari njema za peponi?”

Hadhrat Khadija alijibu: “Silii kwa sababu ya kifo; bali mimi ninalia kwa ajili ya Fatimah ambaye ni msichana mdogo, na wanawake katika usiku wa harusi wanahitaji mwanamke kutokana na ndugu zao na wale wa karibu (maharimu) watakaoweza kuwaambia wao siri zao zilizofichika, na nina- hofia kwamba usiku huo, kipenzi changu Fatimah hatakuwa na mmojawapo.”

Kisha nilimwambia Khadija kwamba: ‘Ninaapa kwa Mola wangu kwamba kama nitabakia kuwa hai mpaka siku hiyo, usiku huo mimi nitakaa ndani ya nyumba hiyo mahali pako (badala yako).’ Sasa ningeomba ruhusa kutoka kwako kwamba unisamehe ili niweze kutimiza ahadi yangu.’”

Baada ya kuyasikia haya, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alianza kulia na aka- nipa ruhusa kubakia na akaniombea Dua. 23

Suti Ya Harusi Yenyewe

Katika ule usiku wa harusi ya Imam Ali (a.s.) na Hadhrat Fatimah (a.s.), Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimpa binti yake suti (vazi) ya harusi ya kuvaa usiku ule. Wakati Hadhrat

Fatimah (a.s.) alipokuwa amekwenda kule kwenye nyumba ya harusi na pale alipokuwa ameketi kwenye mkeka wa kuswalia ili kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu mara akatokea mtu mwenye shida kwenye mlango wa nyumba ya Hadhrat Fatimah (a.s.) na kwa sauti kubwa akasema: “Kutoka kwenye mlango wa nyumba ya utume, mimi ninaomba suti ya zamani, chakavu.”

Kwa wakati ule, Hadhrat Fatimah (a.s.) alikuwa na suti mbili, moja iliyochakaa na nyingine bado mpya. Yeye alitaka kutoa ile suti ya zamani kulingana na maombi ya yule mtu mwenye haja wakati ghafla alipokum- buka aya inayosema: **“Humtapata uchamungu mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda mno…..”**24 Hadhrat Fatimah (a.s.) ambaye alijua kwamba anaipenda ile suti mpya zaidi, alifanya kulingana na aya hii na akatoa ile suti mpya kumpa yule mtu mwenye haja.

Siku iliyofuata, wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipoiona ile suti ya zamani mwilini mwa Hadhrat Fatimah (a.s.), yeye alimuuliza: “Kwa nini hukuvaa ile suti mpya?”
Hadhrat Fatimah akajibu: “Niliitoa kumpa mtu mwenye haja.” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Kama ungevaa ile suti mpya kwa ajili ya mumeo ingekuwa vizuri na yenye kufaa sana.” Hadhrat Fatimah (a.s.) ali- jibu akasema: “Hili nimejifunza kutoka kwako.

Wakati mama yangu Khadija alipokuja kuwa mke wako, alitoa utajiri wake wote kwenye mkono mtupu uliokuwa kwenye njia yako, ilikuwa haina kitu, hadi ikafikia mahali wakati alipokuja mtu mwenye shida kwenye mlango wa nyumba yako na kuomba nguo. Kukawa hamna nguo ndani ya nyumba yako hivyo ukavua shati lako na ukampatia yeye, na ndipo ikashuka aya hii: **“Wala usiufanye mkono wako kama uliofungwa shingoni mwako, wala usiukunjue kabisa, usije ukakaa hali ya kulaumiwa (na) kufilisika ukajuta.”**25

Akiwa amezidiwa na mshangao kwa upendo na uaminifu wa binti yake Zahraa (a.s.), Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yalimdondoka machozi kutoka machoni mwake, na kama ishara ya upendo, yeye alimshikilia Hadhrat Fatimah (a.s.) kifuani kwake (s.a.w.w.).26

1. A Bundle of flowers, Uk. 149
2. Muntakhab Mizan al-Hikmah, Jz.. 1, Uk.457
3. Kitab al-Irshad, Jz. 1, Uk. 270
4. Halliyatul-Muttaqin, uk. 116-117
5. Al-Kafi, Jz. 3, uk. 481
6. Al-Kafi, Jz. 5, uk. 500
7. Al-Kafi, Jz. 5, Uk. 501
8. Wasail ash-Shi’a, Jz. 20, Uk. 249, hadithi ya 25555
9. Halliyatul-Muttaqin, uk. 108-109 (nukta ya 1-3)
10. Pasukh be Masa’il-e Jinsii wa Zanashuii, Uk.235
11. Wasa’il ash-Shi’a, Juz. 20, Uk. 250 hadithi ya 25556
12. Bihar al-Anwar, Juz. 43, Uk.. 120 na 129
13. Bihar al-Anwar, Juz. 43, Uk.. 92
14. Baadhi wamesimulia kwamba ule wakati baina ya ndoa na harusi kuwa ni mwaka mmoja)
15. Bihar al-Anwar, Juz. 43, Uk. 130-131
16. Takriban ratili 8
17. Bihar al-Anwar, Juz. 43, Uk 137
18. Bihar al-Anwar, Juz. 43, Uk 106 na 114
19. Manaqib ibn Shahr Ashub, Juz.3, Uk. 354
20. Izdawaaj Maktab Insaan Saazi, Juz. 2, Uk. 300

21. Manaqib ibn Shahr Ashuub, Juz. 3, Uk. 3554-355
22. Manaqib ibn Shahr Ashuub, Juz. 3, Uk. 356
23. Sar Guzashthaaye Hadhrat Ali (a.s.) wa Fatimah (a.s.), Uk.30
24. Surat al-Imran; 3:92
25. Surat al-Isra; 17:29
26. Sar Guzashthaaye Hazrat Ali wa Fatimah (a.s.), uk. 31

Mlango Wa 2: Taratibu Za Kujamiiana Katika Uislam

Kujamiiana na mahusiano ya kijinsia, pamoja na mwenza halali yanatawaliwa na maumbile asilia, na wakati huo huo ni sunnah ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Ahlul-Bayt wake (a.s.). Yametajwa pia kwamba ndio jambo la kuburudisha zaidi maishani. Kikundi cha marafiki na Shi'a wa Imam as-Sadiq (a.s.) wanasimulia kwamba, Imam alituuliza sisi: "Ni nini kinachoburudisha zaidi?" Sisi tukasema: "Kuna vitu vingi vinavyoburudisha." Imam akasema: "Kile kinachoburudisha zaidi hasa ni kufanya mapenzi na wake zenu."1

Imesimuliwa vilevile kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): "Ama katika dunia hii au katika akhera, mtu hajawahi, na wala hatawahi, kupata starehe yenye burudani zaidi kuliko mahusiano ya kijinsia na wanawake, na hakika haya ndio maelezo ya maneno ya Allah (s.w.t.). ndani ya Qur'an, katika Surat Aali Imran, aya ya 14 Yeye ambapo anasema: **"Watu wamepambiwa kupenda matamanio pamoja na wanawake na watoto....."**

Halafu yeye akasema: "Hakika, watu wa Peponi hawapendelei sana katika starehe za Pepo zaidi kuliko Nikah;2 si chakula wala vinywaji ambavyo vina buru- dani kama hiyo kwao."3

Na kuhusu hali nyingine zote za maisha yetu, Uislam unatoa kutupatia sisi taarifa zote muhimu kwa ajili ya maisha ya kijinsia ya mwanaume na mwanamke. Sababu ya hili ni rahisi; Uislam unatambua hulka ya kimaumbile ya mwanadamu, na umeamuru mahusiano ya kijinsia kwa ajili ya starehe na sio kwa ajili ya kuzaa tu. Matamanio ya ngono hayawezi, na hayapaswi kuzuiwa, bali hasa kurekebishwa kwa ajili ya hali njema ya mtu katika ulimwengu huu na akhera. Endapo kanuni na sheria hizi zitazingatiwa kwa makini na kutekelezwa kwa lengo la burudani na kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kujitenga mbali na maovu ya Shetani, kunahesabiwa kuwa miongoni mwa wema mkubwa kabisa.

Umuhimu Wa Mahusiano Ya Kijinsia

Kuna hadithi nyingi sana zinazobeba ule umuhimu wa uhusiano wa kijin- sia. Una kituo cha ibada na sadaka, na umeitwa kuwa ni *Sunnah* ya Mtume (s.a.w.w.).

Imam as-Sadiq (a.s.) anasimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alizungumza na mmoja wa masahaba zake katika siku moja ya Ijumaa na akamuuliza: "Je, umefunga leo?" Yule sahaba akajibu. "Hapana." Mtume (s.a.w.w.) akamuuliza tena: "Je, umetoa chochote leo kama sadaka?" Akajibu, "Hapana." Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akamwambia: "Basi nenda kwa mke wako na hiyo ndio sadaka hasa kwake yeye."4
Katika hadithi nyingine, Imam as-Sadiq (a.s.) anasimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)

alimwambia mtu mmoja: “Wewe umefunga leo?” Akajibu akasema, “Hapana.”

Mtume (s.a.w.w.) akamuuliza: “Je, umekwenda kutembelea mgonjwa yoyote?” Akajibu, “Hapana.” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akamuuliza: “Je, umekwenda kusindikiza jeneza?” Akajibu, “Hapana.” Mtume (s.a.w.w.) akamuuliza: “Je, umetoa chakula kwa mtu masikini?” Akatoa majibu ya kinyume tena. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akamwambia: “Nenda kwa mke wako, na kumwendea mke wako ni sadaka (Mwendee ili upate malipo kwa ajili ya matendo yote hayo).”5

Muhammad bin Khalad anasimulia kutoka kwa Imam ar-Ridhaa (a.s.): “Mambo matatu ni kutoka kwenye sunnah za manabii watukufu na mitume wa Allah (s.w.t.)., na haya ni kutumia manukato, kukata nywele na kijiingiza sana kwenye mahusiano ya ndoa na wake zao.”6

Kukaa mbali na mahusiano ya kindoa ya mtu na mke wake ni matokeo ya minong’ono ya Shetani, na kuna matokeo ya kinyume mengi sana kama vile mabishano na chuki baina ya mume na mke wake.

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): Mabibi watatu walikwen- da kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kulalamika. Mmoja wao akasema: “Mume wangu huwa hali nyama.” Yule mwingine akasema: “Mume wangu hanusi manukato na wala hatumii manukato.” Na yule wa tatu akasema: “Mume wangu mimi hasogei karibu na wanawake (yaani, hajishughulishi na kujamiiana).”

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), akiwa hana furaha, katika namna ambayo kwamba joho lake lililobarikiwa lilivyokuwa likiburuzika ardhini, aliondoka na kwenda msikitini na akiwa juu ya mimbari, alimtukuza Mwenyezi Mungu na kisha akasema: “Ni nini kimetokea, kwamba kikundi cha wafuasi wangu hawali nyama, au hawatumii manukato, au hawawaendei wake zao? Ambapo mimi ninakula nyama, ninatumia manukato, na pia ninamwendea mke wangu. Hii ndio sunnah yangu, na mtu yoyote anayekwenda kinyume na sunnah hii huyo hatokani na mimi.”7

Imam as-Sadiq (a.s.) vilevile amesimulia: Mke wa Uthman bin Ma’dhun alikwenda kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kila siku Uthman anafunga na wakati wa usiku anajishughulisha katika Swala.” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akaokota makubazi yake na kwa hasira akaenda kwa Uthman (kiasi kwamba hakun- goja kuvaa makubazi yake) na akamkuta katika hali ya Swala.

Kwa vile Uthman alimuona Mtume (s.a.w.w.) aliiacha Swala yake. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akamhutubia akasema: “Allah hakunituma mimi kuwa sufii (anayejitenga peke yake), ninaapa Wallahi, kwamba hilo limenichochea mimi kwenye dini hii safi, yenye imani halisi na rahisi, mimi ninafunga, ninaswali na ninakwenda kwa mke wangu, na yeyote anayependa desturi yangu, ni lazima ashikamane na sunnah yangu na mwenendo wangu, na *Nikah*8 ni sunnah yangu.9

Umuhimu Wa Kumridhisha Mke Wako

Kumridhisha mke wake mtu ni jambo muhimu sana katika Uislam, kama lilivyoonyeshwa na hadithi ifuatayo hapo chini; kwa kweli, kukosa kuridhika kwa kipindi cha muda mrefu kunaweza kusababisha kukosa ashiki na chuki ya mke kwa mumewe.

Imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.): Wakati yeyote kati yenu anapotaka kulala na mke

wake, basi asimharakishe kwani wanawake wanayo mahitaji pia.10 Ni muhimu kwa mume kutambua kwamba hamu ya kujamiiana ya mwanamke inachukua muda mrefu kujionyesha yenyewe, lakini mara inapokuwa imevutika, inakuwa na nguvu sana, ambapo kwa mwanaume ni rahisi, anapata ashiki haraka sana na vilevile anaweza kuridhishwa haraka sana.
Mwisho, inatia moyo kuona kwamba umuhimu uliowekwa na Uislam juu ya kuridhika kwa wote, mwanaume na mwanamke ni kiashirio cha wazi cha uadilifu na wema wa Mwenyezi Muntu (s.w.t.), kwa kweli, imerudia kukaririwa ndani ya Qur'ani kwamba mwanaume na mwanamke waliumbwa kutokana na nafsi moja,11 na huu ni mfano mmoja tu wa hili.

Vitendo Vilivyopendekezwa

Hakuna kanuni maalum kwa ajili ya kujamiiana; chochote ambacho kinawaridhisha wawili hao ni sawa, kadhalika, chochote ambacho hakiwaridhishi wawili hao ni lazima kiepukwe; kikwazo pekee kwenye kanuni hii ni kile ambacho Shari'ah inakikataza kwa uwazi kabisa. Hata hivyo, kuna vitendo kadhaa vilivyopendekezwa ambavyo, kama vikifuatwa, vitatarajiwa kuongozea kwenye hali ya kuridhisha zaidi.

Kabla Ya Kujamiiana

1. Piga mswaki meno yako na tafuna kitu chenye harufu nzuri ili kuondoa harufu mbaya yoyote mdomoni. Kadhalika, jaribu kutokula vyakula vyenye harufu isiyopendeza kabla ya kukutana pia, kama vile kitunguu na kitunguu saumu.

2. Hakikisha unanukia vizuri – harufu safi zaidi ni ile ya mara tu baada ya kuoga au kujisafisha kwa haraka, na harufu mbaya zaidi ni ile ya jasho! Hususan wanawake wanahisia kali sana juu ya harufu.

Matumizi ya manukato, mafuta mazuri na vitu kama hivyo vinapendekezwa sana, ingawa ni muhimu sana kutambua kwamba kutumia vitu vya asili ni bora sana, ambavyo havina mchanganyiko na kemikali ambazo zinaweza kusababisha madhara mwilini.

Hasa, wanja (*kuhl*) umependekezwa sana juu ya wanawake. Imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.): "Kupaka wanja kuyazunguka macho kunakipa kinywa harufu nzuri, na kunazifanya kope za macho kuwa na nguvu na kunaongeza nguvu na mvuto wa kujamiiana.12

Imesimuliwa pia kutoka kwa Imam as-Sadiq (s.a.): Kupaka wanja nyakati za jioni kuna manufaa kwenye macho na nyakati za mchana ni katika sunnah.13

Jalizo: Ingawa hadithi zinapendekeza matumizi ya wanja (*kuhl*), haziruhusu matumizi yake katika maeneo ambayo yanaweza kuonekana kwa wanaume na yakaweza kuwa chanzo
cha mvuto na ushawishi.

Unyegereshano (Kutiana Ashiki)

Umuhimu Wa Unyegereshano

Kama ilivyosisitiziwa mapema, mume kumridhisha mke wake ni muhimu sana, na kujiingiza kwenye kujamiiana haraka na kwa pupa sio njia sahihi. Kuna wastani wa tofauti ya dakika nane kati ya muda ambao mume na mke wanafikia kileleni; mwanaume kwa kawaida

anachukua dakika mbili kufikia kileleni na mwanamke anachukua dakika kumi kufikia kileleni. Kwa hiyo, ili kumridhisha kikamilifu mke wake, mwanaume lazima ampapase na kumchezea kimapenzi na kujishughulisha katika kunyegereshana (kutiana ashki) ili wote wafikie kileleni kwa pamoja kwa wakati mmoja.Uislam unatilia mkazo sana umuhimu wa unyegereshano, kama unavyoashiriwa katika hadithi zifuatazo hapa chini:

Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Usijishughulishe katika kujamiiana na mkeo kama kuku; bali kwanza kabisa jishughulisha katika kutiana ashiki kwa unyegereshano pamoja na mke wako na kuchezeana naye halafu ufanye mapenzi naye.”14

Imesimuliwa pia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Starehe na michezo yote haina maana isipokuwa kwa mitatu tu: Upanda farasi, kurusha mishale na unyegereshano na mke wako, na hii mitatu ni sahihi.”15

Imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.): “Yeyote anayetaka kuwa karibu na mke wake lazima asiwe na papara, kwa sababu wanawake kabla ya kuji- ingiza kwenye tendo la kufanya mapenzi lazima wajiingize kwenye unyegereshano ili kwamba wawe tayari kwa ajili ya kufanyiwa mapenzi.16

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Malaika wa Mwenyezi Mungu na wale ambao ni mashahidi juu ya matendo yote ya wanadamu wanawaangalia katika kila hali isipokuwa wakati wa mashindano ya kupanda farasi na ule wakati ambapo mwanaume anajiingiza katika kujishughulisha na unyegereshano na mke wake kabla hawajajihusisha katika kujamiiana.” 17

Taratibu Za Kunyegereshana

Kuna vikwazo vichache sana kwenye taratibu zinazotumika katika unyegereshano; kupigana mabusu, kukumbatiana na kadhalika yote haya yanaruhusiwa. Hapa chini ni baadhi ya mbinu zinazofaa kwenye taratibu maalum:

A) Upapasaji Kwenye Matiti

Imesimuliwa kutoka kwa Imam ar-Ridhaa (a.s): “Usijiingize kwenye kujamiiana isipokuwa kwanza ujishughulishe katika unyegereshano, na ucheze naye mkeo sana na kumpapasa matiti yake, na kama ukifanya hivi atazidiwa na ashiki (na kusisimka kwa upeo kamilifu) na maji yake yat jikusanya. Hii ni ili ule utoaji wa majimaji uchomoze kutoka kwenye mati- ti na hisia zinakuwa dhahiri usoni mwake na kwenye macho yake na kwamba anakuhitaji kwa namna ileile kama wewe unavyomhitaji yeye.” 18

B) Mapenzi Ya Mdomo (Maongezi)

Imam al-Kadhim (a.s.) aliulizwa: “Kuna tatizo kama mtu atabusu sehemu za siri za mke wake?” Imam alijibu akasema: “Hakuna tatizo.”19

DOKEZO: Ingawa kupiga punyeto (kujisisimua mwenyewe uchi wako mpaka ukatoa manii) kunakatazwa, katika suala la watu waliooana hakuna tatizo kama mke anasisimua tupu ya mume wake mpaka kutokwa na manii, au mume anasisimua tupu ya mke wake hadi anafikia kilele cha raha ya kujamiiana. Hili linaruhusiwa kwa sababu haliingii kwenye (kujisisimua mwenyewe;) ni kujisisimua kwa njia ya mwenza halali

C) Mengineyo

Iliulizwa kwa Imam as-Sadiq (a.s.) “Endapo mtu atamvua nguo mke wake (na kumuacha uchi) na halafu akawa anamwangalia, je kuna tatizo lolote katika hilo?” Yeye akajibu akasema: “Hapo hakuna tatizo, hivi kuna stare- he bora kuliko hiyo ambayo inaweza kupatikana?” Likaulizwa swali jingine tena: “Kuna tatizo lolote iwapo mume atachezea sehemu za siri za mke wake?”

Imam akajibu: “Hakuna tatizo, kwa sharti kwamba hatumii kitu chochote mbali na viungo vya mwili wake (asitumie kitu cha nje cha ziada).”

Halafu tena Imam akaulizwa: “Kuna tatizo lolote kufanya ngono ndani ya maji?”
Imam akajibu: “Hakuna tatizo.” 20

Dokezo: Hadithi hiyo hapo juu inasisitizia makatazo ya kutumia vitu vya nje.

Baada Ya Kujamiiana

1. Ni mustahabu kwamba josho la janaba ‘*Ghusl al-Janaabat*’ linafanywa mara tu baada ya tendo la ndoa, na linapochukuliwa mapema zaidi ndio bora. Vilevile, kama mtu angependa kufanya ngono zaidi ya mara moja katika usiku mmoja, ni bora kwamba kila mara waoge josho la janaba. Hata hivyo, kama hilo litakuwa haliwezekani kutendeka, inapendekezwa kwamba mtu atawadhe kabla ya kila tendo.21

2. Mara tu baada ya kumaliza tendo la ngono, mume hana budi kuoga josho na wakati huohuo ale sehemu ya nta ya nyuki (inayosifika kwa kuponya aina zote za majeraha, hususan mipasuko na mivunjiko) iliyochanganywa na asali na maji au iliyochanganywa na asali safi, halisi, kwani hii itafidia yale majimaji yaliyopotea.22

3. Kama nguvu za kiume za mtu zikiisha haraka baada tu ya kujamiiana, hana budi kujipasha mwili moto na kisha kulala.23

4. Mume na mke hawana budi kutumia mataulo tofauti katika kujisafisha wenyewe. Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba kama litatumika taulo moja tu, hii itasababisha uadui na utengano baina ya wawili hao.24

Vitendo Visivyopendekezwa

Vitendo Vinavyoleta Karaha (Makruuh)

1. Liwati!

Kuna baadhi ya Wanavyuoni wanaosema kuwa Liwati inaruhusiwa kwa ridhaa ya mke, lakini ni kauli zisizo na nguvu, na pia ni kitendo kinachochukiwa sana!

Zayd ibn Thabit anasimulia kwamba mtu mmoja alimuuliza Imam Ali (a.s.): “Je, unaweza kumsogelea mkeo nyuma kwake?” Imam Ali (a.s.) akajibu akasema: “Likatae, lichukie hilo liwe kinyaa kwako! Mwenyezi Mungu anakushusha kwa njia hii (ya kumwingilia mwanamke). Hukuyasikia maneno ya Mola Wako kwamba imesimuliwa kutoka kwa Lut ambaye alisema kuwaambia kaumu yake:

وَلُوطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ أَتَأْتُونَ الْفَاحِشَةَ مَا سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ أَحَدٍ مِنَ الْعَالَمِينَ {80}

"Kulikoni! Mnafanya uchafu ambao hajakutangulieni yeyote kwa (ufasiki) huo katika walimwengu? (Al-A'araf; 7:80). 25

Kuna baadhi ya watu wanaolihalalisha tendo hili kwa kutumia aya ya Qur'ani Tukufu ifuatayo:

نِسَاؤُكُمْ حَرْثٌ لَكُمْ فَأْتُوا حَرْثَكُمْ أَنَّىٰ شِئْتُمْ {223}

"Wanawake ni mashamba yenu, basi yaendeeni mashamba yenu kwa namna muitakayo …"
(Al-Baqarah; 2:223).

Hata hivyo, Imam as-Sadiq (a.s.), katika tafsiri yake juu ya aya hiyo ya Qur'ani hapo juu anasimulia kwamba: "Madhumuni ya aya hii ni kwamba kujamiiana hakuna budi kufanyika kutokea mbele, kwani sababu ambayo kwamba mwanamke katika aya hii amefananishwa na shamba linalotoa mavuno (kutokea juu ya udongo) ambao ni kama tu kule mbele kwa mke kwa sababu huku ndiko ambako kwamba mtoto hutokea kupatikana na kuja ulimwenguni humu."26
Abuu Basiir anasimulia kwamba yeye alimuuliza Imam kwamba ni nini hukmu ya mtu anayemwendea mke wake nyuma. Imam alilichukulia tendo hili kutokubalika na akasema: "Kaa mbali na nyuma kwa mkeo, na maana ya aya hii tukufu ya Surat al-Baqarah hapo juu sio kwamba unaweza kumwingilia mkeo kutokea popote unapotaka, bali haswa ni kwamba huna budi kufanya ngono, na kwa hiyo maana ya aya hiyo ni kumkurubia mkeo kwa wakati wowote uupendao kufanya hivyo."27

2. Kuwa Na Qur'ani Au Majina Ya Allah (S.W.T.) Mwilini Mwako

Imesimuliwa kutoka kwa Ali, mtoto wa Imam as-Sadiq (a.s.): Nilimuuliza ndugu yangu Imam Kadhiim (a.s.): "Je, mtu anaweza kujamiiana na akaenda bafuni wakati akiwa na pete mkononi mwake yenye jina la Allah au aya ya Qur'ani iliyoandikwa juu yake?" Imam alijibu akasema: "Hapana – hilo ni makuruhu."28

3. Kufanya Mapenzi (Ngono) Kwa Kusimama Wima

Inasimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Mume na mke wasije wakajamiiana kama punda wawili waliong'ang'aniana pamoja, kwa sababu kama ikiwa namna hiyo, malaika wa rehma watakaa mbali nao na neema ya Mwenyezi Mungu itaondolewa kutoka kwao.29

4. Kujamiiana Wazi (Bila Kujifunika Nguo)

Imesimuliwa kwamba Muhammad ibn al-Ais alimuuliza Imam as-Sadiq (a.s.): "Je, inaruhusiwa kumwendea mke wangu nikiwa uchi kabisa (yaani kujamiiana bila kujifunika)?"

Imam alijibu akasema: “Hapana, usifanye jambo kama hilo.....”30

5. Kushughulika Na Ngono Chini Ya Anga

Imesimuliwa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.): “Allah anazichukia tabia 24 kwa ajili yenu, enyi watu, na amekukatazeni kutokana nazo; moja ya tabia hizi ni kujamiiana chini ya anga.”31

6. Kushughulika Na Kujamiiana Panapokuwa Na Watu Wengine (Na Wanaweza Kuwasikia Na/Au Kuwaona) Ndani Ya Nyumba

Imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.): “Ni makuruhu kwamba mtu ashughulike katika kujamiiana na mke wake kama, pamoja na kuwepo kwao, kuna mtu mwingine pia ndani ya nyumba hiyo.32

Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Twaeni tabia tatu kutoka kwa kunguru; kujamiiana kwa siri, kwenda kutafuta riziki mwan- zoni mwa asubuhi, na akili na hadhari dhidi ya hatari zinazoweza kujitokeza.” 33

7. Kujishughulisha Na Kujamiiana Mbele Ya Mtoto Mdogo

Imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.): “Mtume amekataza kwamba mtu amwendee mke wake (kwa ajili ya kujamiiana) na mtoto katika susu lake anaweza kuwaona. 34

Imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.): “Epukana na kujamiiana katika sehemu ambayo panaweza kuwa na mtoto anayeweza kuwaoneni.35

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Jiepushe na kwenda kulala (kwa ajili ya kujamiiana) na mke wako wakati ambapo mtoto anaweza kuwaoneni, kwani Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alijua sana hasa kwamba kitendo hiki ni Makruhu na cha kuaibisha sana.”36

8. Kushughulika Na Kujamiiana Ndani Ya Jahazi, Ufukweni 63Au Barabarani

Imesimuliwa katika hadithi kwamba kujamiiana ndani ya jahazi au barabarani kunaishia kwenye laana ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ya Malaika kuwa juu yako mtu.37

Imesimuliwa katika hadithi nyingine kutoka kwa as-Sakuni kwamb Imam Ali (a.s.) aliwapita wanyama wawili waliokuwa wakijamiiana mahali njia ya watu wengi. Imam aligeuka mbali nao.

Ikaulizwa: “Ewe Amirul-Mu’minin, kwa nini uligeukia pembeni mbali nao?” Imam (a.s.) akajibu akisema: “Sio sahihi kwamba mkaribiane katika njia ya watu kama wanyama hawa; kitendo kama hicho kimekatazwa na kifanyike mahali ambapo si mwanaume au mwanamke awezaye kuona.” 38

9. Kuelekea, Au Mtu Kukipa Mgongo Qiblah

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amekataza watu kujamiiana wakati wakiwa wameelekea Qiblah, au mtu mgongo wake kuelekea Qiblah, na amesema kwamba endapo kitendo kama hicho kikifanyika, kinaleta matokeo ya laana ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na Malaika na wanadamu wote kuwa juu yako mwenye kufanya hivyo.39

Dokezo: Ikiwa pale unapokaa wima kutoka kwenye hali ya kulala, uso wako unaelekea

Qiblah, hii inafahamika kama kuelekea Qiblah, na kinyume chake (yaani na mgongo pia).

10. Kukataa Kujamiiana (Kwa Sababu Mbalimbali)

Imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.): Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema kuwaambia wanawake: “Msirefushe Swala zenu kiasi kwamba ikawa ni kisingizio cha kutokwenda kulala (kwa ajili ya kujamiiana) na waume zenu.”40

Nyakati Zinazopendekezwa

Nyakati Za Wajibu

1. Ikiwa Kuna Hofu Ya Haramu (Iliyokatazwa)

Endapo mtu anahofia kwamba anaweza kushindwa na tamaa zake za kingono na minong’ono ya Shetani na akaweza kujiingiza katika vitendo vya haramu, ni wajibu kwamba wajichunge na wajilinde nalo hili.41

Kama mtu yuko peke yake, ni lazima afunge ndoa na hivyo kujiweka mbali na vitendo vyovyote vinavyowezekana kuwa vya haramu (vilivyokatazwa).

Imesimuliwa kutoka kwa Ayatullah Khomeini (r.a.) “Ni faradhi kwa mtu ambaye, kwa sababu ya kutokuwa na mke ataangukia kwenye haram, afunge ndoa.” 42

2. Mara Moja Kwa Kila Miezi Minne

Mtu ni lazima apate kujamiiana na mkewe kijana angalau mara moja katika miezi minne. Hii ni moja ya haki za ndoa za mke na wajibu huo unabaki kufanya kazi isipokuwa ima kama una madhara kwa mume, unahusika na kutumia jitihada za ziada zisizo za kawaida, au mke kusamehe haki yake au masharti ya awali kama hayo yalikuwa yamewekwa na mume wakati wa kufunga ndoa. Haina tofauti kama mume yuko mbali safarini ama yupo nyumbani.

Safwan ibn Yahya alimuuliza Imam ar-Ridhaa (a.s.): “Mtu anaye mke kijana na akawa hajamkaribia kwa kiasi cha miezi, au hata mwaka. Sio kwa sababu anataka kumtaabisha yeye (kwa kukaa mbali naye), bali hasa ni janga fulani limewashukia. Je, hili linahesabiwa kama ni kosa?”

Imam akajibu akasema: “Endapo atamwacha kwa kiasi cha miezi minne, hilo linahesabiwa kama
ni dhambi.”43

Nyakati Zinazopendekezwa (Mustahab)

Kujamiiana, kama kutafanywa katika namna inayoruhusiwa, basi wakati wote kunakuwa ni mustahabu. Hata hivyo, kuna nyakati ambazo kunapendekezwa zaidi.

1. Wakati mke anapokuhitaji kutoka kwa mumewe.
2. Wakati mume anapokuwa amevutiwa na mwanamke mwingine.44

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) “Mtu yoyote atakayeona mwanamke na akavutiwa naye ni lazima aende kwa mke wake na aka- jamiiane naye, kwa sababu kile

ambacho yule mwanamke mwingine ana- cho, na mke wako pia anacho, na mtu asimwachie nafasi Shetani katika moyo wake.

Na endapo mtu hana mke, ni lazima aswali Swala ya rakaa mbili, amtukuze sana Allah (s.w.t.). na kumswalia Mtume – kumtakia rehma yeye na kizazi chake na amuombe Mwenyezi Mungu amjaalie kumpa mke muumini na mchamungu, na kwamba Yeye Allah (s.w.t.). amfanye asiwe mwenye kuhitaji yaliyoharamishwa.45

Nyakati Zisizopendekezwa

Nyakati Haram – Zinazokatazwa

1. Wakati wa heidhi (siku za mwezi za mwanamke):

Allah (s.w.t.). anaeleza ndani ya Suratul-Baqarah, aya ya 222 kama ifuatavyo:

وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الْمَحِيضِ ۖ قُلْ هُوَ أَذًى فَاعْتَزِلُوا النِّسَاءَ فِي الْمَحِيضِ ۖ وَلَا تَقْرَبُوهُنَّ حَتَّىٰ يَطْهُرْنَ ۖ {222}

"Na wanakuuliza juu ya hedhi. Waambie: Huo ni uchafu, basi jitengeni na wanawake (wakiwa) katika hedhi. Wala msiwaingilie mpaka watakapotoharika …..” (Al-Baqarah; 2:222).

Endapo mtu anayejamiiana na mke wake akagundua kwamba kipindi chake cha hedhi kimeanza, basi na ajiondoe na kujitenga naye mara moja.

Ndani wa kipindi cha hedhi, vitendo vingine, mbali na kujamiiana vinaruhusiwa kufanyika kama inavyoonyeshwa na hadithi ifuatayo hapa chini:

Mu'awiyah ibn Umar anasimulia kwamba, yeye alimuuliza Imam as-Sadiq (a.s.): "Ni nini kinachoruhusiwa kwa mwanaume wakati mwanamke anapokuwa kwenye hali ya hedhi?" Imam akajibu akasema: "Mbali na sehemu zake za siri (yaani, mwili wote uliobakia isipokuwa sehemu zake za siri tu). 46

Imran ibn Qanzali anasimulia kwamba yeye alimuuliza Imam as-Sadiq (a.s.): "Ni vipi mwanaume anavyoweza kufaidika kutoka kwa mwanamke ambaye yuko kwenye hali yake ya hedhi?" Imam akajibu akasema: "Yale mapaja mawili (ya mwanamke huyo)." 47

Hata hivyo, ingawa mwili wote uliobakia, wa mwanamke (ukiachilia mbali sehemu zake za siri) unaruhusiwa kwa mume, lile eneo tokea kitovuni hadi magotini ni makuruhu (haipendekezwi kufikiwa);48 kwa hiyo inashauriwa sana kwamba mume azikwepe sehemu hizi vile vile.

Ni muhimu kutambua kwamba haipendekezwi kujishughulisha na ngono baada ya kwisha kwa hedhi. Hata hivyo, kama ni lazima, mwanamke anapaswa kuoga kwanza.49

Mwenyezi Mungu analieleza hili katika muen- delezo wa aya hiyo hapo juu: "**Na wanapokuwa tohara, basi waingilieni kama alivyokuamuruni Mwenyezi Mungu."**

(Al-Baqarah; 2:222).

2. Wakati wa Nifaas 50

3. Wakati wa kufunga katika mwezi wa Ramadhani.51

4. Wakati katika hali ya Ihraam na kabla ya kuswali swala ya *Tawafun Nisaa*.52

5. Pale ambapo inaweza kusababisha madhara makubwa kwa amma mwanaume au mwanamke. Kujamiiana kunaruhusiwa endapo hakuwezi kuleta madhara makubwa.53

Nyakati Makuruhu

1. Katika Hali Ya Ihtilaam

Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Ni Makruh kwamba mwanaume ambaye amekuwa *Muhtalim* (yaani, aliyekuwa katika hali ya janaba akiwa usingizini – kwenye ndoto) amwendee mkewe (ili kujamiiana naye) akiwa katika hali hii, isipokuwa pale atakapooga kwa ajili ya *ihtilaam* yake.”54

2. Wakati Wa Safari, Na Kukiwa Na Uwezekano Wa Kukosekana Maji

Imesimuliwa kutoka kwa Is’haaq ibn Ammaar: “Nilimuuliza Imam as- Sadiq (a.s.): “Mwanamume amefuatana na mke wake wakati wa safari, lakini hakupata maji yoyote kwa ajili ya kufanyia Josho. Je, anaweza kulala (kujamiiana) na mke wake?” Imam akajibu: “Hilo silipendi kama akifanya hivyo nalo ni makruh, isipokuwa kama akiwahofia kwamba kama hatakiendea kilicho halali yake, ataangukia kwenye kilichoharamishwa.”55

Imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Kadhim (a.s.): “Silipendi lile jambo la kwamba mtu anapokuwa safarini, ambaye hana maji halafu anajishughul- isha katika kujamiiana, isipokuwa kama anahofia madhara.” 56

(Katika hali kama hizi, kwa mujibu wa kanuni za Fiqhi, mtu anaweza kutayamman badala ya josho ili kuweza kuswali).

3. Usiku Wa Kupatwa Kwa Mwezi Na Mchana Wa Kupatwa Kwa Jua

Usiku mmoja, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa karibu na mmoja wa wake zake na jioni ili kukatokea kupatwa kwa mwezi, na hakuna lolote lililotokea baina yao. Mke wa Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Kwa nini huna furaha na mimi usiku wote wa leo?” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akajibu: “

Ni nini unachokisema, jioni hii ilikuwa ni usiku wa kupatwa kwa mwezi na mimi ninajua kuwa ni Makruh kwamba nipate starehe usiku huu, kwa sababu Mwenyezi Mungu anakikaripia kikundi cha watu wasiojali na wasio makini kwenye Hujja na ishara Zake, na amewaelezea katika namna ifuatayo:

وَإِنْ يَرَوْا كِسْفًا مِنَ السَّمَاءِ سَاقِطًا يَقُولُوا سَحَابٌ مَرْكُومٌ {44}

“Na kama wakiona kipande cha mbingu kikianguka husema: ni mawingu yanayobebana.”
(At-Tuur: 52:44) 57

4. Baina Ya Subh As-Sadiq (Adhana Ya Alfajir) Na Kuchomoza Kwa Jua Na Kati Ya Kuzama Jua Na Kutoweka Kwa Wekundu Wa Mbingu

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Kupata kuwa na janaba wakati wa wekundu wa jua linapochomoza na wekundu wa jua linapozama ni Makruh.”58

5. Wakati Wa Tetemeko La Ardhi (Na Matukio Mengine Yanayolazimu Kuswali Salat Al-Ayaat)

Imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.) kwamba: “Mtu ambaye haachi raha na starehe katika wakati wa Ishara za Mwenyezi Mungu zinapodhihiri, anatokana na wale watu ambao wamezichukulia ishara zake Mwenyezi Mungu kuwa ni kama mzaha.”59

Mwili Wenye Afya Njema

Mwili wenye afya njema hurusu kuwa na maisha ya uhusiano timamu wa kijinsia. Vitendo kadhaa vimependekezwa katika Uislam, na kama maelekezo haya yatafanyiwa kazi, yatasababisha kuwa na mwili safi na wenye afya njema.

Mambo Yanayopendekezwa:

Mambo Yanayopendekezwa: 60

1. Kusafiri

2. Kufunga swaumu

3. Kula zabibu kavu 21 kwenye tumbo tupu lenye njaa

4. Kunywa maji ya mvua. 61

5. Kuswali Swala ya usiku *Salaat al-Layl*.

6. Kuosha mikono kabla na baada ya kula.

7. Kujisaidia pale inapohitajika haja ya choo.

8. Kuosha miguu (nyayo) kwa maji baridi baada ya kuoga.

9. Kuulinda mwili kutokana na baridi ya majira ya kupukutika kwa majani ya miti bali sio kuukinga na baridi ya wakati wa majira ya kuchipua (yaani kuvaa nguo nzito wakati wa kupukutika na nyepesi wakati wa majira ya kuchipua).

10. Kupata kiwango cha kutosha cha mapumziko.

11. Kula binzari nyembamba (*aniseed*) na tende.

12. Kutafuna vyema chakula chako.

13. Kula chakula pale tu unapojisikia njaa na kuepuka kula wakati umeshiba.

14. Kula chakula kiwango cha kiasi na hivyo kunywa kiasi cha kadiri

Matumizi Ya Mafuta Ya Kuchulia

Matumizi Ya Mafuta Ya Kuchulia62

Hususan mafuta ya kuchulia ni yenye manufaa sana kwa mwili wenye afya njema na vilevile ashiki ya kujamiiana, kiasi kwamba Maimam (a.s.) wamesimulia hadithi juu ya jambo hili:

Imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.) kwamba: “Kuupaka mwili na mafuta ya kuchulia kunalainisha ngozi, kunaboresha hali, kunafanya mtiririko wa maji na vimiminika ndani ya mwili kuwa rahisi, kunaondoa zahama, makunyanzi, afya mbaya na ugumu wa kipato na kunaleta nuru kwenye uso.”63

Imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.) kwamba: “Kuupaka mwili mafuta ya kuchulia wakati wa jioni ni chanzo cha mzunguko katika mishipa ya damu na (hili) huipa nguvu tena hali ya ngozi na kung’arisha uso.”

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba: “Angalau mara moja kwa mwezi, au mara moja, mbili kwa wiki, pakaza mafuta kwenye mwili wako. Hata hivyo, kama wanawake wakiweza, ni lazima wajaribu kutumia mafuta kwenye miili yao kila siku.

Aina Za Mafuta Zifuatazo Zimependekezwa

1. Mafuta Ya Urujuani

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Mafuta ya urujuani ni mafuta ya nguvu: yasugue katika mwili wako ili yaweze kuondoa mau- mivu ya kichwa na macho.”

Mtu mmoja alianguka chini kutoka kwenye ngamia wake, na wakati maji yalipoanza kutoka kwenye pua yake, Imam as-Sadiq (a.s.) akamwambia: “Mwagia mafuta ya urujuani juu yake.” Yule mtu alipofanya hivyo, alitibika na akapona vizuri kabisa. Baada ya hapo Imam akasimulia: “Mafuta ya urujuani wakati wa kipupwe ni ya vuguvugu na wakati wa kiangazi ni yanakuwa poa kidogo64 kama watu wangeelewa yale maufaa ya mafuta haya, wangekunywa kiasi chake kikubwa; mafuta haya yanaondoa maumivu na kutibia na kuponya pua.”

2. Mafuta Ya Willow (Catkin)

Mtu mmoja alikuja kwa Imam as-Sadiq (a.s.) na kulalamika juu ya mikono na miguu iliyoatuka na kuwa na mikwaruzo. Imam akamwambia: “Chukua pamba, iloweke kwenye mafuta ya mti wa *willow* na uiweke hapo katikati (ya muatuko/mpasuko).” Yule mtu alipofanya kitendo hicho, yale maumivu yakatoweka.

3. Mafuta Ya Yungiyungi

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Mafuta ya yungiyungi yana tiba kwa magonjwa 70, na ni bora kama itakuwa yungiyungi nyeupe, ambayo inajulikana pia kama Jasmini ya Kiarabu.”

4. Mafuta Ya Zeituni

Kama mafuta ya zeituni yatachanganywa na asali na yakanywewa badala ya maji kwa muda wa siku tatu, yanaongeza nguvu ya kijinsia (za kujamiiana). Kama mafuta ya zeituni yatapakwa kwenye nywele, yanazuia zisikatike au kuota mvi nyeupe. Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Kula mafuta ya zeituni kunaongeza shahawa na nguvu ya uwezo wa kujamiiana.”65

Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Hasa kula mafuta ya zeituni kwa sababu dawa hii inatibia nyongo, inaondoa kikohozi, inaimarisha neva, inaponya maumivu, inafanya akhlaq kuwa nzuri, inafanya kinywa kunukia vizuri na inamuondolea mtu huzuni.”66

Imesimuliwa pia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Kula mafuta ya zeituni na yasugue mwilini, kwani yanatokana na mti uliobarikiwa.”67

Vile vile imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Mtu yoy- ote anayekunywa mafuta ya zeituni na kuyasugua mwilini mwake, Shetani hatamsogelea karibu yake kwa asubuhi arobaini.”

5. Mafuta Mengineyo

Mume na mke ambao wanataka kuongeza kiwango chao cha mshughuliko wa kujamiiana, lakini wakawa hawajui ni nini wanalazimika kukifanya, kadhalika watu ambao wangependa kufikia starehe zaidi ya kujamiiana, wanapaswa kutumia mafuta ya kuchulia kama vile zeituni ya Kiarabu, mafuta ya nazi, mafuta ya urujuani na mafuta ya zeituni.68

Mambo Yasababishayo Madhara Mwilini Kuhusiana Na Kujamiiana

1. Kujamiiana mwanzoni mwa usiku, iwe wakati wa kiangazi ama wa kipupwe, kunasababisha madhara kwenye mwili kwa sababu wakati huo tumbo na mishipa ya damu kwa kawaida inakuwa imejaa. Kujamiiana kunaweza kusababisha chango (msokoto wa tumbo bila kuharisha), kupooza (kwa uso), jongo (gout), mawe na kutiririka kwa mkojo, henia na udhaifu wa macho.69

Kwa hiyo, kushughulika katika kujamiiana mwishoni mwa usiku kunapendekezwa zaidi kwa ajili ya kudumisha mwili wenye afya njema, kwani kuna mwelekeo wa dhahiri kwamba wakati huo mtu hatakuwa na tumbo lililojaa.

2. Kadhalika, kujamiiana wakati wowote ule ukiwa na tumbo lililojaa ni kwenye madhara. Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba: “Mambo matatu huharibu mwili wa mtu, nayo haya ni pamoja na: kwenda kuoga ukiwa na tumbo lililojaa shibe, kujihusisha na ngono pamoja na mkeo ukiwa na tumbo lililojaa, na kujihusisha na kujamiiana na wanawake wazee, waliodhaifika na wenye umri mkubwa.”70

3. Kuzuia kumwaga manii kwa kurudia mara kwa mara kunaweza kus- ababisha matatizo kwa wanamume, na vile vile hata kwa wanawake.71

Kuimarisha Na Kudhoofisha Tamaa Ya Ngono

Vitu Vinayoongeza Tamaa Ya Ngono:

Vitu Vinayoongeza Tamaa Ya Ngono:72

1. Karoti
2. Vitunguu
3. Nyama
4. Mayai
5. Tikiti maji
6. Komamanga freshi
7. Maziwa halisi
8. Zabibu tamu
9. Mafuta ya ngano

10. Sehemu ya kati ya tende
11. Uvaaji wa viatu vya manjano
12. Kutumia mafuta ya kuchulia kwenye mwili
13. Kupakaza wanja (Kuhl) kwenye macho.

Vitu Vinavyohuisha Na Kuongeza Tamaa Ya Ngono

Vitu Vinavyohuisha Na Kuongeza Tamaa Ya Ngono 73

1. Asali
2. Majozi (*walnuts*)
3. Tende
4. Ndizi

Vitu Vinavyopunguza Tamaa Ya Ngono

Vitu Vinavyopunguza Tamaa Ya Ngono 74

1. Kuoga kwa kutumia maji baridi
2. Kutokula chakula cha wakati wa usiku

Imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Kadhim (a.s.): “Kama watu wakiwa na kadiri wakati wa kula vyakula vyao (yaani, wasile kupita kiasi au chini ya kiasi), miili yao wakati wote itakuwa na afya njema; na kamwe msiwache kula chakula cha jioni, hata kama itamaanisha kula vipande vilivyopukuti- ka vya mkate kwa sababu chakula hicho (cha jioni) ni chanzo cha nguvu ya mwili na nguvu ya kujamiiana.75

1. Wasa’ilush-Shi’a, Juz. 20, Uk. 23, namba 24927
2. Nikah kwa maneno halisi ina maana ya kujamiiana
3. Wasa’ilush-Shi’a; Juz. 20, Uk. 23, namba 24929
4. Wasa’ilush-Shi’a; Juz. 20, Uk. 109, namba 25163
5. Wasa’ilush-Shi’a; Juz. 20, Uk. 109, namba 25163.
6. Wasa’ilush-Shi’a; Juz. 20, Uk. 241, namba 25537
7. Wasa’ilush-Shi’a; Juz. 20, Uk. 107, namba 25158
8. Nikah ina maana ya kuingiliana (na mkeo).
9. Wasa’ilush-Shi’a; Juz. 20, Uk. 106, namba 25157
10. Wasa’ilush-Shi’a; Juz. 20, Uk 118, namba 25184
11. Suratun-Nisaa; 4:1, Surat al-Zumar; 39:5, Surat Luqman; 31:28, Suratun-Nahl; 16:72
12. Halliyatul-Muttaqin, Uk. 91
13. Niyaazha wa Rawabith Jinsi wa Zanashui, Uk 38

14. Halliyatul-Muttaqiin, Uk. 110
15. Wasa’ilush-Shi’a, Juz. 20, Uk.118, namba 25186
16. Halliyatul-Muttaqiin, Uk. 115
17. Ibid., Juz. 20, uk. 188, namba 25185
18. Mustadrak al-Wasaa’il, Juz. 2. Uk.545
19. Niyazha wa Rawabith Jinsii wa Zanashuii, Uk. 55
20. Halliyatul-Muttaqiin, Uk. 111
21. Niyazha wa Rawabith Jinsii was Zanaashuii, Uk. 52
22. Tib wa Behdaasht, Uk. 200
23. Niyazha wa Rawabith Jinsii was Zanaashuii, Uk. 24
24. Halliyatul-Muttaqiin Uk. 112.
25. Wasa’ilush-Shi’a, Juz. 20, Uk. 144, namba 25258
26. Wasailush-Shi’a, Juz. 20, Uk. 134, numba 25253
27. Wasailush-Shi’a, Juz. 20, Uk. 147, namba 25266
28. Wasailush-Shi’a, Juz. 20, Uk. 148, namba 25271
29. Ibid., Juz. 20, Uk. 120, namba 25190
30. Ibid., Juz. 20, Uk. 137, namba 25238, na uk. 138, namba 25239
31. Niyazha wa Rawabith Jinsii was Zanaashuii, Uk. 61
32. Wasailush-Shi’a, Juz. 12, Uk. 380, namba 16565
33. Wasailush-Shi’a, Juz. 20, Uk. 133, namba 25227
34. Wasailush-Shi’a, Juz. 12, Uk. 382, namba 16568
35. Wasailush-Shi’a, Juz. 20, Uk. 134, namba 25229
36. Wasa’ilush-Shi’a, Juz. 20, Uk. 132, namba 25222
37. Ibid., Juz. 20, uk. 138, namba 25240
38. Ibid., Juz. 20, Uk. 133, namba 25226
39. Ibid., Juz. 20, Uk. 138, namba 25240
40. Wasa’ilush-Shi’a, Juz. 20, Uk. 164, namba 25317
41. Hili limethibitishwa pamoja na ofisi ya Ayatullah Sistanii, Qum
42. Niyaazhaa wa Rawabith Jinsii was Zanaashuii, uk. 71
43. Wasa’ilush-Shi’a, Juz. 21, Uk. 458 namba 27573
44. Niyaazhaa wa Rawabith Jinsii was Zanaashuii Uk k. 71
45. Niyaazhaa wa Rawabith Jinsii was Zanaashuii, Uk. 48-49
46. Wasa’ilush-Shi’a, Juz. 2, Uk k. 321, hadith namba 2249
47. Wasa’ilush-Shi’a, Juz. 2 Uk k. 322, hadith namba 2254
48. Halliyatul-Muttaqin, uk. 109
49. Niyaazhaa wa Rawaabith Jinsii was Zanaashuii, Uk. 72
50. Islamic Laws (Shari’ah ya Kiislam) Kanuni namba 520
51. Islamic Laws (Shari’ah ya Kiislam) Kanuni namba 1593
52. Hajj Manaasik, Kanuni ya 219
53. Imethibitishwa na ofisi ya Ayatullah Sistani, Qum.
54. Wasa’ilush-Shi’a, Juz. 20, Uk. 257 hadith ya 25570
55. Wasa’ilush-Shi’a, Juz. 20, Uk. 109, hadith ya 25164
56. Niyaazhaa wa Rawaabith Jinsii was Zanaashuii, Uk. 54
57. Wasa’ilush-Shi’a, Juz. 20, Uk. 126, hadithi ya 25207
58. Niyaazhaa wa Rawaabith Jinsii was Zanaashuii, Uk. 59
59. Wasa’ilush-Shi’a, Juz. 12, Uk. 177, hadithi ya 16008
60. Mengi zaidi hasa yanapatikana kutoka Gonjhaaye Ma’navi, Uk. 318
61. Hili linapendekezwa tu kwenye sehemu ambazo mtu ana uhakika kwamba maji hayo ya mvua hayachafuliwi
na chochote.
62. Niyaazhaa wa Rawaabith Jinsii was Zanaashuii, Uk. 24-25

63. Halliyatul-Muttaqin, Uk. 172
64. Hii inarejelea kwenye athari za mafuta ya urujuani kwenye joto la tambo/la ndani.
65. Al-Kafi, Juz. 6, Uk. 332
66. Makarim al-Akhlaq, uk.190
67. Biharul-Anwar, Juz. 66, uk. 182, hadithi ya 14
68. Niyaazhaa wa Rawaabith Jinsii was Zanaashuii, uk. 22
69. Tib wa Behdaasht, uk. 292
70. Mustadrak al-Wasa'il, Juz. 14, uk. 231 hadithi ya 16578
71. Izdawaaj Maktab Insaan Saazi, Juz. 3, uk. 51
72. Gonjhaaye Ma'navii, uk. 318
73. Tib wa Behdaasht, uk. 300
74. Niyaazhaa wa Rawaabith Jinsii was Zanaashuii, uk. 28
75. Niyaazhaa wa Rawaabith Jinsii was Zanaashuii, uk. 43

Mlango Wa 3: Kanuni Muhimu Za Kifiqhi -1 Kwa Wawili Waliooana

Hali Ya Janaba

Janaba ni kunajisika kiibada kunakosababishwa na kutokwa na manii au kwa kujamiiana, na yule mtu ambaye anawajibika kuoga *Ghusl al- Janaabat* anajulikana kama *Mujnib*.

Mambo Ambayo Ni Makruh Kwa Mwenye Janaba

Mambo Ambayo Ni Makruh Kwa Mwenye Janaba[1]

1. Kula

2. Kunywa

Hata hivyo, kama mtu huyu aliyeko kwenye hali ya janaba akiosha mikono yake, uso na kinywa, halafu akala na kunywa, katika hali hiyo haitakuwa makruh. Ni rahisi kwa hiyo basi kwa mtu kutawadha.

3. Kulala

Hata hivyo, kama mwenye janaba hana maji, au kwa sababu ya kutoku- patikana maji, anaweza kufanya tayammam badala ya Ghusl al-Janabat.

4. Kugusa sehemu yoyote ya kitabu, jalada, pambizo au ukingo wa Qur'ani Tukufu au ile sehemu katikati ya mistari yake.

5. Kufanya tendo la kujamiiana wakati mtu yuko kwenye hali ya *Ihtilam* (yaani aliyetokwa na manii usingizini).

6. Kuweka nywele henna.

7. Kupaka mafuta mwilini mwake mtu.

8. Kuchukua au kukaa na Qur’ani Tukufu.

9. Kusoma zaidi ya aya saba za Qur’ani, mbali na zile ambazo sijdah ya wajibu hutokea (kuzisoma aya hizo ni haram).

DOKEZO: Udhahiri wa ‘Makruh ya Ibada’ ni tofauti na kanuni ya jumla ya makruh, ambayo ni kwamba, ni bora kwamba mtu asilifanye tendo hilo. Kwa mfano, ni makruh kwa msafiri kuswali swala ya Dhuhri, al-Asr, na Ishaai nyuma ya mtu ambaye sio msafiri na kinyume chake,2 au ni makruh kusoma Qur’ani ndani ya sajidah.3

Hii ‘Makruh ya Ibada’ haina maana kwamba ni bora mtu asilifanye tendo hilo, bali hasa ina maana kwamba kama ukikifanya kitendo hicho, basi kiwango cha malipo yake yanayopatikana ni cha chini kulinganisha na kile cha kawaida.

Mambo Ambayo Yanakatazwa Kwa Mtu Mwenye Hali Ya Janaba

Mambo Ambayo Yanakatazwa Kwa Mtu Mwenye Hali Ya Janaba4

1. Kugusa kwa kiungo chochote cha mtu huyo, maandishi ya Qur’ani Tukufu, au jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa lugha yoyote ile iwayo. Ni bora vilevile kwamba yale majina 14 ya Ma’suumin (a.s.) pia yasiguswe katika hali hiyo.

2. Kuingia ndani ya Masjidul-Haraam au Masjidun-Nabii.

3. Kukaa au kusimama katika misikiti mingine yote, na hali kadhalika katika msingi wa tahadhari ya wajib kukaa katika maquba ya Maimam watukufu ni haram pia. Hata hivyo, hakuna madhara iwapo mtu atapita au kukatisha msikiti, kwa kuingia kupitia mlango mmoja na kutokea kwenye mwingine.

4. Kuingia msikitini kwa lengo la kunyanyua kitu au kuweka kitu ndani yake.

5. Kusoma aya za Qur’ani tukufu ambazo ndani yake kuleta sajidah kunakuwa ni wajibu

6. Surat ‘Alif Lam Mim Sajdah (32:15), Surat Haa Mim Sajdah (41:38), Suratun-Najm (53:62) na Surat al-Alaq (96:19).

Josho La Janaba-(Ghuslul-Janaabah)

Nyakati Ambazo Ghuslul-Janaabah Linakuwa Ni Wajib:

1. Wakati mwanaume anapomuingilia mwanamke mpaka kwenye ile sehe- mu ya kutahiriwa kwake au zaidi, hata kama kumwaga manii hakuku- tokea, josho la janaba linakuwa ni wajibu kwao wote.5

2. Kama baada ya kujamiiana mwanaume hakufanya *Istibraa* (kujikamua) kwa ajili ya kutoa manii (ambayo ni kiasi cha kukojoa tu) na kisha akachukua josho, na baada ya hapo akaona utokwaji na kitu na hakuweza kutambua kama ni manii au hapana (yaani mkojo) itachukuliwa kwamba ni manii na kwa hiyo *Ghusul-Janaabah* itakuwa ni wajibu kwake tena.6

3. Kama mwanaume anatokwa na manii kwa kupitiwa usingizini.7

Nyakati Ambazo Ghusl Al-Janaabat Haliwi Wajib

1. Kama mtu anatia shaka kwamba dhakari yake imeingia mpaka sehemu aliyotahiriwa ama laa, hapo josho la janaba haliwi wajib kwao wote.8

2. Yale maji, unyevunyevu ambao unatolewa na mwanaume wakati wa kunyegereshana unaitwa *Madhii* na ni masafi kiibada. Yale majimaji yanayotoka baada ya kumwaga manii yanaitwa *Wadhii*, nayo ni masafi kiibada. Ule uoevu ambao wakati mwingine hutoka baada kukojoa unaitwa *Wadii*, ni msafi kiibada (isipokuwa ukikutana na mkojo) na hakuna mojawapo kati ya haya linalohitajia *Ghusl*. Iwapo mtu atafanya Istibraa baada ya kukojoa na kisha akatoa uoevu na akatia shaka kwamba ni mkojo au moja kati vioevu vilivyotajwa hapo juu, uoevu huo ni msafi kiibada.9

3. Kama mtu anashughulika katika kujamiiana mara moja na akataka kujishughulisha tena mara moja au mbili katika usiku mmoja, josho sio wajibu kwa kila mara baada ya kila tendo moja.

4. Kama mtu amemwaga manii katika usingizi wake na angependa kushughulika na kujamiiana, sio wajibu kwake kuoga josho kisha ndipo ashiriki katika tendo hilo. Ni makruh hata hivyo kujishughulisha katika tendo hilo katika wakati wa hali hiyo.10

Kanuni Muhimu Za Josho (Ghusl)

Taratibu Za Josho (Chini Ya Bafu Ya Manyunyu)

a.) Mtu kwanza ni lazima alete nia ya Ghusl na kisha aoshe kichwa na shingo halafu mwili mzima.

Ni bora kuosha upande wa kulia kwanza na kisha upande wa kushoto. Mwili hauwezi kuoshwa kabla ya kichwa11

b.) Hakuna madhara kama wakati wa kuosha shingo mtu akaosha sehemu kidogo ya upande wa kulia wa mwili wake.12

c.) Kama sehemu ya mwili imenajisika, sio muhimu kwanza kuifanya tohara ndipo uchukue Ghusl; bali wakati unapooga josho sehemu hiyo inaweza kutoharika.13

d.) Endapo sehemu yoyote ya mwili imeachwa na ukavu (hata kwa ukubwa wa kichwa cha sindano) josho hilo linakuwa ni batili.14

e.) Tofauti na wudhuu, katika Ghusl ni sawa kutochunga muwaalaat, yaani, baada ya kuosha kichwa na shingo, mtu halafu anafanya kitu kingine (kwa mfano, kuupaka mwili sabuni), ni sawa kwake kurudi tena kuosha mwili baada yake; sio lazima kwa josho hilo kuanzishwa upya kuanzia mwanzo kabisa.15

f.) Shuruti zote ambazo zinatengua wudhuu, vilevile zinatengua Ghusl.

g.) Kama mtu atatokea kukojoa wakati wa josho au kutokwa na ushuzi, sio lazima kwa josho kuanza upya; josho hilo hilo linaweza kumaliziwa. Hata hivyo, kama mtu atataka kuswali, basi kwa mujibu wa tahadhari ya wajib, wudhuu lazima uchukuliwe hapo kwani hairuhusiwi kuswali kwa tohara ya josho hilo hilo.16

h.) Ghusl yenye nia nyingi kama inavyohitajika, mustahab na wajib, kwa mfano, Ghusl ya

sunna ya Ijumaa inaweza kufanywa wakati mmoja na Ghusl ya Janaba.17

i.) Baada ya Ghusl ya Janaba kufanyika, mtu lazima atawadhe kwa ajili ya Swala. Hii ndio hali kwa majosho yote ya wajibu. Kama nia nyingi zitaingizwa, kwa mfano nia ya mustahab na wajib, hapo tena wudhuu sio lazima.18

Tayammum

Nyakati Ambazo Tayammum Inaweza Kutendwa Badala Ya Ghusl

Kuna hali namna sita ambapo tayammam inaruhusiwa badala ya Josho, ambazo kwamba zifuatazo zinatumika sana kwa wanandoa:

1. Wakati Hayawezi Kupatikana Maji Ya Kutosha Josho

Kama mtu anaishi kwenye sehemu yenye makazi ya watu wengi, anapaswa kufanya juhudi ya kutosha katika kupata maji kwa ajili ya Josho, mpaka wakati ambapo huenda matumaini yote yatakapopotea.19

Kwa hiyo endapo mtu atahitaji kufanya Ghusl ili aweze kuswali, na kwa wakati huo hakuna maji yanayoweza kupatikana, bali mtu akawa na hakika kwamba kabla swala hiyo haijawa qadhaa maji yatapatikana, basi ni lazima mtu asubiri hadi yatakapopatikana maji ili Josho liweze kufanyika.

Tayammam haiwezi kufanyika katika hali hii hata kama muda wa swala (wa fadhila) utakuwa umeingia au kama swala ya jamaa inaswaliwa.20

Hata kama kuna dalili kidogo tu kwamba maji yatapatikana kabla ya wakati wa swala, mtu hawezi kufanya tayammam na kuswali mpaka labda mtu atakapopoteza matumaini kabisa kwamba maji hayatapatikana kabisa kabla ya swala hiyo kuwa qadhaa.21

Hata hivyo, kama mtu ana uhakika kabisa kwamba maji hayatapatikana kabla ya qadhaa, basi hapo mtu anaweza kufanya tayammum na kuswali kwa wakati wa mapema iwezekenavyo.22

2. Wakati Inapokuwa Ni Karibu Kuwa Wakati Wa Qadhaa

Mtu anapaswa kufanya tayammum pale wakati uliobakia kwa swala hiyo kuwa qadhaa ni mdogo sana kiasi kwamba kama mtu atafanya Ghusl, hakutakuwa na muda uliobakia kwa kutekeleza swala hiyo**.**23
Hata kama mtu atakuwa na mashaka kwamba kutakuwa na muda wa kutosha au laa utakaokuwa umebaki kwa ajili ya swala kama akichukua josho au wudhuu, anapasika kufanya tayammam.24

3. Hatari Kwa Afya

Kama mtu akihofia kwamba endapo atatumia maji ataugua maradhi fulani au madhara ya kimwili, au ugonjwa ambao tayari anaugua utaendelea kwa muda mrefu, au utakuwa mkali zaidi au ugumu mwingine zaidi utaweza kujitokeza, basi anapaswa kufanya tayammam. Kwa mfano, kama mtu ana ugonjwa wa macho ama sindano mahali ambapo maji hayaruhusiwi juu yake kwa masaa 24, tayammam inapaswa kufanyika. Hata hivyo, endapo mtu anaweza kuyaepuka madhara hayo kwa kutumia maji ya vuguvugu, aandae maji ya

vuguvugu kwa ajili ya Josho.25

Utaratibu Wa Kufanya Tayammam

Tofauti na utambuzi wa kawaida, kufanya tayammam kwa kweli ni jambo rahisi na jepesi sana; ni rahisi zaidi kuliko kutawadha. Kunapaswa kutekelezwa kama ifuatavyo:

Hatua Ya Kwanza:

Tia nia ya kufanya tayammam (sawa na wudhuu ama Ghusl).

Hatua Ya Pili:

Kwa mikono yote kufunguliwa wazi na kunyooka kuelekea kile kitu ambacho tayammam inaruhusiwa juu yake (udongo, vumbi, mchanga na au jiwe); piga (au weak) mikono yote kwa pamoja, mmoja pembeni ya mwingine juu ya kitu hicho ambacho tayammam inafanyika juu yake.

Hatua Ya Tatu:

Nyanyua mikono yako na uiweke pamoja kama mtu anayeomba du'a, halafu weak vitanga vya viganja vyako juu ya paji la uso kuanzia maoteo ya nywele. Telezesha mikono yako chini juu ya nyusi na ncha ya pua, halafu vishushe viganja vyako kuelekea upande wa kulia wa paji la uso na halafu upande wa kushoto. Kisha rudisha mikono yako katikati ya paji la uso na uiteremshe yote kwa pamoja kuelekea puani, ukihakikisha na vidole pia vinaparaza juu ya nyusi na ncha ya pua. Paji lote la uso linapaswa kufunikwa hadi kwenye nyusi (inapendekezwa kushusha kupita zaidi ya nyusi).

Hatua Ya Nne:

Nyoosha mkono wa kulia ukihakikisha kwamba kiganja chako kimeelekea chini, vidole na dole gumba vikiwa vimefungana pamoja na dole gumba halikuchimbiwa chini ya vidole. Halafu weka upande wa ndani wa mkono wa kushoto katika hali ya wima juu kidogo ya kifundo (yaani, kile kidole kidogo tu ndio kinapaswa kukandamizwa juu ya kifundo cha mkono wa kulia, kiganja cha mkono wako wa kushoto kikuangalie wewe).

Teremsha mkono wa kushoto (ukishusha kiganja chini), ukihakikisha maeneo yote ya ndani ya mkono wa kulia ziefunikwa. Rudia utaratibu huohuo juu ya mkono wa kushoto (bila ya kurudia kupiga mikono juu ya udongo tena).

Mambo Muhimu Kuhusiana Na Tayammam

a.) Kama utaacha hata sehemu ndogo tu ya paji lako la uso au sehemu ya nyuma ya mikono yako katika tayammam, kwa makusudi au kwa kusahau, au hata kwa kutokujua, tayammam yako itakuwa batili. Unapaswa kuwa mwangalifu lakini usizidi kuwa mahususia, kama itaweza kuchukuliwa vya kutosha kwamba paji la uso na nyuma ya mikono vimepakwa itakuwa imetosheleza.26

b.) Kama namna ya tahadhari, upakaji wa kichwa na mikono unapaswa kufanywa kuanzia juu kushuka hadi chini.27

c.) Ni *Ihtiyat mustahab* (tahadhari inayopendekezwa) kwamba hilo paji la uso, viganja vya

mikono na sehemu za nyuma za viganja na mikono vinakuwa tohara.28

d.) Wakati wa kufanya tayammam, pete ni lazima zivuliwe na kizuizi chochote kwenye paji la uso au kwenye viganja au nyuma ya mikono navyo ni lazima viondolewe.29

Kuvitoharisha Vile Vitu Ambavyo Vimechafuliwa Na Manii

Nguo Au Shuka Za Kitanda

Kama mashuka ama chochote cha kuvaa kama nguo au taulo vikinajisika kwa manii vinaweza kutoharishwa katika njia zifuatazo:

A. Kutumia Maji Yanayotiririka

1. Kama kitu hicho bado kina ubichi kutokana na manii, mtu anapaswa kuwa mwangalifu kwamba kisigusane na nguo nyinginezo au vitu vinginevyo kwa sababu hapo navyo vitakuwa vimenajisika.

2. Mtu anapaswa kuosha kile kilichonajisika mara moja chini ya maji ya bomba (*kurr*) katika namna ambayo kwamba:

a.) Maji yanafika kwenye kila sehemu ya lile eneo lililonajisika.

b.) Kuwe hakuna dalili za yale manii hasa yaliyoachwa kwenye nguo (yaani, sugua na kukamua nguo wakati wa kufua kwa namna ambayo hakuna mabaki ya manii yanayoachwa kwenye nguo wala rangi yake).

3. Kama kitu chenyewe ni kipande cha nguo, hakuna haja ya kukipopotoa au kukikamua baada ya kuwa kimetoharishwa (kwa mtindo huo hapo juu), ingawa hili huwa linafanyika kutokana tu na mazoea.

4. Wakati kitu hicho kikiwa kimeoshwa mara moja na kuwa safi kitohara (kwa mtindo huo hapo juu) hii inatosha; hailazimiki kukiosha mara mbili au tatu.

5. Kama kitu kilichonajisika kinatoswa kwenye maji ya bomba yanayotiririka (*kurr*) au maji yanayotembea, kwa namna ambayo maji yanaz- ifika sehemu zake zote zilizonajisika, kinakuwa kimetoharika. Na katika suala la zulia au vazi sio muhimu kulikamua, kulipopotoa au kuliminya.30

B.) Kutumia Mashine Za Kufulia

Hukmu inayotumika kwenye mashine za kufulia ni ile ya maji ya kurr.31 Hivyo kitu ambacho kimekuwa najis kwa manii kinaweza kuwekwa moja kwa moja kwenye mashine ya kufulia, na madhali hakuna dalili ya manii iliyobakia baada ya mzunguko kukamilika, halafu kitu hicho kinachukuliwa kuwa kimetoharika, na hakihitaji kuoshwa tena, au kupopotolewa na kukamuliwa.

Hata hivyo, kama hatua ya tahadhari, linaweza kuwa ni wazo jema kukifanya kile kitu kilichonajisika kuwa kisafi kitohara kwanza (kwa njia ile ya pale juu) na kisha tukiweke kwenye mashine ya kufulia, kwa sababu kama mtu ataweka kitu hicho moja kwa moja ndani ya mashine ya kufulia, na kwa sababu yoyote iwayo manii hayo yakabakia kwenye

nguo baada ya kufuliwa, haitakuwa safi kitohara, na endapo nguo hiyo itakutana na nguo nyinginezo zenye ubichi, nguo hizo pia zitakuwa zimenajisika

Godoro:

A. Kutumia Maji Yanayotiririka

Endapo godoro litanajisika kwa manii kwa sababu yoyote ile iwayo, inawekana kulifanya tohara kwa maji safi yanayotiririka kutoka kwenye bomba au mpira wa maji:

Kama mtu anataka kutakasa godoro kwa kutumia maji safi yaliyounganishwa kwenye chanzo cha bomba – *kurr* – (kwa mfano kwa kutumia mpira wa maji au bomba) hakuna haja ya kuyafuta maji hayo kwa kutumia nguo hiyo au mashine ya kivuta vumbi na kadhalika.

Mara tu yale maji ya kurr yanapolienea eneo lenye najis, litakuwa tohara (madhali ile najasat ayn – manii, itakuwa imeondolewa) [na maji hayo pia yatachukuliwa kuwa tohara].32

Ni muhimu kukumbuka yafuatayo wakati godoro linapokuwa limenajisika kwa manii: Manii hayo yanahamia tu kutoka kwenye godoro kwenda kwenye kitu kingine kupitia unyevunyevu unaobubujika (yaani, unapokuwepo ubichi mwingi katika kile kilichonajisika ambao unapenya kwenye kitu kingine na kukifanya kuwa najisi).

Hiyo najisi haihamishiki inapokuwa kavu, hivyo iwapo utaweka mwili au mkono wako juu ya godoro lenye najisi kavu, huo mkono au mwili wako hautakuwa umenajisika.

Kwa hiyo, inawezekana kulala juu ya godoro ambalo limenajisika bila ya nguo zako kunajisika, alimradi tu kwamba kile kipande ambacho kimenajisika kinabakia kuwa kikavu ili kwamba ile najisi haihamishiwi kwenye nguo hizo kutoka kwenye godoro hilo.

B. Kutumia Maji Machache Kuliko Kurr (Qaliil)

Maji machache kuliko kurr yanatumika katika hali ambazo imma maji ya kurr hayapatikani au kwamba huwezi kuweka kitu kama godoro chini ya maji ya kurr (chini ya bomba). Utaratibu wa kukifanya kitu kiwe kisafi kitohara kwa maji machache ni kama ifuatavyo:

Hatua Ya 1: Kuiondoa Najisi

Manii hayo ni lazima yaondolewe kutoka kwenye godoro hilo. Mbinu inayowezekana ya kufanya hili ni kwanza kumwaga maji kutoka kwenye gilasi kuenea kwenye eneo lote lililoingia doa. Halafu chukua taulo na liweke juu ya ile sehemu iliyolowa na tumia nguvu kuminya juu yake kwa namna ambayo maji hayo yananyonywa na kwamba hakuna manii yanayobakia. Taulo litakalotumika litakuwa limenajisika na litahitaji kuoshwa kitohara.

Hatua Ya 2: Kumwaga Maji Kuliko Kiwango Cha Kurr

Baada ya kuyaondoa yale manii, sehemu hiyo inatakiwa ifanywe kuwa tohara. Hili linafanywa
kwa kuchukua gilasi nyingine ya maji na kumwagia tena maji juu ya eneo lote tena (lile lililokuwa limenajisika).

Maji hayo ni lazima yakamuliwe na kuminywa yatoke kwenye godoro kabla halijawa tohara.

Hili linaweza kufanyika kwa kuchukua taulo na kuliweka juu ya eneo lililoloweshwa kwa namna ambayo wakati nguvu inapoongezwa juu ya taulo hilo maji yote yananyonywa yatoke.

Godoro hilo sasa limekuwa tohara. Kama rai iliyothibitishwa na sio tahadhari ya wajibu, taulo hilo na maji yaliyotolewa yatahesabiwa kuwa ni najisi.

Kama kitu chochote kinakuwa najisi kwa uchafu mwingineo mbali na mkojo, kitakuwa tohara kwa kwanza kuondoa ule uchafu na kisha kumwa- gia maji machache chini ya kiwango cha kurr, mara moja, na kuyaruhusu yamwagike. Bali kama ni nguo na kadhalika, inapaswa kukamuliwa na kuminywa ili kiasi chochote cha maji kilichobakia kiweze kumwagika.33

Kiangalizo: Ni muhimu kabisa kutambua kwamba hata kama sehemu ya juu ya godoro inafanywa kuwa safi kitohara kwa maji machache (*qaliil*) kwa kufuatilia mfano huo hapo juu, sehemu ya ndani ya godoro itakuwa najisi kutokana na kununi ya maji machache. Hata kama godoro hilo litawekwa kwa pembe, bila shaka yatanywea kwenye godoro hilo.34

PENDEKEZO: Ili kuepukana na kazi hii ngumu ya ziada na ugomvi wote wa kulisafisha godoro, kuna manufaa makubwa sana kwamba mtu awe anaweka tandiko la plastiki kati ya shuka na godoro, ili kwamba kama kiasi chochote cha manii kitavuja kwenye shuka hakitavuja kupita kwenye plastiki hadi kwenye godoro.

Mwili Wenyewe

Kama sehemu ya mwili inanajisika kwa sababu ya manii, inaweza kufanywa safi kitohara kwa kumwagiwa maji kiwango chini ya kurr juu yake mara moja kwa namna ambayo kwamba hakuna mabaki ya manii yanayoachwa kwenye mwili. Hili linaweza kufanyika kwa kusimama chini ya bomba la manyunyu.

Hata hivyo, kanuni hii ni tofauti kama najisi yenyewe ni mkojo, ambao kuuosha mara moja hakutoshi, mwili lazima uoshwe mara mbili. Sio lazima kuingia na kutoka kwenye maji ili kupata majosho mawili. Endapo sehemu iliyopata najisi inapanguswa kwa mkono kuruhusu maji kufika hapo tena, hiyo itatosha.35

1. Islamic Laws – Shari’ah ya Kiislam; Kanuni ya 362
2. Islamic Laws, Kanuni ya 1499
3. Islamic Laws, Kanuni ya 1101
4. Islamic Laws, Kanuni ya 361
5. Islamic Laws, Kanuni ya 355
6. Islamic Laws, Kanuni ya 354
7. Islamic Laws, Kanuni ya 351
8. Islamic Laws, Kanuni ya 356
9. Islamic Laws, Kanuni ya 74
10. Islamic Laws, Kanuni ya 362
11. Islamic Laws, Kanuni ya 367
12. Islamic Laws, Kanuni ya 369
13. Islamic Laws, Kanuni ya 378
14. Islamic Laws, Kanuni ya 380
15. Islamic Laws, Kanuni ya 386
16. Islamic Laws, Kanuni ya 392
17. Islamic Laws, Kanuni ya 395

18. Islamic Laws, Kanuni ya 397
19. Islamic Laws, Kanuni ya 655
20. Islamic Laws, Kanuni ya 723
21. Islamic Laws, Kanuni ya 723
22. Islamic Laws, Kanuni ya 723
23. Islamic Laws, Kanuni ya 686
24. Islamic Laws, Kanuni ya 686
25. Islamic Laws, Kanuni ya 677
26. Islamic Laws, Kanuni ya 710
27. Wasa'ilush-Shi'a; Juz. 20, Uk. 109, namba 25163
28. Islamic Laws, Kanuni ya 714
29. Islamic Laws, Kanuni ya 715
30. Islamic Laws, Kanuni ya 160
31. Imethibitishwa na ofisi ya Ayatullah Sistani, Qum.
32. Kanuni ya Desturi kwa Waislam huko Magharibi, Ayatullah Sistani.
33. Islamic Laws, Kanuni ya 163
34. Islamic Laws, Kanuni ya 163
35. Islamic Laws, Kanuni ya 172

Mlango Wa 4: Upangaji Wa Familia

Uzazi Wa Mpango Katika Uislam:

Uzazi 1 wa mpango kama hatua ya binafsi kupanga au kudhibiti ukubwa wa familia kwa sababu za kiafya au kiuchumi zinazoruhusiwa katika Uislam. Hakuna ama aya ya Qur’ani au hadithi dhidi ya udhibiti wa uzazi, wala sio wajibu wa lazima kupata watoto katika ndoa. Aidha, kuna hadithi kadhaa ambazo bila shaka zinathibitisha kwamba kupanga uzazi kunaruhusiwa.

Imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.) kwamba: “Moja ya njia mbili za ukwasi ni kuwa na wategemezi wachache.2

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba: “Imam Ali ibn al- Husein (a.s.) hakuona tatizo katika kukatiza kujamiiana na kumwagia nje na alikuwa akiisoma aya ya kwamba: **‘Na (kumbuka) Mola wako alipowaleta katika wanadamu kutoka migongoni mwao kizazi …..’** 3

Hivyo kutoka kwenye mbegu yoyote Mwenyezi Mungu amechukua ahadi, ina uhakika wa kuzaliwa hata kama (imemwagwa) juu ya jiwe gumu.4

Kwa kulingana na hadithi hiyo hapo juu, uumbaji upo mikononi mwa Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee. Tupange ama tusipange uzazi, kama Mwenyezi Mungu Mtukufu akihukumu, mtoto huyo atatungwa kwenye mimba.

Kwa kuhitimisha ni kwamba hadithi hiyo hapo juu inaonyesha kwamba kupanga uzazi kunaruhusiwa.

Mbinu Za Kuzuia Mimba

Kuna idadi kadhaa ya mbinu au njia za uzuiaji wa mimba. Zile ambazo kwa kawaida ni zenye kutumika sana tutazichunguza hapo chini ili kufahamu iwapo kutumika kwake kunaruhusiwa katika Uislam au hapana.

Uruhusiwaji umetambulika kwa ufafanuzi wa uanzaji wa ujauzito kwa mtazamo wa Kiislam, ambao ni wakati yai la uzazi linapopandikizwa kwenye ukingo wa mji wa mimba tumboni mwa mwanamke.

Kwa hiyo, chochote kinachozuia upandikizaji huo kinaruhusiwa na chochote kinachokatisha mimba, baada ya upandikizaji, huko ni kutoa au kuharibu mimba nako ni haraam (hakuruhusiwi).

Ni muhimu kutambua kwamba mbinu hizi zimechunguzwa kutokana na mtazamo wa fiqhi tu. Kwa maoni ya kiuganga kuhusu kuaminika na uwezekano wa athari za mbinu hizi, tafadhali muone daktari.

Mbinu Zinazoruhusiwa

Mbinu zifuatazo hazihusishi upasuaji kiganga na pia zinageuzika na kutu- mika kwa njia zaidi ya moja. Mwanaume au mwanamke anayetumia mbinu hizi anaweza kuacha kuzitumia wakati wowote ili kuweza kutunga mimba.

1. Kinga Ya Vidonge (Vya Kumeza)

Vidonge vya kudhibiti uzazi huzuia kushika mimba kwa kuzuia utengenezwaji wa mayai ya uzazi. Vidonge hivyo hubadilisha viwango vya homoni na huzima dalili za homoni kutoka kwenye tezi kwa ajili ya ovari kutoa yai la uzazi. Vidonge hivi vinatumiwa kwa njia ya kunywa kwenye ratiba sahihi kwa siku 20 au zaidi wakati wa kila mzunguko mmoja wa hedhi.

Kwa vile aina zote za vidonge kama hivyo huwa vinazuia utengenezwaji wa mayai, basi vinaruhusiwa; hata hivyo, mhusika lazima amuone daktari kuhusu athari ambazo zinawezekana kutokea.

Kuna baadhi ya vidonge ambavyo vinafanya kazi baada ya kujamiiana kukishatokea, kwa mfano, kile ‘kidonge cha asubuhi ya baada’ – *(morning- after pill)*, au kile kilichoendelezwa hivi karibuni, kidonge cha RU486. Halafu tena, kwa vile matumizi ya vidonge kama hivyo yanazuia upandikizwaji wa mayai, basi yanaruhusiwa. Kwa hiyo, vidonge kama vile ‘*morning-after pills*’ na RU486 vinaweza kutumika baada ya kujamiiana LAKINI sio baada ya kuhisi au kutambua kwamba mimba tayari imekwishatungika.

2. Sindano Ya Depo-Provera

Depo-Provera inafanya kazi sawasawa kabisa kama vidonge, bali badala ya kuinywa huwa inapigwa sindano mara moja kila baada ya miezi mitatu. Hii na njia za kuzuia uzazi nyingine kama hii kwa njia ya sindano zinaruhusiwa.

3. Kitanzi (Intrauterie Devices Iud)

IUD ni kitanzi cha plastiki au metali, katika aina mbalimbali za maumbo, ambacho

kinapachikwa ndani ya mji wa mimba (uterasi). Wataalam wa uganga hawajui hasa jinsi IUD inavyofanya kazi.

Kwa wakati huu kuna maoni namna mbili: namna moja inasema kwamba IUD inazuia urutubishaji wa mayai; na ile nyingine inasema kwamba inazuia yai lililoru- tubishwa kupandikizwa kwenye mji wa uzazi.

Kwa vile mimba inaanzia kwenye upandikizaji kwa mujibu wa mtazamo wa Kiislam, matumizi ya IUD kama mbinu ya kudhibiti uzazi yanaruhusiwa, bila kujali tofauti hizo hapo juu miongoni mwa wataalam wa tiba.

4. Mbinu Ya Kizuizi

Mbinu za kizuizi zote zinazuia mbegu ya kiume kupenya na kuingia kwenye mji wa uzazi. Hizi zinafanyika kwa kuifunika dhakari kwa kondomu, au kwa kufunika mlango wa tumbo la uzazi kwa kiwambo, finiko ya mlango wa uzazi, au sponji ya ukeni. Matumizi ya viini vya kuulia ambavyo vinaua mbegu za kiume kabla ya hazijafika kwenye mji wa uzazi vilevile ni mbinu ya kuzuia. Zote ni namna za kudhibiti uzazi.

5. Kujizuia Wakati Wa Kipindi Cha Rutuba

Kuna taratibu aina tatu za kimsingi za kutabiri utayari wa mayai ya mwanamke, ili kuweza kujiepusha na kujamiiana wakati wa takriban siku sita za kipindi cha uwezo mkubwa sana wa kushika mimba wa mwanamke cha kila mwezi..

Njia hizo tatu ni kama zifuatazo:

a.) Mbinu ya kutagwa kwa yai: Mwanamke anajifunza kutambua kile kipindi cha rutuba, yaani utayari wa yai kwa kukagua ile tofauti katika uanzaji wa kutoka kwa ute wa mlango wa uzazi.

Kutoka kwa ute wa mlango wa uzazi kunaashiria kile kipindi cha mbolea kabisa, na hivyo kujiepusha na ngono katika wakati huu kunazuia ushikaji wa mimba.

b.) Mbinu ya mfuatano maalum: Hii ni mbinu inayofanana na ile ya kwan- za, bali inategemea katika kuchunga ile mizunguko ya kila mwezi kwa mwaka mzima ili kutambua zile siku za hatari (za kuweza kushika mimba).

c.) Hali ya Joto: Katika mbinu hii, mbali na kuweka rekodi ya kalenda ya mzunguko wake, mwanamke pia anapima joto lake kila siku ili kugundua utayari wa yai. Anaweza kutambua wakati wa utayari wake wa yai wakati wowote joto lake muhimu la mwili linapoongezeka.

Kiangalizo: Njia nyingine ya kisasa zaidi ni kutabiri utayari wa mayai kwa kutumia kipimia utayari wa yai (ovulation test) ambacho kimeundwa ili kutabiri zile ziku za mbolea zaidi za kuweza
kuwa mjamzito.

6. Kutoa Na Kumwagia Nje (Coitus Interruptus):

Hii ina maana ya kuchomoa dhakari mara tu kabla ya kumwaga manii. Hii ilikuwa ndio mbinu ya kawaida kabisa ya kudhibiti uzazi kabla ya kugunduliwa kwa mbinu za kisasa.

Imesimuliwa kwamba Muhammad ibn Muslim na Abdur-Rahman bin Abi Abdillah Maymun

walimuuliza Imam as-Sadiq (a.s.) kuhusu uchomoaji. Imam akasema: “Ni juu ya mwanaume; anaweza akamwagia popote anapotaka yeye.5

Hata hivyo, katika hadithi nyingine, Muhammad bin Muslim anasimulia kutoka kwa Imam wa tano au wa sita (a.s.) kama ifuatavyo: “Kwa upande wa mtumwa wa kike hiyo imeruhusiwa, hata hivyo, kwa upande wa mwanamke huru, mimi nalichukia hilo isipokuwa kama lilikuwa limeamuliwa hivyo wakati wa kufunga ndoa.6

Kwa kutegemea hadithi hiyo hapo juu, wengi wa Mujitahid wetu wanaami- ni kwamba kuchomoa na kumwagia nje kunaruhusiwa bali ni makruh iwapo ni bila ridhaa ya mkewe mwenyewe. 7

7. Kufisha Mbegu (Za Uzazi) – Sterlization:

Kufisha mbegu kunahusisha upasuaji kiuganga. Kufisha mbegu kwa wanaume, kunakojulikana kama kuhasi, kunahusisha utenganishaji au ufungaji wa bomba katika njia ya uzazi ya mwanaume. Bomba hili au mchirizi unapitisha manii kutoka kwenye korodani kwenda kwenye kibofu cha masalia na viungo vingine vya uzazi.

Kufisha mbegu kwa mwanamke, kunakojulikana kama kufunga kitanzi, kunahusisha uzibaji au utenganishaji wa mirija ya uzazi inayosafirisha yai.

Kufisha mbegu hakuko huru kutokana na vipingamizi, ingawaje kunaruhusiwa kama hakuambatani na mbinu zilizokatazwa zilizoonyeshwa hapo chini.8

Mbinu Zilizokatazwa

Mbinu yoyote ya uzazi wa mpango au kudhibiti uzazi inakatazwa chini ya mazingira yafuatayo:

a.) Pale inapoleta madhara makubwa kwenye afya ya mwanamke, kama vile kuondoa viungo fulani kama vile mifuko ya mayai ya uzazi.

b.) Wakati inapohusisha kitendo haramu, kama vile mwanaume kugusa au kuangalia kwenye sehemu za siri za mwanamke ambazo zimekatazwa au kuharamishwa juu yake kuzitazama, hapo inakatazwa.

Masharti haya yanaweza kupuuzwa tu katika mazingira yaliyozidi mno, inapokuwa ni muhimu kabisa.

Maridhiano Kati Ya Mume Na Mke

Kwa mujibu wa mwelekeo wa kisheria wa shari’ah ya kiislam, mke anayo haki kamili ya kutumia mbinu za kudhibiti uzazi (*contraceptives*), hata bila kuridhia na kuruhusiwa na mume wake.9

Hata hivyo, mke huyo asije akatumia mbinu ambayo inaweza kuingilia kati haki za ndoa za mume wake. Kwa mfano, hawezi kumlazimisha kutumia kondomu au kufanya njia ya kumwagia nje au kukatiza kujamiiana.

Kanuni hii imeegemea kwenye msingi kwamba kadiri ya haki za kindoa za mume juu ya mkewe ni kwamba tu anapaswa kupatikana kwa kujinsia, mwenye kuelekea na mwenye ushirikiano.

Haki hii haiendelei kufikia ile ya kumzalia watoto. Kuzaa watoto au kutozaa ni uamuzi binafsi wa mwanamke, na kwa hiyo, anaweza kutumia njia za kuzuia uzazi kama vile vidonge, sindano au uoshaji wa uke wake baada ya kujamiiana, kwani hizo haziingilii haki za kindoa za mume wake.

Kinyume chake, mume hana haki ya kumlazimisha mke wake asibebe mimba kama akitaka kufanya hivyo, kwa kumlazimisha matumizi ya vidonge, sindano au kitanzi IDU. Hata hivyo, anaweza kutumia kondomu maadamu awe amepata ridhaa ya mkewe juu ya hilo. Kwa nyongeza, anayo haki ya kufanya hivyo kwa kutumia kumwagia nje wakati wa kujamiiana.

Kwa busara ya sawa hata hivyo, maamuzi kama hayo yanafanywa kwa ubora zaidi kwa mashauriano ya pamoja baina ya mume na mke; vinginevyo, inaweza kusababisha kutokuelewana na kutoaminiana.

Mtazamo wa kisheria ni kulinda hame za mwanamke, lakini katika dunia yenyewe, mwanaume na mwanamke lazima waweke msingi wa maisha yao juu ya upendo, huruma na ushirikiano kama ilivyoelezwa katika *Surat ar-Rum*; 30:21, **“Naye amejaalia mapenzi na huruma kati yenu.”**

Kuharibu Mimba (Abortion)

Mtazamo wa Uislamu kwenye suala la kudhibiti au kupanga uzazi na kuharibu mimba ni wa sawasawa kabisa. Unawaruhusu wanawake kuzuia mimba lakini unawakataza kuikatisha. Kuharibu au kutoa mimba baada ya kupandikizwa yai la mbolea (uzazi) kwenye tumbo la uzazi kumekatazwa kabisa na kunachukuliwa kuwa ni uhalifu dhidi ya sheria ya Mwenyezi Mungu, na vile vile kosa dhidi ya hicho kijusi (*foetus*).

Kwa mtazamo wa kimaoni wa Uislam, uharamu wa kutoa kijusi hautegemei juu ya suala la kwamba kijusi hicho kina hali ya binadamu au hapana. Ingawa Uislam haukitambui kijusi kama binadamu kamili, bado unatoa ile haki ya uhai unaowezekana.

Utoaji mimba huwa unafikiriwa kwa sababu mbalimbli. Hizi zitajadiliwa, na mtazamo wa Kiislam katika kila sababu utaangaliwa.

1. Ni Uchaguzi Kati Ya Mtoto Na Kazi Na/Au Mtindo Wa Maisha Ya Anasa

Sababu hiyo hapo juu inaakisi hali ya asili ya ubinafsi wa jamii hii ya kimaada, na haichukuliwi kuwa ni sababu ya halali au yenye kukubalika kwa ajili ya utoaji wa mimba. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ مِنْ إِمْلَاقٍ ۖ نَحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ ۖ {151}

“Wala msiwaue watoto wenu kwa sababu ya umasikini, Sisi tutakupeni riziki ninyi na wao …..”
(Al-An’aam; 6:151).

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ خَشْيَةَ إِمْلَاقٍ ۖ نَحْنُ نَرْزُقُهُمْ وَإِيَّاكُمْ ۚ إِنَّ قَتْلَهُمْ كَانَ خِطْئًا كَبِيرًا {31}

"Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa umasikini, sisi ndio tunaowaruzuku wao na ninyi pia, kwani kuwaua ni kosa kubwa. (Al- Israa; 17:31)

Naam, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu hakutuambia sisi kuwa: ***"Sisi hatuikalifishi nafsi ila kwa yale iliyo na uwezo nayo." (al- An'aam; 6:172).***

2. Mtoto Anatungwa Mimbani Kinyume Cha Sheria

Haya ni matokeo ya mahusiano haramu ya kingono ambayo Uislam unayashutumu kwa nguvu zote, bali hayachukuliwi uhalali unaokubalika wa kuharibu au kukitoa kijusi.

3. Mtoto Ni Wa Jinsia Isiyopendelewa

Sababu hii haina tofauti yoyote ya ubaya na ukatili na ile desturi ya kiarabu ya kabla ya Uislam ya kuwazika watoto wa kike wakiwa hai, na vilevile sio sababu halali ya kukubalika kwa ajili ya kutoa au kuharibu mimba.

4. Mtoto Ni Matunda Ya Ubakaji

Wakati mwanamke anapokuwa amebakwa, anapaswa kutumia vile vidonge vya 'asubuhi ya baada' au RU486 mara moja tu baada ya shambulio hilo la kingono ili kuzuia uwezekano wa upandikizwaji wa mbegu ya uzazi. Hata hivyo, mara tu mimba itakapoanza, basi Uislam hauruhusu kuitoa.

Katika sababu kama hiyo, Uislam hauwezi kuhalalisha utoaji mimba ya mtoto kwa ajili ya dhambi au kosa la baba. Na kuhusu heshima ya mwanamke huyo, Uislam unawashutumu sana wale watu wanaomdharau mwathirika wa ubakaji; badala ya kumshutumu na kumtukana, wanapaswa kuwa wenye huruma juu yake.

5. Mtoto Ana Mapungufu

Kwa matumizi ya vipimo vya mawimbi ya sauti (*ultrasounds*) na tekinolojia nyingine za kisasa kama hiyo, inawezekana kujua iwapo kama mtoto anayo mapungufu mapema kabisa kabla hajazaliwa. Watu wengine wanahalalisha kuharibiwa kwa kijusi chenye hitilafu.

Hata hivyo, Mujtahid wa wakati huu wa sasa hawaruhusu utoaji mimba wa namna hiyo, hata kama hitilafu hizo ni kubwa na mbaya sana kiasi kwamba hazitibiki baada ya kuzaliwa mtoto, na kwamba mtoto anaweza asiishi baada ya kuzaliwa isipokuwa kwa muda mfupi na kwa maumivu makali.

Wazazi wanapaswa kuomba na kutumainia afya njema ya mtoto huyo. Naam, wakati kuna bahati kwamba kijusi kinaendelea kinyume na utabiri wa kiganga. Bahati hii, kwa vyovyote itakavyokuwa finyu na isiyo na umuhimu, bado inatun- yima sisi haki ya kukatiza uhai.

6. Mimba Hiyo Ni Hatari Kwa Mwanamke

Mfano pekee unaoruhusiwa, wa kutoa au kuharibu mimba ni iwapo kijusi hicho kina umri

chini ya miezi minne pungufu (kabla roho haijaingia ndani yake) na madaktari wakaamua kwa uhakika wenye mantiki kwamba uendeleaji wa mimba hiyo utamdhuru mwanamke huyo, au kumsababishia matatizo kwa kiwango ambacho kwa kawaidi hakivuliki. Haiwezekani kukitoa au kukiharibu kijusi hicho baada ya miezi minne bila hata kujali sababu ya utoaji mimba yenyewe.

Malipo Ya Fidia

Kama utafanyika utoaji mimba, yeyote atakayefanya utoaji mimba huo atakuwa anawajibika katika ulipaji wa fidia. Hii ni bila ya kujali iwapo utoaji mimba huo unafanyika kwa hiari, kwa makubaliano ya wazazi wote ama la.

Malipo hayo ya fidia yanafanya sehemu ya mali ya mtoto huyo na itak- wenda kwa warithi wake, yaani wazazi wake hata ingawa inawezekana wakawa washiriki kwenye uamuzi huo. Hata hivyo, ni jambo ambalo, wazazi wake, kama warithi wake, wanaweza kusamehe haki zao, hivyo kuondoa uwajibikaji wa malipo hayo kutoka kwa yule mtu anayefanya utoaji mimba huo.Malipo hayo ni kama ifuatavyo:10

Kama Kijusi Hicho Ni:

Chenye umri hadi kufikia siku 40 – gramu 70 za dhahabu
Chenye umri hadi kufikia siku 80 – gramu 140 za dhahabu
Chenye umri hadi kufikia siku 120 – gramu 210 za dhahabu
Chenye umri hadi kufikia siku 160 – gramu 280 za dhahabu

Kijusi Chenye Umri Hadi Kufikia Siku Zaidi Ya Hapo:

Kama mimba ya mtoto wa kiume inatolewa – gramu 350 za dhahabu
Kama mimba ya mtoto wa kike inatolewa – gramu 1750 za dhahabu
Kwa nyongeza, mtu lazima afanye istighfar na kuomba msamaha wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ili kwamba ule uhai uliotolewa (kwa kuharibu mimba) usije ukatafuta kudai kurudishiwa uhai wake tena.

1. Sehemu kubwa imechukuliwa kutoka Mariage and Morals in Islam, Sayyid Muhammad Rizvi, Contemparary Laws cha Ayatullah Sistani, na A Code of Practice for Muslims in the West
2. Nahjul-Balaghah, hotuba ya 141
3. Suratul-A’raf; 7:172
4. Wasa’ilush-Shi’ah, Jz. 14, Uk. 105.
5. Wasa’ilush-Shi’ah, Jz. 14, uk. 105
6. Wasa’ilush-Shi’ah, Jz. 14, uk. 106
7. Sharh Lumu’ah, Jz. 2, uk.28
8. al-Mustahdathat min al-Masa’il al-Shar’yyah, uk. 19-20; swali la 26
9. Minhaj as-Salihin, Jz. 2, uk. 276
10. Kama ilivyotafsiriwa na Marhum Mulla Asgharali M.M. Jaffer.

Mlango Wa 5: Utungaji Wa Mimba

Vyakula Vinavyopendekezwa

Chakula anachokula mtu sio tu kwamba kina athari kubwa katika mwelekeo wa kiafya wa mtu, bali katika nafsi, moyo na akili vilevile. Kwa hiyo, inapendekezwa sana kwamba wazazi watarajiwa wajihadhari na vyakula vilivyoharamishwa, na hata vile vyakula ambavyo kuvila kunakuwa na wasiwasi.1

Kwa nyongeza, baadhi ya vyakula pia vimependekezwa makhsusi kabisa na Maimam kwa ajili ya mtoto mzuri na halali.

Kabla ya kutungwa mimba ya Hadhrat Fatimah (a.s.), Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu alikaa mbali na Hadhrat Khadijah kwa muda wa siku 40. Katika muda wa siku hizi 40, alifanya vitendo vya ibada na kufunga, na futari yake ilijumuisha chakula ambacho kililetwa kutoka mbinguni. Inapendekezwa kula vyakula vifuatavyo kabla ya kujaribu kutunga mimba:

1. Chicory – Aina Ya Majani Kwa Saladi

a. Imependekezwa kwamba baba atumie kula hiyo *chicory*.2

2. Komamanga

a. Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba: “Kula komamanga ni sababu ya uongezekaji wa utengenezaji wa manii kwa wanaume na kunafanya mtoto (anayezaliwa) kuwa mzuri na mwenye afya bora pia.3

b. Imesimuliwa kutoka kwa Imam ar-Ridhaa (a.s.): “Ulaji wa komamanga tamu unamfanya mwanaume kuwa na nguvu zaidi katika tendo la ndoa na kunaathiri sana uzuri wa mtoto.4

3. Qawoot

Qawoot ni unga au poda inayotengenezwa kutokana na usagaji na uchekechaji wa mchanganyiko ufuatao kwa viwango vinavyowiana: Ngano iliyokaangwa, shayiri iliyokaangwa, mbegu za ufuta zilizokaangwa, mbegu za tikiti la kawaida na za tikitimaji zilizokaangwa, mbegu za tikiti lenye mikunjo (*Deep Ribbed Melon)* zilizokaangwa, mbegu za *Purslane* zilizokaangwa, mbegu za *Coriandor* zilizokaangwa, mbegu za katani zilizokaangwa, mbegu za shamari (kiungo jamii ya karoti) zilizokaangwa, mbegu za mpopi zilizokaangwa, mbegu za dengu zilizokaangwa, ufuta, mbegu za *Pistachio*, kahawa, iliki, mdalasini, lozi/badamu, sukari.

Kwa vile mchanganyiko huu haupatikani katika nchi nyingi, inashauriwa kwamba vitu hivyo vilivyotajwa hapo juu viwe vinaliwa vyenyewe kimoja kimoja, kwa mfano pistachio na badamu.

b. Imependekezwa kwamba wote baba na mama wale *qawoot*: Imesimuliwa kwamba mtu mmoja alimwambia Imam as-Sadiq (a.s.):
“Ewe mwana wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, mtoto wa kiume ndio kwanza amezaliwa ambaye ni dhaifu na mwenye akili pungufu.” Imam ali- jibu akasema: “Kwa nini hamkuwahi kula qawoot? Kuleni qawoot na washaurini familia zenu kufanya hivyo pia. Kwa hakika, qawoot inafanya mnofu kukua na mifupa kuwa imara, na mtoto wa kiume hatazaliwa kutokana nanyi isipokuwa kwamba atakuwa mwenye nguvu.”5

c. Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): Kula qawoot pamoja na mafuta ya mzeituni na nyama kunamnenepesha mtu, kunafanya mifupa kuwa imara, kunaufanya mwili kung'ara na wenye nuru (Nur tukufu) na kunaongeza nguvu na uwezo wa kujamiiana."6

4. Quince (Tunda Aina Ya Pea)

a. Imesimuliwa kwamba Imam as-Sadiq (a.s.) alimuona mtoto mzuri na akasema: "Inaelekea kabisa kwamba huenda baba wa mtoto huyu alikula lile tunda quince – aina ya pea wakati wa usiku wa kutungwa kwa mimba yake."7

b. Imesimuliwa pia kutoka kwake yeye (a.s.) kwamba: "Kula quince kwenye usiku wa kutunga mimba kunafanya uso (wa kijusi) wa kupen- deza na mzuri, na moyo kuwa na nguvu na imara."8

c. Hadithi nyingine kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) anasimulia kwamba: "Yeyote atakayekula quince juu ya tumbo lenye njaa, chanzo cha uzal- ishaji wa mbegu (manii) inakuwa safi na yenye afya, na mtoto wake atakuwa mzuri na mwenye mwenendo mwema."9

d. Imesimuliwa kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikata tunda lake la quince vipande vipande na akampa Ja'far ibn Abi Talib kimoja na akamwambia: "Kula! Quince hii inaleta mng'aro wa rangi na kumfanya mtoto kuwa mzuri."10

Vitendo Vinavyopendekezwa

Ni muhimu sana kutambua kwamba vyingi ya vitendo vilivyotajwa katika sehemu hii ni sawa na vile vilivyodokezwa kwenye mlango wa Taratibu za mahusiano ya kujamiiana, pamoja na nyongeza ya jinsi zinavyoathiri mtoto aliyetungwa kwenye mimba.

Hali Ya Kimawazo:

Hali ya mawazo na moyo ya wazazi ina athari muhimu sana kwa mtoto. Matukio yafuatayo yanaakisi umuhimu wa hali ya kimawazo wakati wa kutunga mimba na matokeo yake

a.) Wakati Nabii Musa (a.s.) alipokuwa akifanya kazi kama mchungaji wa kondoo kwa Nabii Shu'aibu (a.s.), walifanya mapatano kwamba kon- doo yoyote kutoka kwenye kundi kondoo hao ambao watakuwa na rangi mbalimbali (wote wakiwa na rangi nyeusi na nyeupe), watalipwa kwa Nabii Musa (a.s.) kama mshahara wake. Baada ya mapatano haya, Nabii Musa (a.s.) aliifunika fimbo yake na ngozi yenye rangi na akaacha baadhi ya sehemu kama zilivyokuwa, akaning'iniza nguo (aba) yenye rangi kama hizo hizo juu ya fimbo hiyo na kisha akaiweka fimbo hiyo juu ya uwanja wa malisho. Wakati wa kuzaa, kondoo hao wata- iangalia fimbo hiyo.

Mwishoni mwa mwaka, ulipokuwa ni wakati wa kuchukua malipo, Nabii Shu'aib (a.s.) aliona kwamba wengi wa watoto wa kondoo walikuwa na rangi mbalimbali! Nabii Musa (a.s.) akaeleza kwamba haya yalikuwa ni matokeo ya moja kwa moja ya kuiangalia ile fimbo na nguo wakati
wa kuzaa.11

b.) Katika familia ya kiafrika, ambamo mume na mke wote walikuwa na ngozi nyeusi, walipata mtoto mwenye rangi ya hudhurungi (kama ile ya Mhindi mwekundu wa Marekani).

Walipokuwa wakilitafiti hili, wanasayansi wakagundua kwamba yule mume alikuwa na rafiki Mhindi wa Marekani na alikuwa ameweka picha ya rafiki yake huyo ukutani. Ule wakati wa kutunga mimba, macho yake yaliangukia kwenye ile picha na akawa anamfikiria rafiki yake huyo; wazo hilohilo likawa na athari kwenye manii na mtoto mwenye rangi ya hudhu- rungi, sawa na ile ya rafiki yake, ndipo akazaliwa.12

Kwa hiyo, wakati unapojaribu kutafuta kutunga mimba, inapendekezwa kwa kukokotezwa kabisa katika Uislam kwamba vitendo vilivyopen- dekezwa hapo chini vinashikwa ili kutunga mimba ya mtoto safi na mzuri.

1. Jaribu kutulia, kwani hili linasababisha muongezeko wa mzunguko wa damu na hivyo kupatikana mtoto wa kawaida. Imesimuliwa kutoka kwa Imam Hasan (a.s.) kwamba: “(Kama) kila wakati wa kutunga mimba, moyo unakuwa umetulia, mzunguko wa damu unakuwa wa kawaida na mwili unakuwa hauna fadhaa na wasiwasi wowote, basi mtoto atafanana na baba yake na mama.”13

2. Halikadhalika, uhusiano mzuri baina mume na mke na mvuto wa nguvu wa kimwili ni vya manufaa kwa mtoto, ambapo hofu na wasiwasi vitakuwa na matokeo tofauti, hasi juu ya mtoto.14

3. Kuwa mwenye wudhuu na kumdhukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwani hili linaleta utulivu na burudiko la moyo na lina athari chanya, nzuri kwenye manii na hivyo kupatikana mtoto mzuri.15

Mwenyezi Mungu analielezea hili ndani ya Qur’ani tukufu, katika Surat ar-Ra’d, aya ya 28:

الَّذِينَ آمَنُوا وَتَطْمَئِنُّ قُلُوبُهُمْ بِذِكْرِ اللَّهِ ۗ أَلَا بِذِكْرِ اللَّهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوبُ {28}

“Wale walioamini na kikatulia nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu, sikilizeni! Kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu, nyoyo hutulia!” (Ar-Ra’ad; 13:28).

4. Anza kwa Dua ifuatayo:

Imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.) kwamba kabla ya kitendo chenyewe, soma yafuatayo:
“Ewe Mola! Niruzuku na mtoto, na umfanye awe mchamungu. Fanya kusiwe na ziada au mapungufu katika kuumbwa kwake, na umjaalie na mwisho mwema.”16

Hali Ya Mwili

Hali ya mwili ya wazazi pia ina athari na matokeo ya kutambulika juu ya mtoto, na inaweza kupelekea kwenye udhaifu na ugonjwa kwa mtoto kama mtu hatakuwa mwangalifu.

1. Usifanye mapenzi ule usiku unaporudi kutoka safarini, au usiku unaokusudia kusafiri asubuhi yake, kwani mtu kwa kawaida anakuwa mchovu na aliyechoka kwenye usiku wa siku hizi. Imesimuliwa vile vile kwamba hili linaleta matokeo ya mtoto kuwa mzururaji na mbea,17 na mtoto huyo atatumia mali yake katika njia potovu.18

2. Usifanye mapenzi katika masaa ya mwanzo ya usiku, ukiwa na mwili uliochoka na kushiba kabisa, kwani hili linapelekea mtoto kuwa mchawi na kuchagua dunia juu ya akhera.19

Bali fanya mapenzi katika masaa ya baadae kabisa ya usiku, wakati kuchoka kwako takriban kumeondoka, na tumbo lako liko tupu. Imegunduliwa pia kwamba mtoto anayetungiwa mimba katika masaa ya baadae ya usiku anakuwa na akili zaidi.20

Kinga Kutokana Na Shetani

Ili kuweza kuzizuia athari za shetani katika usiku huu muhimu, vitendo vifuatavyopia vinapendekezwa kufanyika:

1. Weka nia kwamba unajaribu kutafuta mtoto, kwa ajili ya radhi na mku- ruba kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu

2. Kabla ya kujishughulisha na tendo lenyewe, soma Qur'ani na umshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa neema aliyokupa.

3. Kabla ya kushughulika na tendo lenyewe, anza na: **"Najikinga na shari za Shetani," kwa sababu hili linakuhakikishia kwamba mtoto atakayezaliwa atakuwa hana sifa za shetani.**

4. Soma: "*Bismillahir-Rahmaanir-Rahyim*."

5. Mkumbuke Mwenyezi Mungu kila mara, hususan wakati wa tendo lenyewe. Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba: "Wakati wowote mtu anapofanya mapenzi na mke wake, Shetani anakuwa yupo. Kisha kama jina la Allah linakumbukwa, Shetani anakwenda mbali sana kutoka hapo, lakini iwapo tendo litatokea na jina la Allah halikutajwa, shetani anachukuwa nafasi kwa kuwa yeye ndie mwenye manii hayo."21

Imesimuliwa pia kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba: "Wakati wowote unapotaka kufanya mapenzi na mke wako, mkumbuke Mwenyezi Mungu. Kwa sababu yoyote ambaye hatafanya hivyo, na mtoto akazaliwa kutokana naye katika hali hiyo, basi atakuwa anatokana na ushirikina wa shetani. Na usafi au kukosa usafi kwa mtoto kunatambulika kutokana na mapenzi na uadui juu yetu sisi Ahlul-Bayt."22

6. Soma Dua ifuatayo:

"Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Yeye Mmoja ambaye hapana mungu ila Yeye, Muumba wa mbingu na ardhi. Ewe Mungu wangu! Kama umenipangia katika usiku huu mrithi, basi usimfanye Shetani akawa na ushiriki, sehemu yoyote au fungu ndani yake mrithi huyo, na mfanye awe mu'min mwaminifu, msafi kutokana na Shetani na vitendo vyake viovu (utukufu wako ni mkuu)"23

"Kwa jina la Allah, na kwa Allah. Ee Allah! Muweke shetani mbali na mimi na muweke shetani mbali na kile ambacho una- nineemesha mimi nacho."24

7. Kazieni mapenzi ya Ahlul-Bayt (a.s.) ndani ya nafsi zenu. Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba: "Wakati mwingine Shetani huja karibu na wanawake kama waume zao." Alipoulizwa ni namna gani ya kutambua iwapo kama Shetani anayo sehemu katika

utungwaji wa mimba za watoto wetu au laa, Imam akajibu akasema: “Kwa njia ya mapenzi au chuki kwetu sisi (a.s.). Hivyo mtu yoyote anayetupenda sisi, Shetani hana sehemu katika kuzaliwa kwake, na yeyote ambaye ni adui yetu sisi, mbegu (manii) yake imetoka kwa Shetani.25

Imesimuliwa katika Hadith kwamba Shetani amesema: “Yeyote ambaye ni adui wa Imam Ali (a.s.), basi bila shaka yoyote mimi nilishiriki katika kile kitendo kati ya baba yake na mama yake.”26

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba: “Watieni msuku- mo (wafundisheni) mabinti zenu na wanawake urafiki wa familia ya Ali (a.s.) na (hivyo) kuwafanya wabaki na hali (ya moyo safi na kuwa mbali na Akhlaq iliyopinda, mbaya).27

Kiangalizo: Mapenzi juu ya Ahlul-Bayt (a.s.) hayamaanishi kwamba tutamke upendo juu yao tu basi, bali hasa ni kuwachukulia kuwa ni mfano wa kuigwa katika kila jambo la maisha yetu ya kila siku na kujitahidi kufanya kazi ya kuuelekea mfano wao.

8. Hakikisha uhusiano wako unaruhusiwa na ni halali. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Imam Ali (a.s.): “Ewe Ali! Yeyote yule anayenipenda mimi na wewe na Maimam kutokana na kizazi chako, basi (wanapaswa) wamshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhalali wake huo, kwa sababu haku- na yoyote bali wale ambao ni halali (wa kuzaliwa) ndio wanaotupenda sisi na hakuna yoyote bali wale ambao ni haramu (kwa kuzaliwa) ambao ni maadui zetu.”28

Kwa hakika, wakati wa kipindi cha Imam Ali (a.s.), njia ya kutambua iwapo kama watoto walikuwa wa halali ama laa ilikuwa ni kuwaleta karibu na Imam na kuona kama walimpenda ama hapana.29

Matendo Yasiyoshauriwa Kufanywa

Ni muhimu kufahamu kwamba vingi ya vitendo vilivyotajwa katika sehemu hii vinafanana na vile vilivyoelezwa kwenye mlango wa Adabu za mahusiano ya kujamiiana, pamoja na nyongeza ya jinsi vinavyoathiri mtoto anayezaliwa.

Vitendo Vya Makruhu (Vya Karaha)

Kwa vile vitendo vingine vina athari hasi, mbaya juu ya mtoto kama vile chuki dhidi ya Ahlul-Bayt (a.s.),30 inashauriwa kwamba vitendo vilivy- otajwa hapa chini viwe vinaepukwa:

1. Kuangalia kwenye sehemu nyeti za siri za mwanamke wakati wa kitendo chenyewe hasa, kwani hili linapelekea kwenye upofu wa mtoto atakayezaliwa.31

2. Kuzungumza wakati wa kitendo chenyewe (isipokuwa kwa kudhukuru Allah (s.w.t.).), kwani hili linapelekea kwenye ububu wa mtoto atakayezaliwa.32

3. Kuwa na hinna juu ya mwanaume, kwa vile hili husababisha ukhuntha wa mtoto anayezaliwa (yaani, msichana anakuwa na tabia za kiume na kinyume chake).33

4. Kufikiria au kutamani mwanamke mwingine wakati wa kitendo, kwa vile hili linapelekea kwenye wenda wazimu wa mtoto atakayezaliwa.34

5. Kufanya mapenzi mbele ya mtoto, ambaye ama anaweza kuona au kusikia sauti za

kitendo hicho, kwani hili linaleta matokeo ya mtoto huyo kutokuja kuokolewa (kutoka kwenye moto wa Jahannam) na kuwa mzinifu.35

6. Kufanya mapenzi wakati ambapo kuna mtu aliyeko macho ndani ya nyumba, ambaye anaweza kuona au kusikia sauti za kitendo hicho, kwani hili linaleta matokeo ya mtoto kutokuja kuokolewa (kutoka kwenye moto wa Jahannam) na kuja kuwa mzinifu.36

7. Kufanya mapenzi kwa kusimama wima, kwani hili linapelekea mtoto kuwa na tatizo la kukojoa kitandani**.**37

8. Kufanya mapenzi juu ya paa la nyumba, kwani hili linaishia kwenye mtoto kuwa mnafiki, na mmbea (mzushi).38

9. Kufanya mapenzi chini ya mti wa matunda, kwani hili linapelekea mtoto kuwa muuaji na kiongozi wa udhalimu**.**39

10. Kufanya mapenzi chini wa mwanga wa moja kwa moja wa jua, kwani hili linapelekea mtoto kuwa masikini, hata mpaka kifo chake.40

11. Kufanya mapenzi wakati mwanaume yuko katika hali ya *Muhtalim* (yaani, anapokuwa na hali ya janaba kwa ndoto usingizini mwake) na kabla ya kuchukua Wudhuu au Josho, kwani hili linasababisha mtoto kuja kuwa mwendawazimu.41

Ni muhimu vilevile kuzingatia akilini vitendo vinginevyo vile vyenye karaha – Makruh – wakati wa taratibu za kawaida za mahusiano ya kujamiiana (kama zilivyoelezwa kwenye Mlango wa 2: Adabu za Mahusiano ya Kujamiiana). Hivi ni vifuatavyo:

1. Kuwa na Qur’ani au Majina ya Allah (s.w.t.). mwilini mwako.
2. Kufanya mapenzi ukiwa uchi kabisa (bila cha kujifunika).
3. Kufanya mapenzi barabarani au ndani ya boti.
4. Kuelekea au kukipa mgongo Qibla.
5. Kukataa kujamiiana (kwa sababu mbalimbali – za visingizio).

Kiangalizo: Mara mwanamke anapokuwa kaishapata ujauzito, inashauri- wa kujiepusha kutokana na kufanya mapenzi bila ya Wudhuu, kwani hili linasababisha mtoto kuwa masikini na upofu wa ndani42

Nyakati Zinazoshauriwa

Ni muhimu kutambua kwamba nyingi ya nyakati zilizotajwa katika mlan- go huu ni sawasawa na zile zilizotajwa kwenye mlango wa Taratibu za Kujamiiana, pamoja na nyongeza ya jinsi zinavyomuathiri mtoto anayezaliwa.

Nyakati Zinazofaa (Mustahab)

1. Usiku wa Jumapili (kuchea Jumatatu). Mtoto anayetungwa kwenye mimba usiku huu atakuwa mwenye kuridhika na chochote Mwenyezi Mungu Mtukufu atakachomjaalia nacho, atakuwa na kumbukumbu nzuri na atakuwa Hafidh (mwenye kuhifadhi) wa Qur’ani Tukufu.43

2. Usiku wa Jumatatu (kuchea Jumanne). Mtoto anayetungiwa mimba kwenye usiku huu atakuwa na ustawi au neema ya Uislamu, na fursa ya Shahadat na hatoadhibiwa pamoja na

washirikina. Atakuwa na kinywa kilicho na harufu nzuri na moyo wa huruma. Atakuwa ni mtu mwenye kutoa sadaka na ulimi wake utasalimika na kusema uongo, kusengenya au kutoa shutuma za uongo.44

3. Usiku wa Jumatano (kuamkia Alhamisi) Mtoto anayetungwa mimbani kwenye usiku huu atakuwa mtawala miongoni mwa watawala wa Shari'ah, au mwanachuoni miongoni mwa wanachuoni
wa kidini.45

4. Mchana wa Alhamisi, wakati wa kumalizika kwa mchana. Huu ndio muda muafaka, bora kabisa na umependekezwa sana kwa ajili ya utun- gaji mimba. Shetani hatasogea karibu na mtoto anayetungwa kwenye mimba usiku huu mpaka anapokuja kuzeeka na usalama wa dini na dunia utakuwa wake.46

5. Usiku wa Alhamisi (kuchea Ijumaa). Mtoto anayetungwa mimbani kwenye usiku huu atakuja kuwa mubalighin, msemaji fasaha na msomaji wa Qur'ani.47

6. Siku ya Ijumaa, baada ya wakati wa Alasiri. Mtoto atakayetungwa mimbani wakati huo atajulikana sana miongoni mwa watu wenye busara na wanachuoni wakubwa.48

7. Siku ya Ijumaa, baada ya wakati wa swala Isha. Mtoto atakayetungwa kwenye mimba wakati huo atakuwa anatokana na watu wema na wanaofaa.49

8. Usiku wa kwanza wa mwezi wa Ramadhani.50

Nyakati Zisizopendekezwa

Ni muhimu kutambua kwamba nyingi ya nyakati zilizotajwa katika mlango huu ni sawasawa na zile zilizotajwa katika mlango wa Taratibu za Kujamiiana, pamoja na nyongeza ya jinsi zinavyoathiri mtoto anayezaliwa.

Nyakati Haramu

1. Wakati wa kipindi cha hedhi ya mwanamke, hata katika ile siku ya mwisho, mpaka tone la mwisho la damu litakapodondoka. Ujauzito bado unawezekana, na mtoto atakayetungwa mimbani atasumbuliwa na (*phagedemic ulcers*) – aina ya vidonda vya tumbo na ukoma.51

Imesimuliwa vile vile kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba: "Hakuna adui kwetu sisi Ahlul-Bayt, isipokuwa yule ambaye amezaliwa kwa njia ya haramu na yule ambaye alitungwa mimbani wakati wa hedhi.52

Ni muhimu vile vile kuzingatia akilini vitendo vingine haramu wakati wa taratibu za kawaida za kujamiiana (kama zilivyotajwa katika Mlango wa 2: Taratibu za Kujamiiana): Hizi ni:

1. Wakati wa Nifaas
2. Wakati wa saumu katika mwezi wa Ramadhani
3. Wakati katika hali ya Ihraam
4. Wakati ambapo inaweza kusababisha madhara makubwa ama kwa mume au kwa mke.

Nyakati Za Karaha (Makruh)

1. Kati ya asubuhi sadiki (Adhana ya swala ya al-Fajr) na kuchomoza kwa jua.53

2. Kati ya kuzama kwa jua mpaka kupotea kwa wekundu wa angani.54
3. Usiku wa kupatwa kwa mwezi.55
4. Mchana wa kupatwa kwa jua.56
5. Wakati wa tetemeko la ardhi (au matukio mengine yanayolazimu Swala – *Salat al-Ayat*).57

Kama atatungwa kwenye mimba katika nyakati hizo hapo juu, wazazi hawataona sifa yoyote wanayoipenda kwa mtoto wao, kwa sababu hawakuziona hizi ishara za Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa za muhimu.58

6. Katika tarehe ya mwanzo wa mwezi (isipokuwa mwezi mosi ya Ramadhani, ambapo ni mustahab), katikati ya mwezi (unapoonekana mwezi kamili) na mwishoni mwa mwezi (kunapokuwa hakuna mwezi), kwani itakuwa ni chanzo cha hali ya wendawazimu, ukoma mweusi na kupooza kwa mama na mtoto.59

Hadithi nyingine inasimulia kwamba kutunga mimba wakati wa mwanzo wa mwezi na katikati ya mwezi kunapelekea kwenye wendawazimu na mtoto kutawaliwa na Jinni,60 na kutunga mimba wakati wa mwisho wa mwezi kunaongezea uwezekano wa kuharibika kwa mimba.61

7. Baada ya swala ya Adhuhuri (mpaka takriban karibu na wakati wa Asr), kwani hii inapelekea mtoto kuwa na makengeza.62

8. Kati ya Adhana na Iqaamah kwani hii inapelekea kwa mtoto kuwa shauku ya kuua.63

9. Usiku wa Eid al-Fitr, kwani hii inasababisha katika mtoto kuwa chanzo cha maovu.64

10. Usiku wa Eid al-Udh’haa, kwani hilo linapelekea kwa mtoto kuwa na vidole (sita) 6 au (vinne) 4.65

11. Usiku wa nusu ya Shaaban (mwezi 15), kwani hili linapelekea kwenye mtoto kuwa na hali ya ndege mbaya (nuksi au kisirani) na alama nyeusi usoni mwake.66

12. Siku ya mwisho ya mwezi wa Sha’ban, kwani hii inapelekea kwa mtoto kuwa msaidizi na mkusanyaji kodi wa madhalimu.67

13. Usiku wa Ashuraa’.

Kupanga Mimba

Tunaweza kuhitimisha kutokana na yote hayo hapo juu kwamba lengo la mahusiano ya kijinsia ni la njia mara mbili: kuridhisha haja ya mtu ya kimaumbile na kuzaa.

Miongozo kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Ahlul-Bayt wake (a.s.) kwa wazi kabisa inaonyesha urefu wa muda ambao mtu anaweza kuchukua ili kupata mtoto anayefaa. Mahusiano ya kijinsia kwa ajili ya utungaji mimba yanapaswa kufanywa kwa tofauti kabisa, vyote kiakili na kivitendo.

Wakati mwingine, inaweza kutokea kwamba kutokana na ukosefu wa taar- ifa au sababu nyinginezo, mazingira ya upatikanaji wa mimba ya mtoto yanakuwa hayakupangwa. Taarifa hiyo hapo juu inaweza kwa hiyo kuwa chanzo cha wasiwasi kwa ajili ya wazazi kuhusu matokeo yanayowezekana ya utungaji wa mimba katika nyakati na kwa vitendo visivyopendeza.

Ni muhimu kuzingatia akilini kwamba kuna mambo mengi yanayochangia katika utengenezaji wa mtoto, kama vile hali asili ya kurithi (*genetics*), lishe, hali ya kijamii, na kadhalika.
Taarifa zilizotajwa hapo juu ni baadhi tu ya haya mambo ambayo yanaweza kuathiri mtoto aliyezaliwa.

Kwa nyongeza, inawezekana kuyakinga matokeo ya kijyume yanay- owezekana kutokea kwa vitendo kama vile sadaka, kusoma Qur'ani na kutafuta tawasali (uombezi mtukufu) kutoka kwa Ahlul-Bayt (a.s.).68

1. Surat al-Baqarah, aya ya 168: "Enyi watu! Kuleni katika vile vilivyomo ardhini vilivyo halali na vizuri."
2. Vilevile inajulikana kama Succory, huu ni mtishamba ambao mizizi yake iliyokaushwa, kusagwa na kukaangwa inatumika kama kighushi cha, au kitu mbadala na kahawa.
3. Wasa'ilush-Shi'ah, Jz. 25, Uk. 104, namba 31499
4. al-Kafi, Jz. 5, Uk. 35
5. Biharul-Anwar, Juz. 66, Uk.278
6. Ibid, Juz. 104, Uk. 80
7. Makatimul-Akhlaq, uk. 88
8. Barqaa'i, Uk. 549
9. Biharul-Anwar, Juz. 81, Uk. 101
10. Wasa'ilush-Shi'ah, Jz. 25, uk. 165 hadithi ya 31538
11. Bahdasht Izdawaaj az Nazr Islam, Uk. 89
12. Izdawaaj Asaan; Uk k. 245
13. Biharul-Anwar, Jz. 14. Uk. 379
14. Rayhaan-e Beheshtii, Uk. 33
15. Rayhaan-e Beheshtii, Uk. 39
16. Wasa'ilush-Shi'ah, Jz. 20, Uk. 117, Hadithi ya 25180
17. Wasa'ilush-Shi'ah, Jz. 20, uk. 253, Hadithi ya 25560
18. Hilliyatul Muttaqin, uk. 112-114
19. Ibid.
20. Rayhaan-e Beheshtii, uk. 40
21. Al-Kafi, Jz. 5, uk. 502
22. Sharh Man laa Yahdhural Faqii, Jz. 8, Uk . 202
23. Al-Kafi, Jz. 5, Uk. 503
24. Al-Kafi, Jz. 5, uk. 503
25. Tafsir Nur al-Thaqalayn, Jz. 3, Uk . 183
26. Niyazhaa wa Rawabith Maadaraan wa Janiin, Uk. 76
27. Sharh Man laa Yahdhural Faqii, Jz.3, Uk. 493
28. Al-Amaali cha Sheikh Saduq, Jz. 7, Uk. 383
29. Manaaqib ya Ibn Shahr Ashuub, Jz.3, Uk k. 207
30. Biharul-Anwar, Jz. 39, uk. 278, Hadithi ya 87
31. Wasa'ilush-Shi'ah, Jz. 20, Uk. 122, Hadithi ya 25197
32. Wasa'ilush-Shi'ah, Jz. 20, Uk. 121, Hadithi ya 25195
33. Wasa'ilush-Shi'ah, Jz. 20, Uk. 125, Hadithi ya 25205
34. Hilliyatul Muttaqiin, Uk. 112-114
35. Wasa'ilush-Shi'ah, Jz. 20, uk. 133, Hadithi ya 25223
36. Niyaazhaa wa Rawaabith Jinsii was Zanaashuii, Uk. 64
37. Hilliyatul Muttaqiin, Uk. 112-114
38. Ibid. (Hilliyatul Muttaqiin, uk. 112-114)
39. Hilliyatul Muttaqiin, Uk. 112-114

40. Hilliyatul Muttaqiin, Uk. 112-114
41. Wasa’ilush-Shi’ah, Jz. 20 Uk . 148, Hadithi ya 25271
42. Wasa’ilush-Shi’ah, Jz. 20, Uk. 148
43. Hilliyatul Muttaqiin, Uk k. 112-114
44. Hilliyatul Muttaqiin, Uk. 112-114
45. Hilliyatul Muttaqiin Uk. 112-114
46. Hilliyatul Muttaqiin, Uk. 112-114
47. Hilliyatul Muttaqiin Uk. 112-114
48. Hilliyatul Muttaqiin, Uk. 112-114
49. Hilliyatul Muttaqiin, Uk. 112-114
50. Hilliyatul Muttaqiin, Uk. 112-114
51. Hilliyatul Muttaqiin, Uk 110
52. Niyaazhaa wa Rawaabith Jinsii was Zanaashuii, uk. 69
53. Wasa’ilush-Shi’ah, Jz. 20, Uk. 126-127, Hadihi ya 25207
54. Ibid
55. Ibid
56. Ibid
57. Ibid
58. Niyaazhaa wa Rawaabith Jinsii was Zanaashuii, uk. 59
59. Wasa’ilush-Shi’ah, Juz. 20, Uk 129, hadithi ya 25214
60. Wasa’ilush-Shi’ah, Juz. 20, Uk. 129, hadithi ya 25212
61. Wasa’ilush-Shi’ah, Juz. 20, Uk. 129, hadithi ya 25208
62. Hilliyatul Muttaqin, Uk. 112-114
63. Hilliyatul Muttaqin, Uk. 112-114
64. Hilliyatul Muttaqin, Uk. 112-114
65. Hilliyatul Muttaqin, Uk. 112-114
66. Hilliyatul Muttaqin, Uk. 112-114
67. Hilliyatul Muttaqin, Uk. 112-114
68. Imethibitishwa na ofisi ya Ayatullah Sistanii, Qum.

Mlango Wa 6: Mimba

Kuumbwa Kwa Mtoto Kwa Mujibu Wa Qur’ani Tukufu

Katika aya kadhaa za Qur’an Tukufu, Mwenyezi Mungu ametaja uumbaji wa mtoto na hatua za mabadiliko mtoto. Ni kwa kuchunguza muujiza huu ambapo mtu anapenda bila kupinga, kumshukuru na kumtukuza Yeye, Mbora wa Waumbaji.

Katika Suratul-Mu’minun, aya ya 12 – 14, Yeye anasema:

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ سُلَالَةٍ مِنْ طِينٍ {12}

ثُمّ جَعَلْنَاهُ نُطْفَةً فِي قَرَارٍ مَكِينٍ {13}

ثُمّ خَلَقْنَا النُّطْفَةَ عَلَقَةً فَخَلَقْنَا الْعَلَقَةَ مُضْغَةً فَخَلَقْنَا الْمُضْغَةَ

عِظَامًا فَكَسَوْنَا الْعِظَامَ لَحْمًا ثُمّ أَنْشَأْنَاهُ خَلْقًا آخَرَ فَتَبَارَكَ اللّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ {14}

"Bila shaka tulimuumba mwanadamu kutokana na asli ya udongo. Kisha tukamuumba kwa tone la manii, lililowekwa katika makao yaliyohifadhika. Kisha tuliumba tone hilo kuwa pande la damu, na kukalifanya pande la damu hilo kuwa nyama, kisha tukalifanya pande hilo kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama, kisha tukamfanya kiumbe kingine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu, Mbora wa waumbaji." (al-Mu'minun; 23: 12-14).

Katika aya hizo hapo juu, Mwenyezi Mungu Mtukufu anataja hatua 7 za uumbaji:

Hatua ya kwanza: Mwanadamu mwanzoni kabisa anaanza kama udongo; kwa maneno mengine, sehemu za udongo zisizo na uhai zinavyotunzwa kwenye mwili hai kwa njia ya chakula.

Hatua ya Pili: Chembehai inajizalisha yenyewe kwa njia ya manii; hivyo mwanadamu anatengenezwa katika mbegu (majimaji ya shahawa), na kuwekwa katika sehemu madhubuti ya kupumzika (tumbo la uzazi la mama).

Hatua ya Tatu: Mabadiliko ya kwanza katika ovari iliyorutubishwa ni ubadilishaji kwenye namna ya donge au mgando mzito wa damu, au bonge lililoning'inia.

Hatua ya Nne: Chembehai za zaigoti hukua kwa ugawanyikaji katika pingili; halafu donge hilo huanza taratibu kupata umbile katika kukua kwake kama kijusi (bonge la nyama).

Hatua ya Tano: Kutokea hapa inaanza mifupa.

Hatua ya Sita: Nyama sasa hukua juu ya mifupa, kama vinavyofanya viungo na mfumo wa neva.

Hatua ya Saba: Hadi hapo ukuaji wa mtoto wa binadamu ni kama ule wa mnyama. Hata hivyo, hatua muhimu sasa inachukuliwa na kile kijusi kinakuwa binadamu kamili. Huu ni ule upuliziaji wa roho ya Mwenyezi Mungu ndani yake. (huu unaweza kuwa sio muda maalum; bali unaweza kuwa sambamba na ule wa ukuaji wa kimwili).

Katika suala la uumbaji wa kijusi, inasimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Ile mbegu ndani ya tumbo la uzazi la mama inachukua siku arobaini kugeuka kuwa bonge, kisha baada ya siku arobaini linakuwa donge la nyama (kijusi); wakati mtoto anapofikia

miezi minne, kwa amri ya Mwenyezi Mungu, Malaika wawili hukipa kile kijusi roho na kuainisha riziki, muda wa kuishi, matendo (Aamaal), ustawi na dhiki za mtoto huyo.1

Huenda ni kwa sababu hii kwamba imeshauriwa kwamba hususan baada ya siku ya arobaini ya kujamiiana, mtu anapaswa kuwa muangalifu zaidi wakati anapoandaa chakula. Chakula hicho lazima kiwe kisafi kiroho (kisiwe najisi) na kiwe halali kwani hili litakuwa na athari juu ya mtoto huyo.2

Imam as-Sadiq (a.s.) vilevile aliielezea hatua ya maendeleo ya uumbaji kama ifuatavyo: “Baada ya kukamilika viungo vya mwili vinavyohitajika, Mwenyezi Mungu anatuma Malaika wawili ambao wana kazi ya uundaji wa mtoto, na kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, wao huunda masikio na macho na viungo vyote vya ndani na vya nje vya mwili huo.”3

Katika Dua ya Imam Husein ya Aarafat, anarejelea kwenye mfuatano wa uumbwaji na anajaribu kuzihesabu zile neema zilizotolewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu katika namna ifuatayo:

“Umeniasilisha mimi kwa Rehma Zako
kabla sijawa kitu cha kukumbukwa
Umeniumba kwa udongo,
Kisha ukanipatia nafasi katika migongo ya baba zangu
Salama kutokana wasiwasi wa maangamizi na
matukio ya ajabu ya zama na miaka.

Nilibaki kuwa napita kutoka mgongo hadi tumbo kwa muda
Nisioukumbuka wa siku zilizopita
Na karne zilizokwishapita.

Katika upole Wako, neema na wema kwangu mimi,
hukunipeleka kwenye himaya ya viongozi wa ukafiri,
wale ambao walivunja ahadi Yako na
wakatangaza uongo kwa mitume Wako.

Bali ulinipeleka kwenye ule mwongozo
ambao ulikwishaamuliwa mapema kwa ajili yangu,
namna ulivyoniwepesishia na ulivyonilea.

Na kabla ya hapo ulikuwa na huruma juu yangu
kupitia ufanya mitindo Wako wa hisani na neema tele.
Ulianzisha uumbwaji wangu kutoka kwenye tone la manii
Lililomwagika na ukanifanya nikae kwenye utusitusi mara tatu
miongoni mwa nyama, damu na ngozi.
Hukunipa mimi kushuhudia kuumbwa kwangu,
wala hukuniaminisha mimi na lolote kati ya mambo yangu.
Kisha ukanituma duniani kwa ajili ya mwongozo
ambao ulikwisha kuamuliwa kwa ajili yangu,
kikamilifu na usioharibika.”4

Imam Zainul-Abidiin (a.s.) katika du’a yake baada ya Sala ya usiku – Salatul-Lail ndani ya Sahifah Sajjadiah anakitaja hiki kipindi cha kushangaza cha kijusi na cha wakati wa kunyonya. Anamshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuelezea mshangao wake juu ya jinsi Allah (s.w.t.). alivyoumba kiumbe kizuri kama hicho kutokana na mbegu chache.

“Ewe Mungu Wangu,
Umenifanya nishuke kama maji duni
kutoka kwenye viuno vyenye mifupa myembamba na njia finyu,
kwenda kwenye tumbo la uzazi linalosonga,
ambalo ulikuwa umelifunika kwa mastara;

Umenigeuza geuza kutoka hali hii hadi hali ile
mpaka ukanitengeneza kwenye umbo kamilifu
na ukaweka ndani yake viungo vya kimwili,
kama ulivyoeleza kwenye Kitabu Chako:
Kwanza tone,
kisha bonge,
kisha pande (la nyama),
kisha mifupa,
kisha ukaivisha mifupa kwa nyama,
kisha ukanitoa mimi kama kiumbe mwingine kama ulivyopenda.

Halafu pale nilipohitaji riziki Zako,
na nikawa siwezi kufanya lolote bila ya msaada wa neema Zako,
ulinichagulia kirutubisho kutoka kwenye neema ya chakula na vinywaji,
ambacho ulikiweka mikononi mwa mtumishi Wako,
ambaye kwenye tumbo lake ulinipa mimi mapumziko,
na kwenye makazi ambamo tumboni mwake Wewe ulinihifadhi mimi.

Kama ungeniaminisha mimi katika hatua zile, Ewe Mola Wangu,
kwenye bidii zangu au ungenisukuma kupata msaada
kwenye nguvu zangu mwenyewe
bidii ingeniondoka na nguvu zingechukuliwa mbali kabisa.

Hivyo umenilisha kupitia neema Zako
kwa chakula cha wale Wema na Wapole;
Umefanya hivyo kwa ajili yangu kwa fadhila kwangu
hadi kwenye hatua yangu hii ya sasa
Mimi siukosi wema Wako
wala fadhila Zako haziniweki mwenye kusubiri.

Bado pamoja na yote hayo,
imani yangu haijawa thabiti vyakutosha,
kwamba ningeweza kujikomboa mwenyewe
kwa kile ambacho kinapendelewa zaidi na Wewe.”[5]

Katika moja ya Hadith al-Qudsi, Mwenyezi Mungu Mtukufu anazungumza na wale wasio na shukurani na anasema: “Ewe mwanadamu! Hujanitendea Mimi haki! Niliufanya uzito wako kuwa mwepesi ndani ya tumbo la mama yako!

Baada ya hapo nilifanya njia ya kuzaliwa kwako kutoka kwenye sehemu finyu na ya giza kuwa laini (na inayovumilika). Pale ulipoweka mguu duniani nje ya tumbo hilo, niliona kwamba ulikuwa huna meno ya kulia chakula; niliweka matiti yaliyojaa maziwa katika kifua chenye joto cha mama (yako). Niliufanya moyo wa mama yako kuwa wenye huruma juu yako, na moyo wa baba yako wenye upendo, kiasi kwamba wanabeba uzito wa kukupa wewe chakula, na hawalali mpaka wahakikishe kwamba wewe umelala.

“Ewe mwana wa Adam! Fadhila zote hizi hazikuwa kwa sababu uliziom- ba kutoka Kwangu, wala kwamba Mimi nilikuhitaji wewe. Na pale hali ya uundwaji wako wa kimwili ilipokuwa tayari, na meno yako yakaota, nilik- ufanya ufurahie (na ufaidike) kutokana na aina tofauti za vyakula na matunda ya kiangazi na kipupwe.

Hata hivyo! Licha ya huruma zote hizi, baada ya kuwa hukunitambua Mimi (kama Muumba Wako na Mpaji Wako), ukaniasi Mimi.”6

Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) amesema kwamba: “Pepo ya mtu iko chini ya nyayo za
mama yake.”7

Mwenyezi Mungu Mtukufu anaeleza ndani ya Qur’ani Tukufu, katika *Surat al-Faatir*, aya ya 11 hivi:

وَمَا تَحْمِلُ مِنْ أُنْثَىٰ وَلَا تَضَعُ إِلَّا بِعِلْمِهِ ۚ {11}

“….. Na mwanamke yeyote hachukui mimba wala hazai ila kwa elimu Yake …..” (Surat Al-Faatir; 35:11).

Imesimuliwa pia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Kama imea- muliwa kwamba Mwenyezi Mungu atafanya mtoto azaliwe, Yeye atamuumba katika umbile lolote lile alipendalo.”8

Hii inatuonyesha sisi kwamba uzazi wa mtoto ni neema ya moja kwa moja kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na ambako kunapaswa kutolewa shukurani endelevu juu yake. Kwa kweli kuwepo kwa mtoto kumefananishwa na tunda la mti, ambako kunamsogeza mwanamke na mwanaume karibu zaidi na kila mmoja wao.

Na kuhusu akina mama, Uislamu umewafanyia dunia nzuri ya kupendeza, ambamo kila mmoja lazima awaheshimu na kuwaenzi. Mwenyezi Mungu Mtukufu anayatambua na kuyataja matatizo yanayobebwa na akina mama: Katika Surat Luqmaan, aya ya 14, Yeye anasema:

حَمَلَتْهُ أُمُّهُ وَهْنًا عَلَىٰ وَهْنٍ {14}

“….. Mama yake amembeba kwa udhaifu juu ya udhaifu….. (Surat Luqmaan; 31:14).

Katika Surat al-Ahqaf, aya ya 15, Yeye anaelezea hivi:

حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا ۖ {15}

“….. Mama yake amechukua mimba yake kwa taabu, na akamzaa kwa taabu ….. (Surat Al-Ahqaf; 46:15).

Kwa hakika hadhi ya akina mama ni hali ya juu zaidi hata kuliko ya baba kama inavyoonyeshwa na hadithi zinazofuata:

Mtu mmoja alikuja kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akamwambia, “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, je nifanye wema kwa nani?” Mtume (s.a.w.w.) akasema, “Kwa mama yako.” Hivyo, yule mtu akasema, “Na baada ya hapo nifanye wema kwa nani?” Mtume (s.a.w.w.) akasema, “Mama yako.”

Halafu yule mtu akauliza tena, “Na halafu tena nifanye wema kwa nani?” Mtume (s.a.w.w.) akajibu. “Mama yako.” Halafu yule mtu akasema tena, “Baada ya hapo, nifanye wema kwa nani? Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema, “Kwa baba yako.” 9

Imesimuliwa vilevile kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliulizwa, “Ni yupi kati ya wazazi wawili ambaye ana cheo kikubwa?” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akajibu, “Yule ambaye, kwa muda wa miezi tisa yeye amekuwe- ka katikati ya pande mbile (tumbo la uzazi), na kisha akakuleta duniani humu na akakupa maziwa kutoka kwenye matiti yake.” 10

Kuna ahadith nyingi kuhusu umuhimu wa akina mama wajawazito na wanaonyonyesha, baadhi yake ambazo zitasimuliwa hapa chini. Hata hivyo, inapasa kuzingatiwa akilini kwamba hizo zinakwenda bega kwa bega pamoja na majukumu ambayo yanapasa kubebwa kwa kadiri ya uwezo wake wote mtu.

Majukumu hayo kwa kawaida yanakuwepo wakati mtu anapokuwa na dhamira ya kufikia daraja za juu za Akhlaq na ukaribu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na akapenda kufanya bidiii kuelekea kwenye lengo hili la kimaadili. (Haya yatajadiliwa kwa kina zaidi katika sehemu zinazofuata.).

a) Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Malipo ya mwanamke, kuanzia wakati wa ujauzito hadi wakati wa kuzaa kwake na kunyonyesha, ni sawasawa na yale ya mtu aliyeko kwenye njia (jihadi) ya Allah, na iwapo mwanamke anafariki dunia katika muda huo kwa sababu ya matatizo na machungu ya uzazi, anakuwa na malipo ya shahidi.”11

b) Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Wakati wowote mwanamke atakapoiacha dunia hii kwa sababu ya maumivu ya uzazi, katika Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu atamfufua kutoka kwenye kaburi lake akiwa msafi bila ya hesabu (ya dhambi); kwa sababu mwanamke kama huyo ameyatoa maisha yake kutokana na matatizo na uchungu wa uzazi.”12

c) Imesimuliwa vilevile kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Kila wakati mwanamke anapokuwa na mimba, katika muda wote wa kipindi cha ujauzito anakuwa na cheo cha mtu anayefunga, mtu anayefanya ibada wakati wa usiku, na mtu anayepigana katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa uhai na mali yake. Na wakati anapojifungua, Mwenyezi Mungu humpa thawabu nyingi sana kiasi ambacho hakuna anayeweza kujua mpaka wake kwa sababu ya ukubwa wake.

Na pale anakumnyonyesha mwanawe, kwa kila mfyonzo mmoja wa mtoto huyo, Mwenyezi Mungu humpa malipo ya kumuachia mtumwa mmoja kutoka kwa wana wa Isma’il, na wakati kile kipindi cha kumnyonyesha mtoto kinapokamili- ka, mmoja wa Malaika wakuu wa Mwenyezi Mungu humgusa upande wake mmoja na kusema: “Anza matendo yako upya,

kwani Mwenyezi Mungu amekwisha kukusamehe makosa yako madogo madogo yote.”13

d) Katika wakati wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), mtu mmoja alikuwa anafanya Tawaf (ya Ka’ba Tukufu), akiwa amembeba mama yake mabegani mwake. Wakati alipomuona Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), alimuuliza, “Kwa kufanya hivi, je, nitakuwa nimelipa haki za mama yangu?” Kwa hili Mtume (s.a.w.w.) alijibu, “Hapana, hujalipa hata angalau moja ya vile vilio vyake vya wakati ule wa kukuzaa wewe.” 14

e) Mtu mmoja alikuja kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akauliza: “Ninaye mama yangu mzee, ambaye kwa sababu ya umri wake wa uzee hawezi hata kusogea. Ninambeba kwenye mabega yangu na kumuwekea vipande vya chakula mdomoni mwake na kumsafisha. Je, nimelipa haki zake?” Kwa swali hili Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alijibu, “Hapana, kwa sababu tumbo lake lilikuwa mahali pako wewe, na katika muda wote huo, aliyapenda maisha yako.” 15

f) Imesimuliwa kutoka kwa Imam Zainul-Abidiin (a.s.): “Haki ya mama yako ni kwamba ujue kwamba yeye alikubeba mahali ambapo hakuna mtu anayembeba yoyote. Amekupa kutokana na tunda la moyo wake ambalo hakuna mtu anayelitoa kwa yeyote, na amekulinda kwa viungo vyake vyote. Yeye hakujali kama angekuwa na njaa ilimradi wewe uwe umekula umeshiba, au kama alikuwa na kiu madhali wewe umekunywa, hakujali iwapo angetembea bila nguo ilimradi wewe umevaa, kama alikuwa juani madhali wewe ulikuwa kivulini. Aliusamehe usingizi wake kwa ajili yako. Alikulinda kwenye joto na baridi, vyote ili uweze kuwa ni wake yeye. Hutaweza kumuonyesha yeye shukurani, isipokuwa Mwenyezi Mungu akusaidie na upate mafanikio.” 16

Hadithi hiyo hapo juu inapaswa kuwapa wanawake wajawazito matumai- ni, ambao bila shaka yoyote watakabiliana na tatizo moja au jingine katika kipindi hiki.

Kwenye nyakati za shida, mtu lazima ajue kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaandalia wanawake vyote, uwezo na tamaa ya kuzaa na kulea watoto, kwani kama vile Imam as-Sadiq (a.s.) anavyosimulia: “Allah (s.w.t.). amempa kila mwanamke subira ya wanaume kumi, na wakati wa ujauzito Mwenyezi Mungu humpa uwezo wa wanaume kumi wengine zaidi.17

Wajibu Na Majukumu Katika Kipindi Cha Ujauzito

Kama kile kipindi cha kushika mimba, au hata zaidi ya hapo hasa, mawazo na vitendo vya mama vinakuwa na athari katika akhlaq, vitendo na imani ya yule mtoto ambaye hajazaliwa, kwa vile mtoto huyo ni kama kiungo cha mama huyo na anapata mambo yote muhimu ya maendeleo makuzi kutoka kwake.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ameeleza kwamba ustawi na upotovu wa mtoto unapangwa na kuamuliwa ndani ya tumbo la mama yake.” 18

Na katika riwaya nyingine, Imam Ali (a.s.) vilevile amesema kwamba kuhusiana na Akhlaq, desturi na ushikdini, mtoto anatengenezwa na mama yake na anachukua moyo kutokana na akhlaq yake (mama). 19

Hivyo ni wajibu wa mama kwamba anajenga mazingira bora kiasi iwezekanavyo kwa ajili ya nyumba ya awali ya mtoto.

Uangalifu wakati wote na mazingatio ya mama kwamba mawazo yote na vitendo vinakuwa

kwa mujibu wa mafundisho ya Uislam na Ahlul-Bayt (a.s.), ni muhimu sana na unasisitizwa sana.

Hili ni muhimu hasa kwa sababu mtoto sio wa familia tu, bali ni mwanajamii na anaweza kuwa chanzo cha neema na mafanikio. Kwani ni kupitia tabia hii ambapo watakatifu na wanazuoni mashuhuri wamekuja duniani humu na wakaacha athari, sio tu jamii zao, bali pia katika historia ya ulimwengu, inataja utakatifu au utakaso wa manabii watukufu wawili, Yahya ibn Zakariya (a.s.) na Isa ibn Maryam (a.s.) kuanzia siku ya kuzaliwa kwao:

وَسَلَامٌ عَلَيْهِ يَوْمَ وُلِدَ وَيَوْمَ يَمُوتُ وَيَوْمَ يُبْعَثُ حَيًّا {15}

"Na amani iko juu yake siku aliyozaliwa na siku atakayofariki, na siku atakayofufuliwa na kuwa hai." (Surat Maryam; 19:15)

وَالسَّلَامُ عَلَيَّ يَوْمَ وُلِدْتُ وَيَوْمَ أَمُوتُ وَيَوْمَ أُبْعَثُ حَيًّا {33}

"Na amani iko juu yangu siku ya niliyozaliwa na siku nitakayokufa, na siku nitakapofufuliwa kuwa hai." (Surat Maryam; 19:33).

Kadhalika ndani ya *Ziyaaratul-Waaritha*, tunashuhudia utakaso wa Imam Husein (a.s.): "Nashuhudia kwamba, kwa hakika wewe ulikuwa nuru katika viuno vitukufu, na matumbo yaliyotakasika; uchafu wa ujinga haukuwahi hata kukugusa, wala mwenendo wake wenye tope na uchafu haukuweza kukutia wewe madoa kamwe."

Baba anakuwa na wajibu mkubwa na muhimu katika kumsaidia mama kudumisha moyo mzuri na maendeleo kwa kumuunga mkono na kumsaidia kwa kila hali.

Kwa kufahamishwa na kuelewa kuhusu mabadiliko ambayo mama atakuja kuyapitia, na vile vile mahitaji yake ya kimwili, kihisia na kiakili, yeye baba anaweza kusaidia katika kuundwa kwa hali ya mazingira motomoto na ya upendo hapo nyumbani ambayo ni muhimu kwa malezi na makuzi ya uhakika ya mtoto.Kisa kifuatacho kinadokeza wazi umuhimu wa vitendo vya baba na mama wakati katika kipindi cha ujauzito.

a) Wakati Allamah Majlisi (mkusanyaji wa *Biharul-Anwaar*) alipokuwa bado mtoto mdogo, alikwenda na baba yake kwenye msikiti mmoja huko Isfahani. Muda baba yake alipokwenda kuswali, yeye aliendelea kubaki katika eneo la nje ya msikiti akicheza.

Wakati baba yake alipotoka msikitini, aliona kwamba mwanawe ametoboa kwa sindano mfuko wa ngozi ya maji uliokuwa umejaa maji tele ambao ulikuwa ni mali ya msikiti, na maji yote yalikuwa yamemwagika chini.

Baba yake akawa amefadhaika sana na wakati alipofika nyumbani kwake, alikisimulia kituko chote kwa mke wake na akasema kwamba kitendo hiki ni lazima kitakuwa ni matokeo ya mambo tuliyowahi kufanya.

Aliendelea kusema kwamba kwa kila namna alivyojaribu kufikiri juu ya vitendo vyake kabla

ya kutungwa kwa mimba hiyo, wakati wa kutunga mimba, vinywaji vya halali na kila aina ya uwezekano, hakuweza kupata jibu la uwezekano wa chanzo na akamuomba mkewe naye kufikiria juu ya hilo vile vile.

Baada ya kufanya hivyo, mke naye akajibu, ‘siwezi kufikiria juu ya jambo lolote lile isipokuwa kisa kimoja tu. Siku moja wakati nilipokuwa mjamzito wa mimba yake huyu, nilikwenda kwenye nyumba ya jirani na nikaona Mkomamanga. Nilitoboa kidogo na nikanyonya kiasi kidogo cha juisi kutoka humo.’ Kilikuwa ni hiki kitendo kidogo tu kilichokuja kusababisha kitendo cha baadaye ambacho kilitokea kwa mwanawe wa kiume huyo.20

Tunamuomba Mwenyezi Mungu awajaalie akina mama tawfiq (fursa tuku- fu adhimu) ili waweze kubeba majukumu na wajibu wao kwa kiasi cha uwezo wao wote, na hivyo waweze kutumia kwa vitendo hadithi ifuatayo ya Imam as-Sadiq (a.s.) kwa watoto wao: “Mwenye furaha ni yule ambaye mama yake anayo johari ya thamani adhimu ya utakaso au usafi na mawazo halisi.” 21

Vyakula Vinavyopendekezwa

Chakula cha kijusi (tumboni mwa mama) kinapatikana kutoka kwenye damu ya mama na kwa hiyo, kingi ya kile mama anachokula na kunywa hatimaye kwa namna moja au nyingine. Inasimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.): “Mwenyezi Mungu ameinasa damu katika tumbo la mama, ili kwamba iwe ni riziki au chakula cha mtoto.” 22

Imesimuliwa vilevile kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Chochote kile anachokula mama, kunywa au kuvuta wakati wa ujauzito, Mwenyezi Mungu pia anakigawa kwa mtoto.” 23

Kwa hiyo tena, kama katika ushikaji mimba, ni muhimu sana kwamba mama anakuwa muangalifu na chakula anachokula. Hususan kuhusu vinywaji haramu na vyakula haramu, imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba, “Athari ya mapato ya haramu zinatokeza dhahiri ndani ya kizazi cha mtu.”24

Katika riwaya nyingine imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.): “Dhambi zote ni mbaya, na dhambi iliyo mbaya zaidi kati ya zote ni ile ambayo damu na nyama vinakulia humo (vyakula vya haramu).”25

Inapendekezwa kutumia kula vyakula vifuatavyo katika kipindi cha ujauzito:

1. Kidari Cha Mnyama Wa Nyama:

a) Ina matokeo mazuri kwa mama mjamzito na inafanya mtoto atakayeza- liwa kuwa mzuri na

mwenye nguvu. 26

2. Chicory Aina Ya Majani Kwa Saladi

a) Ni nzuri kwa ajili ya uongezaji (wa ukubwa) wa mtoto.

b) Inaongeza majimaji yaliyo katika mzunguuko wa kiuno, yanamfanya mtoto kuwa mzuri na yanaongeza uume wa mtoto wa kiume.

c) Ni kisababisho cha uzuri wa mtoto.

d) Kuyala kwa wingi ni chanzo cha uongezekaji wa mali, na mtoto wa kiume. Chicory27 vilevile n

dawa nzuri kwa ajili ya ini.

3. Tende

a) Ni dhahiri kutokana na Ahadith kwamba chakula kilicho bora zaidi na dawa kwa mwanamke mjamzito ni tende.28

b) Imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.): “Hakuna chakula kilicho bora zaidi kwa mwanamke mjamzito kuliko tende mbivu**.**29

c) Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Kwa wanawake wajawazito, hususan wakati wanapojifungua, chakula kili- cho bora zaidi ni tende, kwa sababu Mwenyezi Mungu ameapia kwa umashuhuri na utukufu wake. Na iwapo wanawake watatumia kula *ratb* (aina fulani ya tende mbivu) katika masiku haya, watoto wao wanaozaliwa, iwe wa kiume au binti, watakuwa ni wavumilivu na wenye subira.” 30

d) Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Iwapo mwanamke atakula tunda tuhafa, mtoto wake atakuwa mzuri, na endapo atakula boga, kumbukumbu yao wote, mama na mtoto itaongezeka, na kula *ratb* (aina ya tende mbivu) na tende za kawaida kunatia nguvu mwili.”31

Kiangalizo: Imesimuliwa pia kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba mtu anapaswa kulinusa tuhafa kabla ya kulila. 32

e) Tende zinajulikana kama matunda ya Peponi na zilikuwa ndio matunda ya chaguo la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Na zimetajwa vilevile ndani ya Qur’ani tukufu. 33

Tende zina sifa kumi na tatu zenye umuhimu wa lazima, na aina tano za vitamini, zinazofanya ziwe chakula chenye rutuba nyingi. Madini ya chokaa (calcium) ndani ya tende ni muhimu sana kwa uimarishaji wa mifupa, na ile fosfati kwa ajili ya kuunda ubongo na kulinda udhaifu wa neva na uchovu, na patasiamu au magadi kwa ajili ya kuzuia vidonda na majeraha ya michubuko ndani ya tumbo.34

4. Tiini Tunda

4. Tiini 35 **Tunda**

a) Limetajwa na kutumiwa kuapia juu yake ndani ya Qur’ani Tukufu. 36

b) Ulile likiwa kavu, kwa vile hii inaongeza nguvu ya kujamiiana na inazuia bawasiri kikundu (*piles*).

c) Kula tiini kunazuia msokoto wa tumbo (*colic*).37

d) Imesimuliwa kutoka kwa Imam ar-Ridhaa (a.s.) kwamba tiini zinaon- doa harufu mbaya kutoka mdomoni, hufanya mifupa kuwa imara, zinasababisha nywele kukua, na zinazuia magonjwa.

e) Haipendekezwi kwa wale wenye ugonjwa wa kisukari, tumbo au mchafuko wa utumbo, au watu wenye uzito mkubwa. Kula kupita kiasi pia kunasababisha matatizo ya tumbo na

macho; hata hivyo, kula figili kunazimua athari hizi.38

Ubani Makka Na

5. Ubani Makka39 **Na** 40

a) Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba mtu ana- paswa kuwafanya wanawake wajawazito kula ubani Makka, kwani kwa kweli ubani Makka unapokuwa ni chakula kwa mtoto aliyeko tumboni, itaufanya moyo wake kuwa wenye nguvu na kuongeza akili maarifa yake.41

6. Mafuta Ya Zeituni

a) Mwanamke mwenye mimba asiache kunywa mafuta ya zaituni kwani yanafanya rangi yake kuwa angavu, na yanasafisha ini lake na la mtoto pia.42

7. Komamanga

7. Komamanga 258

a) Limependekezwa sana kuliwa kabla ya chakula cha kifungua kinywa asubuhi katika siku za Ijumaa.
b) Linamfanya mtoto kuwa mwema (mwadilifu).
c) Zuri sana kwa kutuliza kichefuchefu, kuzuia upungufu wa damu, homa ya nyongo ya manjano, maumivu ya viungo, shinikizo la damu na bawasiri. 43
d)Yeyote anayekula komamanga moja, moyo wake utajazwa *Nuur* na Shetani hatanong'ona kwao kwa muda wa siku arobaini.

8. Qawoot – Unga Wa Mchanganyiko Maalum

a) Kama italiwa na wazazi wote wawili, inakuwa ni chanzo cha nguvu na kukosa kuwa zuzu, akili dhaifu na hali ya ujinga juu ya mtoto.

b) Kumlisha mtoto kwa Qawoot kunasababisha kuongezeka kwa nguvu, ukuaji wa mnofu, na uimara
wa mifupa.

9. Tunda Jamii Ya Pera - Quince

a) Ni chanzo cha nguvu ya moyo, usafi wa tumbo, usafi dhahiri wa akili na ujasiri na uzuri wa mtoto.44

b) Linaleta mng'aro kwenye moyo, na kutibu maumivu ya ndani kabisa (kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu). 45

c) Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba wanawake wenye mimba wanapaswa kula tunda hili jamii ya pera, ili kwamba mtoto awe mwenye kunikia vizuri zaidi na rangi yake kuwa halisi zaidi.46

d) Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): "Fanyeni wanawake wenye mimba wale tunda hili jamii ya pera – *Quince*, kwani linawafanya watoto kuwa wazuri zaidi." 47

e) Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Kula *quince* – jamii ya pera

kunafanya rangi ya ngozi kuwa dhahiri zaidi na kuwa na usafi kamili, na kunamfanya mtoto wa mtu kuwa mzuri na mwenye afya njema vilevile.” 48

Quince – jamii ya pera lina vitamini B1, B2, B6 na C, magnesi na fosforasi.49

10. Tikiti Maji

a) Linamfanya mtoto kuwa mchangamfu na mwenye tabia njema kabisa.50

b) Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Hakuna mwanamke mwenye mimba anayekula tikitimaji pamoja na jibini isipokuwa kwamba mwanawe atakayezaliwa anakuwa mzuri na wa umbile zuri.” 51

11. Vitu Vingine Mbalimbali

a) Kula tunda la lozi, mchele wenye kapi, plamu nyeusi, samaki, dengu, kabichi, saladi, asali, maharage, zabibu, pichi, mafuta ya zeituni, mbegu za ***hazel***, karanga na mazao ya mifugo (hususan maziwa) pia vina manufaa sana katika kipindi cha ujauzito. 52

Tabia Za Baadhi Ya Vyakula Vilivyotajwa Hapo Juu

1. Hazel Nuts: Ni nzuri kwa kuzuia upungufu wa damu, mchango au msokoto wa tumbo (ingawa sio kwa zaidi sana). 53

2. Maharage meupe: Ni bora kwa watu ambao kazi zao zinahusiana na kufikiri zaidi.

3. Zabibu: Tunda lenye kalori nyingi. Linaondoa ulegevu, linasafisha damu na figo, na kuondoa tindikali ndani ya damu na kuleta nguvu.

4. Mapichi – *Peaches*: Yana madini ya chuma, Vitamini B na C, ni mazuri kwa ajili ya ini na yanaboresha rangi ya uso.54

5. Lozi: Linalainisha kifua, kutia nguvu kwenye kibovu na kuponya kuun- gua wakati wa kwenda haja ndogo. Lina fosforasi, potasiamu au magadi, magnesi, madini ya chokaa – kalisi, salfa na chuma. Mafuta ya lozi yana Vitamin E. 55

6. Mchele wa kapi: Punje za BRAN kama vile ngano, shayiri, mtama na mchele ni chanzo muhimu cha Vitamin B. Mchele bran ambao ngozi yake ya nje (ambayo lina vitamin) imeondolewa inasababisha baridi yabisi na jongo (*rheumatism* na *gout*), kuongezeka kushuka kwa nywele au nywele kupata mvi mapema. Wanawake wenye mimba hawashauriwi kula sana aina hii ya mchele, na kuula pamoja na kitunguu kibichi ili kufidia upungufu wa vitamini.

7. Plamu nyeusi: Plamu nyeusi na manjano zina vitamini A, B, na C, Potasiamu, sodiamu, magnesi oksidi, wanga, chuma, kalisi, fosforasi na magnesi. Ni mazuri kwa kutibia baridi yabisi na jongo (gout), kuziba kwa mishipa na kutia sumu kwenye chakula. Yanapoliwa wakati wa asubuhi kwenye tumbo tupu lenye njaa, yana manufaa kwa ajili ya kufunga choo.

8. Dengu: Ni nzuri kwa ajili ya upungufu wa damu na inaongeza maziwa.

Ina vitamin A, B na C, fosforasi, chuma na kalisi. Kuila kupita kiasi kunaweza kusababisha giza la macho na matatizo ya hedhi; hata hivyo, kula mafuta ya simsim na kuipika kwa majani ya kiazisukari kunaweza kutuliza athari hizi.

9. Kabichi: Lina vitamini A, B na C, na ni tiba kwa magonjwa yote. Ni zuri vilevile kwa tatizo la kukosa usingizi na uzito wa sikio (yaani mtu anapokuwa hasikii sawasawa). Linaongeza ukuaji wa mtoto na linaponya maumivu ya bawasiri (kutokwa na puru).

10. Saladi: Sehemu ya saladi iliyosindikwa ina madini ya chuma na magnesi. Ndani yake yenyewe, saladi ina madini ya shaba na ina manufaa kwa ini. Magnesi iliyomo humo ina manufaa kwa misuli, neva na ubongo. Inaongeza uzuiaji wa magonjwa ya kuambukiza.

11. Ua la Tanipu: Lina vitamini A, B, na C, fosforasi, madini ya chokaa, potasiamu, madini ya joto na salfa. Linaimarisha mwanga wa macho, na kwa sababu ya vitamini A, inatibia upovu wa usiku. Linalainisha kifua na kutibia vikohozi na mafua. Linazuia na kutibia ukoma mweusi. Ile salfa pamoja na Vitamin A vinazuia na kupunguza mawe kwenye kibovu. Linashusha shinikizo la damu na pia lina faida kwa ajili ya kuimarisha ovari na msisimko wa kingono.

Kwa sababu ya virutubisho vyake, maua ya tanipu (na shira na jamu yake) yanashauriwa kwa wanawake wenye mimba na wanaonyonyesha kwa ajili ya maendeleo ya mtoto, wepesi wa uotaji meno, uimarishaji wa mifupa, kutembea na kuongea kwa haraka na kinga dhidi ya magonjwa. (Shira: Weka tundu katikati ya ua la tanipu, lijaze sukari na ifanye iyayuke kuwa majimaji. Hii ni malham/kitulizo kizuri kwa ajili ya kifua na pia inaweza kulishwa watoto). 56

Kiangalizo: Hewa safi na oksijeni kwa wingi ni vitu muhimu sana kwa ajili ya maendeleo mtoto mwenye afya.

Vitendo Vinavyopendekezwa

Kwa ajili ya watoto wenye sifa njema na maumbo kamilifu, akina mama wanashauriwa kufanya kwa wingi zaidi ya vitendo vifuatavyo kiasi iwezekanavyo:

Vitendo Vya Kawaida

Vitendo Vya Kawaida57

1. Wakati wote jaribu kuwa katika hali ya wudhuu, hasa wakati wa kula chakula.

2. Wakati wote jaribu kuelekea Qibla wakati unapofanya matendo ya kila siku, hususan kula na kunywa.

3. Toa sadaka kila siku kwa ajili ya ulinzi wa mtoto.

4. Usijiangalie kwenye kioo wakati wa usiku.

5. Jihadhari na aina zote za dhambi, hususan kusengenya na uongo.

6. Tekeleza vitendo vyote vya wajibu na jaribu kufanya vitendo vingi mus- tahabu vilivyopendekezwa kwa kiasi kinachowezekana.

7. Jaribu kuwa umetulia na kuwa na mawazo yenye kusaidia wakati wote, na usiwe mwenye hasira.
8. Zuia mawazo ya wasiwasi wowote unaowezekana kuhusu makuzi na maendeleo ya mtoto au mimba kwa kupata taarifa zote muhimu, na zaidi ya yote hasa, kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu

9. Sikiliza, na soma Qur'ani kwa wingi iwezekanavyo, na hivyo kusaidia mtoto wako kuwa hafidh wa Qur'ani kuanzia akiwa tumboni.

10. Sikiliza hotuba kutoka kwa wanavyuoni.

11. Fanya josho la Ijumaa – *Sunnat Ghusli-Jumu'ah* – kwa Ijumaa 40 (tafadhali kumbuka kwamba mimba kwa kawaidi ni majuma 40. Kwa nyongeza, imesimuliwa katika hadith kwamba mtu anayechukua *Ghuslul-Jumu'ah* kwa wiki 40 mfululizo, mtu huyo hatakabiliwa na mbinyo wa kaburini).

12. Swali swala ya usiku *Salatul-Layl* mara 40 kwa kima cha chini kabisa.

Kama mtu hawezi kuamka kabla ya Swala ya al-Fajr na kuswali, basi inawezekana kuiswali baada ya Swala ya Isha.58 Kama hili pia hali- wezekani, inashauriwa kuswali Qadhaa.

13. Kula zabibu kubwa kwa siku arobaini kwenye tumbo tupu lenye njaa, kila siku vipande 21, kila kipande kuliwa baada ya kusoma Bismillah.

14. Mkumbuke Mwenyezi Mungu Mtukufu (sina dhikri ya Allah) wakati wote.

15. Saidia watu wengine katika matatizo yao.

16. Kuangalia nyuso za watu wachamungu na mandhari nzuri za kimaum- bile.

17. Usijichanganye na watu wenye tabia mbaya.

18. Nenda ukafanye Ziyaarat.

19. Tekeleza Swala zako kwa wakati wake uliopangwa.

20. Mpe mtoto jina akiwa tumboni, na chagua majina mazuri kama Muhammad, Ali, Fatimah na umuite kwa jina hili.

21. Zungumza na mtoto akiwa tumboni, kwani hili linaongeza ukaribu wa wazazi na mtoto huyo. Hili linabakia katika kumbukumbu ya mtoto, hata baada ya kuzaliwa. 59

Vitendo Maalum Kwa Ajili Ya Kila Mmojawa Miezi Ile 9 Ya Ujauzito.

Mwezi Wa 1:

Soma Surat Yaasin (36) na al-Saffaat (37) siku ya Alhamisi na Ijumaa na kasha pulizia kwenye tumbo.
Kula tufaha tamu wakati wa asubuhi
Kula komamanga kabla ya kifungua kinywa siku za Ijumaa.
Kula kiasi kidogo cha *Khakhe Shafaa*60 (kipimo cha mbegu ya dengu) kabla ya kuchomoza kwa jua.
Swali swala zako za kila siku katika nyakati fadhilah.
Soma Adhana/Iqamah kabla ya swala na mkono wako juu ya tumbo.
Soma Surat al-Qadr (97) ukiwa na tende mbili kila siku na kuzila ukiwa na tumbo tupu.

Mwezi Wa 2:

Soma Surat al-Mulk (67) siku ya Alhamisi na Ijumaa.

Soma *Swalawat* – Swala ya Mtume (pamoja na *Wa Ajjil Farajahum* ikiongezwa mwishoni) siku ya Alhamisi mara 140 na siku ya Ijumaa mara 100: ***"Allahumma swali 'alaa Muhammadin wa aali Muhammad, Wa Ajjil Farajahum."***

Soma Swalawat hii ndefu ifuatayo pamoja na mkono wako juu ya tumbo: ***"Allahumma swali 'alaa Muhammadin wa aali Muhammad, Wa Ajjil Farajahum wa ahlik 'aduwwahum minal-jinna wal-insi minal awwalina wal aakhirina."***

"Ewe Mola! Wape rehma na amani Muhammad na kizazi cha Muhammad, na harakisha kuondolewa kwao kutoka kwenye mateso, na waangamize maadui zao, na walaani maadui zao miongoni mwa majinni na watu kuanzia mwanzo hadi mwisho (wa wakati).61
Kula nyama na tuhafa tamu na kiasi cha maziwa kila wiki.
Soma Surat al-Tawhiid (112) juu ya jujube 2 (tunda la rangi nyekundu nzito; pia linajulikana kama tende ya Kichina) kila siku na uzile kwenye tumbo tupu.

Mwezi Wa 3:

Soma Surat Aali Imraan (3) katika siku za Alhamisi na Ijumaa. Soma Swalawat (pamoja na Wa Ajjil Farajahum) mara 140.

Soma ile Swalawat ndefu kabla ya kila swala ukiweka mkono juu ya tumbo: ***"Allahumma swali 'alaa Muhammadin wa aali Muhammad, Wa Ajjil Farajahum wa ahlik 'aduwwahum minal-jinni wal-insi minal awwalina wal aakhirina."***

"Ewe Mola! Wape rehma na amani Muhammad na kizazi cha Muhammad, na harakisha kuondolewa kwao kutoka kwenye mateso, na waangamize maadui zao, na walaani maadui zao miongoni mwa majinni na watu kuanzia mwanzo hadi mwisho (wa wakati)." 62

Kula ngano na nyama na kunywa maziwa kila wiki. Kunywa asali kila asubuhi.
Soma Ayat al-Kursi (Surat al-Baqarah; 2:255) juu ya tuhafa kila siku na kula tunda hili kwenye tumbo tupu. Kula kiasi kidogo sana cha Ubani Makkah (kipimo cha mbegu moja ya dengu) kwenye tumbo tupu.63

Mwezi Wa 4:

Soma Surat ad-Dahr/al-Insaan (76) mnamo siku Alhamisi na Ijumaa. Soma Surat al-Qadr (97) katika rakaa moja ya kila Swala yako.

Baada ya swala za kila siku, soma *Suratul-Kawthar* (108), *Suratul-Qadr* (97) na ile Swalawat ndefu pamoja na kuweka mkono juu ya tumbo: ***"Allahumma swali 'alaa Muhammadin wa aali Muhammad, Wa Ajjil Farajahum wa ahlik 'aduwwahum minal-jinna wal-insi minal awwalina wal aakhirina."***

"Ewe Mola! Wape rehma na amani Muhammad na kizazi cha Muhammad, na harakisha kuondolewa kwao kutoka kwenye mate- so, na waangamize maadui zao, na walaani maadui zao miongoni mwa majinni na watu kuanzia mwanzo hadi mwisho (wa wakati)."64

Soma:

رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَزْوَاجِنَا وَذُرِّيَّاتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ وَاجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِينَ

{74} إِمَامًا

“…..Mola wetu! Utupe katika wake zetu na watoto wetu yaburud- ishayo macho, na utujaalie kuwa viongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu.” (Al-Furqaan, 25:74).

Soma: *Astaghfirullaha Rabbi wa Atuubu Ilaik*. (Ninaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na natubia Kwako) mara saba (7).
Soma Swalawat mara 140 baada ya kumaliza Swala.
Kula tuhafa tamu, asali na komamanga.
Anza kuswali *Salatul-Layl* (kama huwezi hili kwa wakati wake, basi swali qadhaa).
Soma ***Suratut-Tiin*** (95) juu ya tiini mbili kila siku na uzile kwenye tumbo tupu.
Chagua jina la mtoto kabla haijatimia miezi 4 na siku 10 ya umri wa mimba.

Mwezi Wa 5:

Soma *Surat al-Fath* (48) katika siku za Alhamisi na Ijumaa.
Soma *Surat an-Nasr* (110) katika swala ya kila siku.
Sugua Khakhe Shafaa juu ya tumbo.
Kula tende moja kila siku asubuhi.
Kuanzia mwanzoni mwa mwezi wa tano, wakati wa Swala, anza kusoma Adhana na Iqama ukiwa na mkono wako juu ya tumbo.
Soma *Surat al-Hamd* (1) juu ya yai moja kila siku na ulile yai kwenye tumbo tupu lenye njaa.

Mwezi Wa 6:

Soma *Surat al-Waqiah* (56) siku za Alhamisi na Ijumaa.
Soma *Suratut-Tiin* (95) katika moja ya rakaa za Swala za Magharibi na Isha.
Paka Khakhe shafaa juu ya tumbo, baada ya kila swala.
Kula tiini na zeituni baada ya kifungua kinywa.
Imma wakati wa asubuhi au usiku, jaribu kula uboho wa mfupa,65 na jiweke mbali na vyakula vya mafuta.
Soma *Surat al-Fath* (48) juu ya komamanga kila siku na ulile wakati ukiwa na tumbo tupu.

Mwezi Wa 7:

Kuanzia kwenye mwezi wa 7, kwa siku 40 baada ya Swala ya al-Fajr soma *Surat al-An’aam* (6) juu ya malozi na kisha ule matunda hayo.
Kuanzia mwezi wa 7 na kuendelea, kula lozi moja kwa siku.
Soma *Surat al-Nahl* (16) siku ya Jumatatu.
Soma *Surat Yaasiin* (36) na *Surat al-Mulk* (67) siku za Alhamisi na Ijumaa.
Kuanzia mwezi huu na kuendelea, soma *Surat an-Nuur* (24) mara kwa mara.
Kuanzia mwezi huu na kuendelea, baada ya tasbihi, soma mara tano Sura hizi: *Surat al-Hadiid* (57), *Suratul-Hashr* (59), *Suratul-Saff* (61), *Suratul- Jumu’ah* (62) na *Suratut-Taghabun* (64) mara kwa mara.
Soma *Surat al-Qadr* (97) na *Surat at-Tawhiid* (112) katika Swala za kila siku.
Soma Swalawaat mara 140 kila siku.
Kula tikiti maji kiasi kidogo baada ya chakula (usinywe maji kabla au baada).
Soma *Surat Yaasiin* (36) juu ya quince (tunda aina ya pera) kila siku na ule tunda hilo

kwenye tumbo tupu.

Mwezi Wa 8:

Soma *Surat al-Qadr* (97) mara 10 katika siku za Jumamosi baada ya Swala ya al-Fajr.
Soma *Suratut-Tiin* (95) mara mbili katika siku za Jumapili baada ya swalat Subhi.
Soma *Surat-Yaasiin* (36) kwenye siku za Jumatatu.
Soma *Suratul-Furqaan* (25) siku ya Jumanne.
Soma Surat *ad-Dahr/al-Insaan* (76) kwenye siku ya Jumatano.
Soma *Surat-Muhammad* (47) mnamo siku ya Alhamisi.
Soma *Suratus-Saffaat* (37) siku ya Ijumaa.
Kula mtindi mtamu kwa asali.
Kula komamanga tamu kwenye siku ya Ijumaa ukiwa na tumbo tupu.
Kama hakuna hofu ya madhara, tumia siki (katika chakula chako) mara moja kwa wiki.

Mwezi Wa 9:

Usitumie kula *garam masala*.66
Chinja kondoo wa kafara kwa ajili ya Imam Mahdi (a.s.) na kisha kula kutoka humo kiasi.

Kula tende na kabaab. Kuhusu kula tende, imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Katika mwezi ambamo wanawake wajawazito hujifungua watoto, walisheni tende kwani watoto wao watakuwa wavumilivu na waadilifu.”67

Soma *Suratul-‘Asr* (103) na Suratu-Dhaariyaat (51) ndani ya swala za Dhuhuri na Al-‘Asr.
Soma *Surat al-Hajj* (22) kwenye siku ya Alhamisi na *Surat al-Faatir* (35) kwenye siku ya Ijumaa usiku.
Soma *Suratul-Insaan/al-Dahr* (76) juu ya kiasi fulani cha tende na maziwa kila siku na kula kwenye tumbo tupu.
Jaribu kujiepusha kuangalia picha na kujitazama kwenye kioo.
Fanya matembezi ya kila siku kwa hatua za taratibu.

Dua Na Maombi Yanayopendekezwa

Dua za kawaida katika kipindi chote cha ujauzito.68

1. Soma Surat Mariam (19) kila siku kwa ajili ya mtoto mwadilifu na mchamungu.

2. Soma Surat Yaasiin (36) mara 40 (kila mara moja ipulize kwenye koma- manga na kisha ulile tunda hilo)

3. Soma Surat Yusuf (12) mara arobaini (kila mara moja ipulize kwenye tuhafa na kisha ulile tunda hilo).

4. Soma Sura hizi: al-Hadid (57), al-Hashr (59), at-Taghabun (64), al- Jumu’ah (62), na as-Saff (61)
mara arobaini (40) kabla ya kulala siku ya Alhamisi usiku au usiku wowote ule.

5. Soma Surat at-Tawhiid (112) mara 50 kila siku baada ya swalat Subhi.

6. Soma Suratul-Qadr (97) mara 50 kila siku baada ya swala ya al-Fajr.

7. Soma Suratul-Anbiyaa (21) mfululizo (angalau mara moja kwa wiki) kwa ajili ya mtoto

mchamungu.

8. Kwa ajili ya mtoto mwenye subira, soma Surat al-‘Asr (103) ukiwa na mkono wako juu ya tumbo lako.

9. Soma *Ziyaarat al-Jam’iah* mara 40.

10. Soma *Ziyaarat Aale Yaasiin* (na ile Dua inayoifuatia) kwa mara 40.

11. Soma mara arobaini (40) *Ziyaarat ‘Ashuuraa* (pamoja na laana 100 na salaam na Dua Alqamah 100, kama laana hizo 100 na salaam hazi- wezekani, basi hata mara 10 itatosheleza.).

12. Soma *Ziyaarat al-Imaam al-Mahdii (a.s.)* mara 40.

13. Soma *Hadith al-Kisaa* mara 40.

14. Soma *Duaul-Tawassul* mara 40.

15. Soma *Duaa Kumail* siku ya Alhamisi usiku mara 40.

16. Soma *Dua an-Nudba* kwenye asubuhi ya siku ya Ijumaa (kabla ya Dhuhr) mara 40.

17. Soma *Dua as-Samaat* kwenye mchana wa siku ya Ijumaa mara 40.

18. Soma *Dua al-‘Ahd* mara 40 mfululizo baada ya Swalat al-Fajr.

19. Mswalie Bwana Mtume – *Swalawaat* 140 kwa siku.

20. Soma Istighfaar mara 70 baada ya swalaa.

21. Soma *Tasbih al-Hadhrat Fatimah (a.s.)* baada ya kila swala, na kila usiku kabla ya kulala.

22. Soma Qur’ani Tukufu yote mara moja (na uziwasilishe thawabu zake kwa Imam al-Mahdi a.s.).

23. Wakati wa kuhisi mtisiko wa mtoto, weka mkono wako juu ya tumbo na soma *Swalawaat* na Surat *al-Tawhiid* (112).

Kiangalizo: Ni muhimu kutambua kwamba kwa ajili ya zile Dua za kila wiki 40 zilizopendekezwa (kama vile Dua al-Kumail), kwamba kuna takriban wiki 40 katika ujauzito.

Dua Za Ki-Qur’ani Kwa Ajili Ya Watoto Wanyofu

1. Dua ya Nabii Ibrahim (a.s.):

رَبِّ هَبْ لِي مِنَ الصَّالِحِينَ {100

فَبَشَّرْنَاهُ بِغُلَامٍ حَلِيمٍ {101}

“Ewe Mola Wangu! Nipe (mtoto) miongoni mwa watendao wema. Ndipo tukampa habari njema ya mwana mpole.” (As-Saffaat; 37:100- 101)

2. Dua nyingine ya Nabii Ibrahim (a.s.):

رَبِّ اجْعَلْنِي مُقِيمَ الصَّلَاةِ وَمِنْ ذُرِّيَّتِي رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَاءِ {40}

“Mola Wangu! Nijaalie niwe msimamishaji swala na kizazi change (pia) Mola Wetu! Na uyapokee maombi yetu. (Al-Ibrahim; 14:40)

3. Dua ya Nabii Zakariya

رَبِّ هَبْ لِي مِنْ لَدُنْكَ ذُرِّيَّةً طَيِّبَةً إِنَّكَ سَمِيعُ الدُّعَاءِ {38}

“Pale pale Zakariya akamwomba Mola Wake, akasema: Mola Wangu! Umpe kutoka Kwako kizazi kizuri, hakika Wewe ndiye Mwenye kusikia maombi.” (Al-Imraan; 3:38)

4. Dua ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.):

وَأَصْلِحْ لِي فِي ذُرِّيَّتِي إِنِّي تُبْتُ إِلَيْكَ وَإِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ {15}

“….. Na unitengenezee watoto wangu, kwa hakika ninatubu Kwako na hakika mimi ni miongoni mwa walionyenyekea.” (Al-Ahqaf; 46:15)

6. Dua nyingine ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.):

رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَزْوَاجِنَا وَذُرِّيَّاتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ وَاجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا {74}

“….. Mola Wetu! Utupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho, na utujaalie kuwa viongozi kwa wamchao Mungu.” (Al- Furqaan 25:74)

Dua ya Imam Zainul-Abidiin kwa ajili ya watoto kama ilivyosimuliwa ndani ya *Sahifatul–Sajjadiya*, ni Dua inayoshauriwa sana kusomwa katika wakati wa ujauzito na baada ya hapo:

“**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehma. Mwenye kurehemu.”**

“Allahumma wa munna ‘alaiyya bibaqaai wuldiy wa bi-iswlaahihim liy wa bi imtaa‘i bihim.

“Ewe Mola! Kuwa na huruma juu yangu kupitia uhai wa watoto wangu, ukiwaongoza katika njia iliyonyooka kwa ajili yangu, na ukiniwezesha kuwafaidi!”

“Ilaahiy amdudliy fiy a’amaarihim, wa zidliy fiy aajaalihim, wa rabbi liy swaghiirahum, wa qawwi liy dhwa’iyfahum, wa aswihha liy abdaanahum wa adyaanahum wa akhlaaqahum, wa ‘afihim fiy anfusihim wa fiy jawaar- ihihim wa fiy kulli maa ‘uniytubihi min amrihim, wa adrir liy wa ‘alaa yadiy arzaaqahum. Waj’alhum abraaran atqiyaa buswaraaa sami’iyna mutwi’iyna laka, wa liawliyaaika muhiybiina munaaswihiyna, walijamiy’i a’adaaika mu’aanidiyna wa munghidhwiyna, aamiina.”

“Mola Wangu! Yafanye maisha yao kuwa marefu kwa ajili yangu, waongezee vipindi vyao, zidisha kilicho kidogo kwa ajili yangu, wape nguvu wanyonge kwa ajili yangu, warekebishie miili yao kwa ajili yangu, kujitolea kwao kidini, na akhlaq zao, wape afya katika nafsi zao, viungo vyao, na kila kitu ambacho **kinanihusu** mimi katika mambo yao, na uni- jaalie mimi na juu ya mikono yangu riziki yao! Wafanye wawe wanyofu, wenye kuhofia, wenye busara, wasikivu na watiifu Kwako, wenye mahaba na mwelekeo mwema kwa marafiki Zako, na wapinzani sana na wenye chuki kubwa kwa maadui Zako wote! Amiina!”

“Allahumma sh’dud bihim ‘adhwudiy, wa aqim bihim awadiy, wa kathir bihim ‘adadiy, wa zayyin bihim mahdhwariy, wa ahyi bihim dhikriy, waak- finiy bihim fiy ghaybatiy, wa a’inniy bihim ‘alaa haajatiy, waj’alhum liy muhibiyyna, wa ‘alaiyya hadibiyna muqbiliyna mustaqimiina liy, mutwiy’iyna, ghayra ‘aaswiyna wa laa ‘aaqqiyna wa laa mukhalifiyna wa laa khatwii’yna.

“Ewe Mungu, kupitia kwao niimarishie mkono wangu, ninyooshee mgon- go wangu uliolemewa na unizidishie idadi yangu, na uupambe uwepo wangu, na uhuishe kumbukumbu yangu, nitoshelezee kupitia kwao pale ninapokuwa sipo, na unisaidie katika haja zangu, na uwajaalie mahaba juu yangu na upendo, kuwaendea, waadilifu, watiifu, kamwe wasiofanya maasi, wasiokhalifu au wenye kufanya hatiauonevu!”

“Wa a’inniy ‘alaa tarbiyatihim wa ta-adiybihim, wa birrihim, wahabliy min ladunka ma’ahum aulaadan dhukuuran wa-j’al dhaalika khairaan liy, wa aj‘alhum liy ‘awnaan ‘alaa maa sa-altuka.”

“Nisaidie katika malezi yao, elimu yao, na utii wangu kwao, nijaalie mion- goni mwao kutoka Kwako mtoto wa kiume, na umfanye mwema kwangu, na uwafanye wao wawe msaada kwangu katika lile ninaloliomba kutoka Kwako!”

“wa a’izaniy wa dhuriyatiy min shaytwaani rajiymi, fainnaka khalaqtanaa wa amartanaa wa nahaytanaa waraghabtanaa fiy thawaabi maa amar- tanaa wa rahhabtanaa ‘iqaabahu, wa ja’alta lanaa ‘a duwaan yakiy- dunaa, sallatw’tahu minnaa ‘alaa maa lam tusallitw’naa ‘alayhi minhu, askantahu swuduuranaa, wa

ajraytahu majaariyaa, laa ya ghfulu in ghafalnaa, wa laa yansaa in nasiynaa, yu-uminunaa 'iqaabika, yukhawfu- naa bighayrika."

"Nipatie mimi na kizazi changu hifadhi kutokana na Shetan aliyelaaniwa, kwani Wewe umetuumba sisi, umetuamuru sisi, na umetukataza sisi, na umetufanya sisi tuwe na tamaa juu ya thawabu za yale uliyotuamrisha, na hofu juu adhabu yake! Umetujaalia sisi adui ambaye anapanga mipango dhidi yetu, ukampa mamlaka juu yetu, ukamruhusu kukaa ndani ya vifua vyetu na ukamfanya atembee ndani ya mishipa ya damu zetu, yeye hajali japo sisi tuzembee, yeye hasahau, ingawa sisi tunasahau; anatufanya sisi tujihisi tuko salama kutokana na adhabu Zako na anatujaza hofu kwa mwingine asiyekuwa Wewe!"

"In hamamnaa bi faahishatin shaja'aanaa 'alayhaa, wa in hamamnaa bi 'amali swaalihin thabatwanaa 'anhu, yata'aaradhu lanaa bilshshahawaati, wayanswibu lanaa bilsh-shubhaati,
in wa'aadanaa kadhabanaa, wa in mannanaa akhlafanaa, wa illa taswrif 'annaa kaydahu yud- hwilnaa,wa illa taqinaa khabblahu yastazilanaa."

"Kama tukikaribia kufanya maovu, yeye anatutia moyo kufanya hivyo, na kama tunataka kufanya amali njema, yeye anatuzuia kufanya hivyo. Anatupinga sisi kupitia hisia, na anatujengea mashaka na wasiwasi. Kama akituahidi sisi, anatudanganya, na endapo akinyanyua matumaini yetu, anashindwa kuyatimiza. Kama hutazigeuza hila zake juu yetu, yeye atatupotosha, na kama hutatulinda kutokana na udhalimu wake, atatufanya sisi tuteleze."

"Allahumma faaqhar sultanaahu 'annaa bisultaanika hattaa tahbisahu 'annaa bikathratid-du'aai laka fanuswbiha min kaydihi fiy al-ma'asuw miyna bika."

"Ewe Mungu, hivyo uyashinde mamlaka yake juu yetu kwa mamlaka Yako, kiasi kwamba unamrudisha nyuma kutoka kwetu kupitia wingi wa du'a zetu Kwako na sisi tunaziacha hila zake na kuamka miongoni mwa wale waliolindwa Nawe kutokana na dhambi!"

"Allahumma a'atwiniy kulla suwliy, wa-aqdhwi liy hawaaijiy, wa laa tamna'aniy l-ijaabata wa qad dhwamintahaa liy, wa laa tahjub du'aaiy 'anka wa qad amartaniy bihi, waamnun 'alayyaa bikulli maa yuslihuniy fiy dunyaaya wa aakhiratiy maa dhakartu minhu wa maa nasiytu,
aw adh-hartu aw akhfaytu aw a'alantu aw asrartu."

"Ewe Mungu, nijibu kila ombi, nijaalie juu yangu haja zangu, usizuilie kutoka kwangu majibu Yako unapokuwa umekadiria majibu, usiyawekee pazia maombi yangu kutoka Kwako, wakati Wewe ukiwa umeniamuru kuyafanya, na unineemeshe kupitia kila kitu ambacho kitaniweka sawa katika dunia hii na ile ijayo ya akhera, katika kila kitu ambacho ninakikum-buka au kukisahau, ninachokionyesha au kukificha, ninachofanya hadharani au ninachokifanya siri!"

"Wa-j'alniy fiy jami'yi dhaalika minal-muswalihiyn bi suwliy innaaka, al-munjihiyna bi-twalabi ilayka ghayril-mamnuw'iyna bi tawakkuli 'alaykal-mu'awwadhiyna bi tta'awwudhiyna bika, ar-raabihiyna fiy tijaarati 'alayka, mujaariyna bi'izzaka, muwassa'i 'alayhim ar-rizkul-halaalu min fad- hilika, al-waasi'i bijuwdika wa karamika, al-mu'azziyna minal-dh-dhula bika, wal-mujaariyna minadh-dhulmi bi'adlika, wal-mu'aafiyna minal- balaai bi-rahmatika, wal-mughniyna minal-faqri bighinaaka, wal-ma'a- suwmiyna minadh-dhunuwbi waz-zalali wal-khatwaai bitaqwaaka, wal- muwafiqiyna lilkhaiyri war-rushdi wa

swawaabi bitwa'atika, wa muhaali baynahum wa baynadh-dhunuwbi biqudratika, at-taarikiyna likulli ma'aswiyatika, saakiniyna fiy jiwaarika."

"Nijaalie (katika yote haya, kupitia maombi yangu) kuwa miongoni mwa wenye kuweka mambo sawa (swalihiin), wale wanaojibiwa vyema wanapoomba kutoka Kwako na ambao hawanyimwi wanapoweka mategemeo yao Kwako, wale ambao wenye mazoea ya kuomba hifadhi Kwako, wale wanaonufaika kwa biashara pamoja Nawe, wale waliopata kimbilio kwa nguvu Zako, wale ambao wanaopewa riziki halali kwa wingi kutoka Kwako, neema isiyo na mipaka kupitia upaji na ukarimu Wako, wale wanaofikia daraja ya juu baada ya unyonge, kupitia Kwako, wale wanaookoka na dhulma kwa uadilifu Wako, wale wanaondolewa kwenye mateso kwa rehma Zako, wale wanaookolewa kwenye dhiki baada ya umasikini kwa ukwasi Wako, wale waliokingwa na madhambi, kuteleza na mahatia kwa uchamungu wao na hofu juu Yako, wale waliofanikiwa katika wema, na wongofu na usahihi kupitia utii juu Yako na wale waliokingwa dhidi dhambi kwa uwezo Wako, wanaojizuia na kila tendo baya la kufru juu Yako, wale wakaazi wa jirani Yako."

"Allahumma a'atwinaa jamiy'a dhaalika bi-tawfiyqika wa rahmatika, wa a'idhnaa min 'adhaabis-sa'iyri, wa a'atwi jamiy'al-muslimiyna wal-mus- limaati wal-mu'minina wal-mu'minaati mithlal-ladhiy sa-altuka linafsiywa liwuldiy fiy 'aajilid-dun'yaa wa ajilil-aakhirati, innaka qariybun mujiybun samiy'un 'aliymun 'afuwun ghafuwrun raawfun rahiymun. Wa aatinaa fiy ad-dun'yaa hasanatan, wa fiyl-aakhirati hasanatan wa qinaa 'adhaaban-naari."

"Ewe Mungu, nipatie yote hayo kutokana na utoaji wako wa mafanikio na rehma Zako, tujaalie kinga kutokana na adhabu ya kuungua, na utupe Waislam wote, waume kwa wake, na waumini wote wanaume kwa wanawake, kama kile nilichoomba kwa ajili yangu na wanangu, katika ukaribu wa dunia hii na ya akhera! Hakika Wewe ni Mkaribu, Mwenye kujibu, Mwenye kusikia, Mjuzi wa yote, Mwenye kuridhia, Msamehevu, Mpole, Mwenye huruma! Na utupatie mema katika dunia hii, na mema katika akhera, na utukinge na adhabu ya Moto!"

1. Tafsiir Gaazar, Jz. 6, Uk. 235
2. Niyaazhaa wa Rawaabith Jinsii was Zanaashuii, Uk. 36
3. Biharul-Anwaar, Jz. 6, Uk. 334
4. http://allslam.org/masoom/writings/duas/arafah.html [16]
5. http://al-Islam.org/sahifa/dua32.html [17]
6. Biharul-Anwaar, Jz. 60, Uk. 362
7. Mustadrakul-Wasaail, Jz. 15, uk.180
8. Niyaazha wa Rawabith Maadaraa wa Janiin, Uk. 10
9. Al-Kafi, Juz. 2, Uk. 159-160
10. Mustadrakul-Wasaail, Jz. 2, Uk. 628
11. Makarimul-Akhlaq, Uk. 238
12. Bihaarul-Anwaar; Juz. 101, Uk. 108
13. al-Kafi, Jz. 5, uk. 496
14. Tafsiir Fi Dhilaalil-Qur'ani, Jz. 5, Uk. 318
15. Mustadrakul-Wasaa'il, Jz. 2, Uk. 628
16. Treatise of Rights, Sahifatus-Sajjadiyyah
17. Mustadrakul-Wasaa'il, Jz. 10, Uk . 46
18. Kanzul-A'maal, namba 490
19. Ghurarul-Hikm, hadithi ya 1862
20. Khaanwaade dar Islam, Uk. 161

21. Biharul-Anwaar, Jz. 23, Uk.79
22. Biharul-Anwaar, Jz. 60, Uk. 322
23. Biharul-Anwaar, Jz. 60, Uk. 322
24. al-Kafi, Jz. 5, uk.124
25. Niyaazhaa wa Rawaabith Maadaraan wa Janiin, Uk. 66
26. Tabib Khaanwaade, Uk. 66
27. Rayhaan-e Beheshti, Uk. 107
28. Tafsiir Nur al-Thaqalayn, Jz. 3, Uk. 330
29. Tuhaf ul-'Uquul, Uk. 83
30. Al-Kafi, Jz. 6, uk. 24
31. Halliyatul-Muttaqiin, Uk. 1125
32. Wasa'ilush-Shi'ah, Jz. 25, Uk. 160, hadithi ya 31521
33. Surat al-Anaam; 6:99, Surat Mariam; 19:25
34. Izdawaaj Maktab Insaan Saazi, Jz. 7, Uk. 65
35. Rayhaan-e Beheshti, Uk. 108-109
36. Suratut-Tiin; 95:1
37. Gonjhaay-e Ma'navii, Uk. 347
38. Khaas Mivehaa Wa Sabziihaa.
39. Huu ni ulimbo mkavu au gundi ambao unapati kana kwa mapana huko Makka, na pia unajulikana kama Libaan kwa Kiarabu
40. Huu haupendekezwi kwa wale wanaoishi kwenye maeneo makavu ya chumvi chumvi (majangwani)
41. Halliyatul-Muttaqiin, Uk. 126
42. A'jaaz khuuraakiihaa, Uk. 308 - 311
43. Masaail 'Ilmi Dar Qur'an, Uk. 140
44. Al-Kafi, Jz. 6, Uk. 357
45. Gonjhaay-e Ma'navii, Uk. 350
46. Halliyatal Muttaqiin, Uk. 125
47. ?
48. Biharul-Anwar, Jz. 81, uk. 101
49. Rayhaan-e Beheshti, Uk. 106
50. Bargeye Rahnama
51. Biharul-Anwar, Jz. 62, Uk. 299
52. Rayhaan-e Beheshti, Uk. 109-112
53. Khaas Miveha Wa Sabziihaa
54. A'jaaz Khoraakiihaa
55. Khaas Miveha Wa Sabziihaa
56. Khaas Miveha Wa Sabziihaa
57. Zaidi vinapatikana kutoka Rayhaaney-e Beheshti, uk. 103 - 106
58. Imethibitishwa na ofisi ya Ayatullah Sistaanii, Qum.
59. Fasalnaameye Shir Maadar, namba 9.
60. Udongo wa ardhi tukufu ya Karbala, Iraqi.
61. Biharul-Anwar, Jz. 86, Uk. 289
62. Biharul-Anwar, Jz. 86, Uk. 289
63. Hili halishauriwi kwa wale wanaishi kwenye nchi kame na zenye chumvichumvi (majangwa).
64. Biharul-Anwar, Jz. 86, Uk. 289
65. Pia unajulikana kama 'bongo' kwa ki-Gujarati
66. Mchanganyiko fulani wa viungo wenye asili ya India
67. Mustadrak al-Wasaa'il, Jz. 3, Uk. 112
68. Nyingi zinapatikana kutoka kwenye Rayhaaney-e Beheshti, Uk. 103-106

Mlango Wa 7: Kujifungua

Matendo Yanayoshauriwa

Matendo Yanayoshauriwa[1]

1. Soma Suratul-Inshiqaq baada ya swala katika mwezi wa tisa (9). Wakati uchungu wa uzazi unapoanza, isome hii, na kama itakuwa haiwezekani kuisoma kwa ulimi wako, basi isome kichwani mwako.

2. Kunywa shira (syrup) ya zafarani wakati wa uchungu wa uzazi ili kupunguza maumivu (isije ikawa kabla ya hapo, kwani hili linaweza kusababisha kuporomoka kwa mimba).

3. Kwa wakati mwanamke anapodhani kwamba uchungu wa uzazi utaan- za, jimwagie maji ya vuguvugu (sio ya moto).

4. Wakati wa uchungu wa uzazi, kuwa na vitu vinavyonukia vizuri karibu yako na uvute hewa huku ukiwa umefungua mdomo wako.

5. Usile kiasi kikubwa cha chakula, bali kula chakula kizuri na chakula chenye nguvu nyingi, na ujiepushe na vyakula vinavyosababisha kufunga choo.

6. Soma zile Dua zilizopendekezwa kwa ajili ya kujifungua.[2]

7. Ibn Abbas amesimulia kwamba kuandika majina ya As'hab al-Kahf (Watu wa Pango) na kuyafunga majina haya kuzunguka paja la kushoto la mwanamke anayepitia kipindi kigumu cha uchungu wa uzazi kunapendekezwa sana. [3]

8. Usivae nguo za nailoni, kwani hizi zinazuia mionzi ya jua kuufikia mwili, na kwa hiyo, kusababisha ukosefu wa vitamin B na uzaaji mgumu zaidi.

9. Moja ya sababu za hali ya ugumu wa uchungu wa uzazi kwa wanawake wengi ni woga na hofu kwa ajili ya ukosefu wa maandalizi. Kwa hiyo, inashauriwa kwamba ujiandae kabla kwa ajili ya ile hali ya uchungu wa uzazi (leba), kiakili na kimwili. Kusoma na kuwa na ufahamu wa kile kitakachotokea kunasaidia sana katika kupunguza woga.

10. Mazoezi yanayopendekezwa vilevile kunasaidia katika kupunguza maumivu ya wakati wa kuzaa (leba). [4]

1. Rayhaaneye Beheshti, uk. 120- 123
2. Tafadhali rejea kitabu, 'A Mother's Prayer' cha Saleem Bhimji na Arifa Hudda
3. Tafsiir Minhaaj al-Sadiqiin, Jz. 5, Uk. 334
4. Rejea kwa daktari wako au vitabu vya mwongozo kwa ajili ya taarifa zaidi.

Mlango Wa 8: Baada Ya Kujifungua

Vyakula Vinavyopendekezwa

1. Tende Safi

1. Tende Safi 1

a) Imesimuliwa kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: “Kitu cha kwanza mwanamke anachopaswa kula baada ya kujifungua kiwe ni *ratb* (aina ya tende freshi), kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu alimwambia Hadhrat Maryam baada ya kumzaa Nabii Isa ale *ratb*.” 2

Alipoulizwa, “Je kama sio msimu wa ratb iweje?” Yeye akajibu akasema: “Basi ale tende tisa kutoka Madina, na kama hizo nazo hazi patikani, basi tende zozote tisa zitatosha. Hakika Mwenyezi Mungu amesema: “Naapa kwa Heshima na Utukufu Wangu, kwamba mwanamke yeyote ambaye amezaa hivi punde na akala *ratb*, nitamfanya mwanawe kuwa mwenye subira.’”

b) Imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.) kwamba lisha tende aina ya Birmi kwa mwanamke baada ya kuzaa mtoto wake ili kwamba mtoto huyo awe jasiri na mwenye subira.

c) Kula tende sio tu kwamba kuna manufaa kwa mama huyo bali kuna athari kwenye maziwa ya kifuani vilevile, na pia ni kwenye manufaa zinapolishwa watoto.3 Kwa vichanga vinavyoanza kuzaliwa, imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.) kwamba weka kajipande kadogo katika kinywa cha kitoto hicho, na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alifanya hivyo kwa Imam Hasan na Imam Husein (a.s.).

2. Maji Ya Mto Furati Na Khakhe Shafaa

2. Maji Ya Mto Furati Na Khakhe Shafaa4 **(Juu Ya Kipaa Cha Mdomo Wa Mtoto)**

a. Imesimuliwa kwamba maji ya Furati na khakhe shafaa yawekwe kwenye mdomo wa mtoto, na kama maji ya mto Furati hayapatikani, basi maji ya mvua badala yake.5Na6

b. Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba khakhe shafaa inapaswa kuwekwa kwenye kinywa cha mtoto, kwani hii inamkinga na maumivu na majonzi.7

c. Katika riwaya nyingine kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.), inasimuliwa kwamba yeye amesema: “Hakuna mtu ambaye anakunywa maji ya mto Furati na akayaweka kwenye mdomo wa mtoto isipokuwa kwamba yeye ni rafiki yetu, kwa sababu Furati ndio mto wa mu’min.8

3. Nyingineyo

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba wakati mtoto anapozaliwa, chukua kiasi cha maziwa kutoka kwa mama yake (kipimo cha mbegu ya adesi), yachanganye na maji na uweke matone mawili katika tundu ya pua ya kulia ya mtoto huyo, na kisha ya kushoto, na usome Adhana katika sikio lake la kulia na Iqaamah katika sikio lake la kushoto, kabla hawajakata kiunga mwana kutoka kitovuni mwake. Kama hili likifanyika, hofu haitamfika mtoto huyo kamwe na Umm Sabyaan (jinni subiani) hatamsumbua kamwe. 9

Matendo Yanayoshauriwa

1. Ukubalikanaji Wa Mtoto, Awe Wa Kiume Au Wa Kike

Kwa bahati mbaya, hata leo hii, wengi bado wanayo ile kasumba kwamba watoto wa kike hawafai na kuwashughulikia watoto wa kiume na wa kike kwa tofauti. Ambapo, iko wazi kabisa ndani ya Qur'ani Tukufu kwamba mtoto ni kiumbe cha Mwenyezi Mungu Mtukufu na Yeye anajaalia mtoto wa kiume kwa yeyote amtakaye na mtoto wa kike kwa amtakaye. 10

Inasimuliwa kwamba wakati pale Imam Zainul-Abidiin (a.s) alipobashiriwa habari njema za kuzaliwa kwa mwanawe, yeye hakuuliza iwapo kama alikuwa wa kiume au wa kike, bali hasa kwanza aliuliza, maumbile (umbo) yake yako sawasawa?

Kisha alipoambiwa kwamba mtoto huyo alikuwa mwenye afya njema na hakukuwa na dosari yoyote katika maumbile yake, yeye alisoma haya: ***"Alhamdulillahi al-ladhiy lam yakhluq miniy shaiyaan mushawwahaan"***

"Sifa zote ni za Mwenyezi Mungu ambaya hakuumba kutoka kwangu kitu chenye umbo lisilo sawa."11

Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Ni jambo la neema kwa mwanamke kwamba mtoto wake wa kwanza awe ni wa kike."12

Imesimuliwa kwamba mabinti ni wema na neema na vijana ni fadhila. Mtu ataulizwa kuhusu fadhila alizopewa, ambapo wema na neema vitaongezwa.13

2. Kusoma Adhana Na Iqaamah

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ameeleza kwamba yeyote ambaye atazaliwa mtoto, anapaswa kumsomea Adhana kwenye sikio lake la kulia na Iqaamah kwenye sikio la kushoto, kwani hili ni ulinzi kutokana na uovu wa Shetani.14

Kwa kuongezea, katika simulizi nyingine imeelezwa kwamba mkunga au mtu mwingine lazima aambiwe amsomee Iqaamah katika sikio la kulia ili jinni asije akamsumbua mtoto, wala asije akawa mwendawazimu. 15

Imesimuliwa vilevile kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alithibitisha kwamba zilisomwa Adhana na Iqaamah kwenye masikio ya Imam Hasan (a.s.) na Imam Husein (a.s.), na pia Suratul-Fatiha, Ayatul-Kursi, mwisho wa Suratul-Hashir, Suratul-Ikhlaas, Suratul-Falaq, na Suratun-Naas.16

3. Nguo Za Mtoto

Kutoka kwenye hadithi wakati wa kuzaliwa Imam Hasan (a.s.) na Imam Husein (a.s.), ni dhahiri kwamba ni makuruhu kumfunga mtoto kwenye nguo ya manjano mara tu baada ya kuzaliwa; bali inapendekezwa kumfunika kwenye nguo nyeupe.17

4. Josho (Ghusl)

Imeelezwa katika kitabu Fiqh al-Ridhaa kwamba moja ya mambo yanay- opendeza (mustahab) lililosisitizwa sana (wengine wanadiriki hata kuliita la wajibu) baada tu ya kuzaliwa kwa mtoto ni kumpatia mtoto huyo Ghusl. Mtu lazima aweke nia kwamba ninampa mtoto huyu ghusl kwa ajili ya radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu na halafu kwanza aoshe

kichwa chake, kisha upande wa kulia na halafu upande wa kushoto.18

Hata hivyo, inapasa ifahamike kwamba hili linapaswa kufanyika tu iwapo lina usalama kiafya na sio lenye madhara kwa mtoto huyo.

5. Kunyoa Nywele

5. Kunyoa Nywele 19

Hii inahusisha unyoaji wa nywele zote za mtoto (anayetoka tumboni) mara tu baada ya kuzaliwa, na kutoa dhahabu au fedha kulingana na uzito wa nywele hizo kama sadaqah. Halafu nywele hizo zizikwe ardhini. Inapendekezwa kulifanya hili katika siku ya saba baada ya kuzaliwa mtoto.

Nywele ni lazima zinyolewe zote kabisa bila kuacha kishungi au shole (sokoto) la nywele kwenye paji.Imesimuliwa kwamba mtoto mwenye kishungi aliletwa karibu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.); kisha Mtume hakumswalia mtoto huyo na akasema kwamba kishungi chake kinyolewe kiondoke.
Inashauriwa kwamba baada ya kunyolewa kwa nywele hizo, inapaswa akandwe kwa zafarani kichwani mwake. Ukandaji wa damu ya aqiqah hata hivyo unakataliwa kwa nguvu kabisa na umeitwa ni kitendo cha kijahilia.

6. ‘Aqiqah Na

6. *‘Aqiqah* 20 **Na** 21

Hii inahusisha uchinjaji wa mnyama kwa jina la mtoto kwa ajili ya ulinzi wake. Aqiqah ni sunna iliyokokotezwa sana kwa yeyote yule mwenye uwezo (baadhi wamediriki hata kuiita ni wajibu), na ni bora kama itafanyi- ka katika siku ya saba baada ya kuzaliwa mtoto.22

Kiangalizo: Inashauriwa kwamba huo unyoaji wa nywele, utoaji wa dhahabu/fedha kama sadaka na Aqiqah vifanyike kwenye sehemu moja hiyohiyo na kwa wakati mmoja, ingawaje ni sunna kwamba unyoaji wa nywele ndio ufanyike mwanzo.

Kiangalizo: Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba Aqiqah sio sawa sawa na kafara (*qurbaanii*)

7. Utahiriwaji Wa Wavulana

7. Utahiriwaji Wa Wavulana23

Kutahiri ni wajibu juu ya wavulana, na pamoja na kunyoa na Aqiqah, inapendekezwa kwamba yafanyike yote katika siku ya saba baada ya kuzaliwa kwa mtoto, ingawaje hili likifanyika kabla ya hapo hakuna madhara.24

Kama haikufanyika wakati huo, ni sunna kwamba ifanyike hadi wakati wa balehe ya mtoto huyo, ambapo baada ya hapo ni wajibu juu ya kijana huyo mwenyewe kuifanya. Hata hivyo, wanavyuoni wengine wameeleza kwamba pale mtoto anapokaribia kubalehe, ni wajibu juu ya mlezi kumfanyia. Hasa imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.) kwamba mtu anayekuwa muislam anapaswa kutahiriwa, hata kama ana umri wa miaka 80.

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba watoto wanapaswa kutahiriwa kwani kunafanya mwili kuwa msafi zaidi, kunafanya nyama za mwili kukua haraka, na ardhi

inachukia sana mkojo wa mtu asiyetahiriwa.

Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba ardhi inakuwa najisi kwa siku arobaini kutokana na mkojo wa mtu asiyetahiri- wa, na katika riwaya nyingine, imesimuliwa kwamba ardhi inatoa mkoromo wa huzuni kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa sababu ya mkojo wake mtu asiyetahiriwa.

Imesimuliwa vilevile kwamba endapo utamtahiri kijana, na ile ngozi ya kifuniko ikakua tena na kufunika dhakari, mtahiri tena, kwa sababu ardhi inalalamika kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa muda wa siku arobaini kwa sababu ya kufunikwa kule kutahiriwa kwake.

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Mtu yeyote ambaye hajatahiriwa asiongoze swala, na ushahidi wake haukubaliki, na endapo atafariki (katika hali hiyo) basi msimswalie kwa vile ameacha sunna kubwa sana ya Mtukufu Mtume, isipokuwa kama ameiacha kwa hofu ya kifo ambacho kingetokana na kutahiriwa kwake.” Inashauriwa kusoma du’a ifuatayo wakati wa kutahiri:25

“Ewe Mungu! Hakika (hili tunalofanya) limo katika njia ya Sunnah Yako na Sunnah ya Mtume Wako (s.a.w.w.) kukutii Wewe na dini Yako na kutimiza amri Yako, nia na kutekeleza sheria ambazo umeamua kuzifanya zifuatwe bila masharti. Kwa hiyo umempa muonjo wa joto la chuma kupitia kutahiriwa kwake na kufikwa na jambo ambalo kwa hakika Wewe unalijua vizuri zaidi kuliko mimi. Ewe Allah! basi mtakase na dhambi zake; umuongezee umri; na umuondolee kutoka mwilini mwake magonjwa ya mlipuko na maumivu; na uongeze utajiri wake; na umlinde kutokana na umasikini; kwani kwa hakika Wewe unajua zaidi na sisi hatujui kitu.”

8. Karamu (Walimah)

Hii inahusisha kuwalisha waumini juu ya kuzaliwa mtoto na kwa ajili ya kutahiriwa kwa mtoto huyo (hizi zinaweza kukusanywa na kufanywa kwa pamoja wakati mmoja).
Inashauriwa kuwakaribisha ndugu na marafiki mnamo siku ya saba baada ya kuzaliwa kwa mtoto (au karibu na siku hiyo) kushiriki katika tukio adhimu la kuzaliwa kwa kichanga hicho.
Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Sherehe na karamu katika siku ya kwanza ni wajibu, kwenye siku ya pili ni vizuri, na kwenye siku ya tatu hiyo ni riyaa (yaani, ni kwa ajili ya watu wengine na sio kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu).” 26
Ni makuruhu kwa waalikwa wote kuwa ni matajiri, bali mchanganyiko wa matajiri na masikini sio tatizo.
Ni mustahab pia kwamba waalikwa waitikie huo mwaliko wa kwenye walimah huo

9. Kutoga (Kutoboa) Masikio

Kutoga masikio ya mtoto huyo ni jambo linalopendekezwa.27

10. Kugusana Kwa Mama Na Mtoto Na Kunyonyesha Na

10. Kugusana Kwa Mama Na Mtoto Na Kunyonyesha28 Na29

Moja ya vitendo bora baada ya kuzaa ni kuogesha mtoto huyo na kisha kumrudisha karibu na ngazo ya mama yake na kuwafunika na blanketi. Nusu saa baada ya kuzaliwa, mtoto anakuwa anatambua kabisa na mchangamfu, na ndio wakati muafaka wa kujizoesha kunyonya na mguso wa mama yake.

Zile siku chache za mwanzo maziwa hayatengenezwi kwa wingi; hata hivyo, kiasi kile kinachotoka kinatosha, kinafaa na muhimu kwa mtoto aliyezaliwa punde. Ni muhimu sana kwamba kuchoka kwa mama na kukosa maziwa (kwa wingi) kusije kukatumiwa kama ni sababu ya kumlisha mtoto kwa chupa kwa hili linasababisha kucheweza kutengeneza maziwa kutoka kwa mama na mtoto kutokuwa na uwezo wa kunyonya sawa sawa. Vile vile kunaongeza uwezekano wa maambukizi kwa mtoto.

Aqiqah - Mtazamo wa karibu zaidi

Aqiqah - Mtazamo wa karibu zaidi 30

Umuhimu Wa Kufanya Aqiqah

Imesimuliwa kwamba maisha ya mtoto yameambatishwa na Aqiqah**,**31 na endapo kama haikufanyika, inamuanika mtu kwenye taabu na kifo. Kama ikicheleweshwa, ni sunnah juu ya baba mpaka kubalekhe kwa mtoto, na baada ya balehe, inakuwa ni sunnah juu ya mtoto mwenyewe.32

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba Aqiqah ni muhimu kwa mtu yeyote tajiri, na kama mtu ni masikini, anapaswa kufanya Aqiqah mara tu anapopata pesa, na kama hatapata pesa yoyote, basi ni sawa tu. Endapo mtu hakufanya Aqiqah, na akawa alifanya kafara (*qurbaani*), hii itatosha.

Imesimuliwa kwamba mtu mmoja alimuuliza Imam as-Sadiq (a.s.): “Tumeomba kondoo kwa ajili ya Aqiqah lakini hatuwezi kupata hata mmoja, je, unashauri nini? Je, tunaweza kutoa thamani ya kondoo huyo kama sadaka badala yake?” Imam alijibu akasema: “Hapana, ombeni mpaka mpate mmoja kwani Mwenyezi Mungu anapenda ulishaji wa wengine …”

Umar ibn Yazid anasimulia kwamba yeye alimuuliza Imam as-Sadiq (a.s.): “Mimi sijui kama baba yangu alinifanyia Aqiqah au hapana.” Imam akajibu akasema: “Itekeleze wewe,” na hivyo akafanya Aqiqah katika umri wa utu uzima wake.

Katika riwaya nyingine imesimuliwa kwamba mtu mmoja alimuuliza Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba endapo mtoto atafariki katika siku ya saba, je, Aqiqah bado inapaswa kufanyika? Imam akajibu kwamba ikiwa mtoto atafariki kabla ya swala ya Adhuhuri, Aqiqah inakuwa sio lazima, bali endapo mtoto huyo atafariki baada ya Adhuhuri, basi itekeleze Aqiqah.

Ni Nini Kinachopasa Kichinjwe

Ni kawaida miongoni mwa ulamaa kwamba Aqiqah iwe ni kondoo, ngamia au mbuzi, na kwamba Aqiqah kwa ajili ya mvulana inapaswa iwe mnyama dume na Aqiqah kwa ajili ya msichana iwe mnyama jike.

Kama ni ngamia, anapaswa awe na umri wa miaka mitano. Kama ni mbuzi inapaswa awe na umri wa mwaka mmoja zaidi ya huo, kama ni kondoo, anapaswa awe angalau na umri miezi sita au zaidi na ni bora kama mwezi wa saba utakuwa umetimia.

Korodani zake zisikatwe na pia ni bora kama hazitapondwa vile vile. Pembe zake zisivunjwe (kiasi kwamba akatoa damu) na masikio yake yasikatwe. Asiwe mwembamba aliyekonda sana, wala asiwe kipofu, wala asiwe kilema sana kiasi kwamba kutembea kunakuwa ni kugumu juu yake.

Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba, kama ilivyosimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.), Aqiqah sio sawa na kafara (qurbaani) ambayo ina shuruti kali kwa ajili ya mnyama anayetolewa kafara.

Kwa hiyo, kama haiwezekani kutekeleza shuruti hizo hapo juu, kondoo yoyote yule ni sawa, ingawa aliyenenepa ni bora zaidi.

Dua Wakati Wa Aqiqah

Wakati33 wa kumchinja mnyama kwa ajili ya Aqiqah, du'a zifuatazo zinapasa kusomwa:

1. Mwishoni mwa du'a hii, mtu lazima ataje jina lake na jina la baba yake [kwa mfano, kama jina la baba ni Taahir na jina la baba yake ni Abdullah utasema, Taahir ibn (mwana wa) Abdullah] Dua hii inaanza na Aya za 78 na 79 za Suratul-An'am zikufuatiwa na Aya za 162 na 163 za Suratul-An'am hiyo hiyo:

"Enyi watu wangu! mimi simo katika hayo mnayoyashirikisha (na Allah). Mimi nimeuelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba mbingu na ardhi, hali ya kuwa nimewacha dini za upotovu, mimi si miongoni mwa washirikina. Hakika swala yangu na ibada zangu na uzima wangu na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola wa ulimwengu wote. Hana mshirika, na hayo ndiyo niliyoamrishwa, na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu). Ewe Allah! kwa hakika mnyama huyu anatoka Kwako na anarudi Kwako kwa Jina la Allah na Yeye Allah ni Mkubwa kuliko maelezo yoyote yanayoweza kutajwa juu Yake. Ewe Allah! shusha rehma na amani juu ya Muhammad na kizazi chake Muhammad na ikubali hii kutoka kwa (jina lako na jina la baba yako)."

2. Dua ifuatayo pia lazima isomwe wakati mnyama anapokuwa anachinjwa (mtoto huyo akiwa ni mvulana ama msichana).

"Kwa jina la Allah, na kwake Allah, na sifa zote ni zake Mwenyezi Mungu pekee, na Allah ni Mkubwa kuliko maelezo yoyote yanayoweza kuelezwa juu Yake. Kwa imani kamili kwake Allah na mapenzi kwa Mtume wa Allah (s.a.w.w.) na wana shukurani juu ya riziki ya Allah (s.w.t.). na kinga iliyotolewa kwa amri ya Allah na utambuzi kamili na mazingatio juu ya neema Zake juu yetu sisi Ahlil-Bayt."

Kama mtoto ni mvulana, basi du'a ifuatayo pia inapaswa isomwe:

"Ewe Mungu! Umetuzawadia sisi mtoto mwanaume na Wewe unajua vizuri zaidi ni nini ulichotuzawadia sisi, na kurejea Kwako ni kile tuna- chokifanya sisi - hivyo basi ridhia kutoka (kafara) hili kutoka kwetu juu ya mila (sunnah) Yako na sunnah ya Mtume Wako, (rehma na amani juu yake na juu ya kizazi chake) na utuweke mbali na Shetani aliyelaaniwa. Kwa ajili Yako damu (ya mnyama huyu) imemwagwa, na Wewe huna mshirika na sifa zote njema ni Allah pekee, Mola wa ulimwengu wote."

3. Dua ifuatayo pia ni lazima isomwe katika wakati wa kumchinja mnya- ma. Pale mtu atakapofikia mabano ya pembe, atataja jina la mtoto huyo na lile la baba yake [kwa mfano, kama jina la mtoto ni Jabir na jina la baba ni Kumayl, basi utasema: Jabir ibn Kumayl] na kisha uendelee na sehemu ya du'a iliyobakia. Maelezo ya kwanza ya du'a hii ni kwa sababa ya mtoto mvulana, du'a ya pili ni iwapo kama mtoto ni wa kike.

“Kwa jina la Allah na kwa Allah, Aqiqah hii (uchinjaji wa mnyama) ni kwa ajili ya [Jina la mtoto na jina la kwanza la baba yake]. Nyama yake badala ya nyama ya mtoto; damu yake badala ya damu yake mtoto; mifupa yake badala ya mifupa ya mtoto vyote vinatolewa Kwako. Ee Allah! ikubali hii kwa ajili kile ambacho kwacho mtoto huyu atakingwa na kuhifadhiwa, kwa jina la kizazi cha Muhammad, rehma na amani ya Allah iwe juu yake na juu ya kizazi chake.

“Kwa jina la Allah na kwa Allah, Aqiqah hii (uchinjaji wa mnyama) ni kwa ajili ya [Jina la mtoto na jina la kwanza la baba yake]. Nyama yake badala ya nyama ya mtoto; damu yake badala ya damu yake mtoto; mifupa yake badala ya mifupa ya mtoto vyote vinatolewa Kwako. Ee Allah! ikubali hii kwa ajili kile ambacho kwacho mtoto huyu atakingwa na kuhifadhiwa, kwa jina la kizazi cha Muhammad, rehma na amani ya Allah iwe juu yake na juu ya kizazi chake.”

Jinsi Gani Itakavyogawanywa?

Inashauriwa kwamba mifupa hiyo isije ikavunjwa; bali inapaswa kuten- ganishwa kwenye maungio yake. Ni bora vile vile kwamba nyama hiyo igawanywe ikiwa imepikwa (kwa angalau na maji na chumvi tu) na ngozi yake kutolewa kama sadaka.

Inapendekezwa kwamba miguu na mapaja ya aqiqah (hii inaweza kuh- esabiwa kama moja ya tatu au moja ya nne ya kondoo huyo kutegemeana na namna ya ugawaji) lazima itolewe kwa mkunga (au daktari) yule aliye- saidia wakati wa kujifungua na iliyobakia itolewe kwa watu iliwe kama sadaka. Ikiwa mkunga au daktari huyo ni Myahudi, basi thamani ya robo ya kondoo huyo lazima itolewe (kumpa yeye badala ya nyama).

Kama mtoto huyo alizaliwa bila ya mkunga au daktari, basi inapasa kutole- wa kwa mama ambaye anaweza kuigawa kwa yeyote anayemtaka yeye; ni lazima yeye aitoe kwa waislamu angalau kumi hivi, na kama anaweza kuigawa kwa wengi zaidi ni bora. Sio lazima kwamba nyama hiyo itolewe kwa masikini tu; hata hivyo, ni bora zaidi kwamba inatolewa kwa wachamungu na masikini.

Inashauriwa kwamba huyo baba na mama (na wale ambao wanawatege- mea wao, kama vile watoto wao na wazazi) wao hawali kutoka kwenye nyama iliyopikwa ya Aqiqah, na hii imesisitizwa hasa kwa mama.

Namna Inayopendekezwa Ya Kumpongeza Mtu Wakati Wa Kuzaliwa Kwa Mtoto

Inasimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba alimpongeza mtu mmoja kwa mtoto ambaye Mwenyezi Mungu alikuwa amembariki naye kwa namna ifuatayo (kumekuwa na simulizi nyingi za namna hiyo kutoka kwa Imam Hasan (a.s.) vilevile): 34

“Mwenyezi Mungu akuruzuku na shukurani juu ya alichokujaalia, na akibariki kile alichokujaalia nacho, na amfanye afikie umri wa balekhe, na akujaalie na uadilifu wake mtoto huyu.”35

Kumpatia Mtoto Jina

Umuhimu Wa Kumpa Mtoto Jina

Imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Kadhim (a.s.) kwamba wema wa kwanza ambao baba

anaweza kuufanya kwa ajili ya mwanawe ni kumpatia jina36 zuri.

Ni haki ya mtoto kwamba wazazi wake wampatie jina zuri na kumtunza na kumtendea wema.37 Katika riwaya nyingine, imesimuliwa kwamba miongoni mwa haki za mtoto ni pamoja na jina bora, kumfundisha kuandika na kumuozesha wakati anapofikia umri wa utu uzima (balekhe).38

Wakati Gani Wa Kumpa Mtoto Jina

Inasimuliwa kutoka wa Imam Ali (a.s.): “Mtoto anapaswa kupewa jina wakati akiwa bado yuko tumboni, na kama hakupewa jina na mimba ikaporomoka, katika Siku ya Kiyama atakuja kumuuliza baba yake, “Kwa nini hukunipatia jina?” Mtukufu Mtume alimpatia jina Muhsin, mtoto wa Hadhrat Fatimah wakati akiwa yuko tumboni, na Muhsin huyu ni yule mtoto ambaye, baada ya kufariki kwa Mtukufu Mtume, yeye alikuwa bado yuko tumboni wakati Umar alipomfanya kuwa (afe) Shahidi.”

Imesimuliwa kutoka kwa Maimam (a.s.) kwamba: “Mtoto wa kiume haz- aliwi kwetu sisi, Ahlul-Bayt, isipokuwa kwamba anaitwa Muhammad kwa siku saba, na halafu kama ikihitajika, jina hilo linaweza kubadilishwa au kuondolewa.”39

Imeelezwa ndani ya Fiqh al-Ridhaa kwamba weka jina (yaani, tangaza jina hilo kwa wengine) mnamo siku ya saba.

Majina Yanayopendekezwa

Kumwita mtoto kwa majina ya Ahlul-Bayt (a.s.) ni tangazo la wazi la mapenzi na urafiki kwao, na dini sio chochote bali ni mapenzi na urafiki wa Ahlul-Bayt (a.s.) kama Allah (s.w.t.). anavyoelezea ndani ya Qur’ani Tukufu, katika ile Surat al-Imraan; 3:31:

إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ {31}

“Sema: Ikiwa ninyi mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni mimi Mwenyezi Mungu atawapenda ……” (Al-Imraan; 3:31).

Imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.) kwamba majina yanayofaa zaidi kwa ajili ya mtoto ni yale ambayo yanaashiria utumwa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kama vile Abdullah (mtumwa wa Allah), na majina bora zaidi kwa mtoto ni yale ya Mitume.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema kwamba yeyote aliye na watoto wanne na akawa hajamuita yoyote kati yao kwa jina langu, huyo amenionea mimi.40

Inasimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Katika nyumba ambamo majina ya baadhi ya watu wake ni yale ya mitume (a.s.), neema za nyumba hiyo hazitatoweka kamwe.41

Katika riwaya nyingine, imesimuliwa kutoka kwa Imam al-Kadhim (a.s.) kwamba umasikini na ufukara kamwe havitaingia kwenye nyumba ambamo jina la Muhammad, au Ahmad, au Ali, au Hasan, au Husein, au Ja’far, au Talib, au Abdullah, au Fatimah linapatikana.42

Imesimuliwa kutoka kwa Imam Husein (a.s.); “Kama ningekuwa na watoto mia moja, ningependelea kuwaita wote kwa jina la Ali.”43

Imesimuliwa kwamba mtu mmoja alikwenda kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akauliza: “Ametujia (amezaliwa) mtoto wa kiume kwetu, je nimuite jina gani?” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alijibu akasema: “Muite yeye jina bora kabisa katika majina niliyonayo mimi, nalo ni Hamza.”

Imesimuliwa kutoka kwa Jabir ambaye amesema: Nilikwenda kwenye nyumba ya mtu mmoja nikiwa pamoja na Imam al-Baqir na mtoto mmoja akatoka nje yake. Imam akamuuliza: “Unaitwa nani?” Yeye akajibu akase- ma. “Ninaitwa Muhammad.” Imam akamuuliza: “Ni lipi jina la cheo (kuniyah) chako?” Yeye akajibu: “Ni Abu Ali.” Imam akasema; “Wewe umejitoa kwenye ngome ya Shetani. Kwa kweli, kila wakati Shetani anapomsikia mtu akiitwa Ya Muhammad! au Ya Ali! anatoweka zake na wakati anaposikia mtu akiitwa kwa jina la maadui zetu, yeye anafurahia na anajifaharisha katika hilo.”

Katika hadithi nyingine, inasimuliwa kwamba mtu mmoja alikuja kwake Imam as-Sadiq (a.s.) na akasema kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa amemjaalia mtoto mwanaume, Imam akampongeza, na akasema, “Wewe umempatia jina gani? Yeye akajibu, “Nimemwita Muhammad.” Imam akageuzia kichwa chake kuangalia chini ardhini na akawa anaendelea kurudia jina hilo Muhammad mpaka uso wake karibu uguse ardhi.

Kisha akasema, “Maisha yangu, watoto wangu, wake zangu, baba yangu, mama yangu na watu wote wa dunia hii watolewe kafara kwa ajili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kwa sababu umempa jina lililobarikiwa kiasi hicho, basi usije ukamtukana na usiwe unampiga na usimkaribie kwa ubaya. Na ulijue hili kwamba hakuna nyumba ambamo hili jana la Muhammad linapatikana bali kwamba kila siku nyumba hiyo inafanywa kuwa tukufu na safi halisi.”

Katika riwaya nyingine inasimuliwa kwamba mtu anapaswa kumheshimu binti ambaye jina lake ni Fatimah na asiwe anamtukana yeye na kamwe asimpige.”

Majina ya kivyeo ya Hadhrat Fatimah (a.s.) yanaweza kutumika kwa maji- na ya mabinti:

Mubaraka: Aliyebarikiwa.
Tahira: Aliyetakasika.
Zakiyya: Mwenye hekima.
Radhiya: Aliyetosheka.
Mardhiyya: Aliyeridhiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu
Siddiqah: Aliye mkweli.
Muhaddathah: Ambaye Malaika wanazungumza naye.
Muhaddithah: Anayesimulia hadithi za Mtume (s.a.w.w.).
Zahrah: Mwenye nuru.

Majina Ambayo Hayapendekezwi Kutumika

Katika riwaya kadhaa imesimuliwa kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amekataza kumwita mtoto kwa majina yafuatayo: Haakim, Hakim, Khalid na Maalik.

Na amesema kwamba majina mabaya sana kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Harith, Maalik na Khalid. Na pale jina linapokuwa ni Muhammad, amekataza vyeo (kuniyah) vinne: Abu Isa, Abul Hakim, Abu Malik na Abul-Qasim, kwani vyote, majina na vyeo havikubaliki kwa Mtume (s.a.w.w.).

Katika riwaya moja, imesimuliwa kwamba mtu anapaswa kutomwita mtoto Yaasiin, kwani

hilo ni makhususia kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pekee.

1. Halliyatul Muttaqin, Uk. 125-127
2. Surat Maryam, 19:25
3. Israar Khuuraakiihaa, Uk . 96
4. Udongo mtakatifu wa Karbala, Iraqi.
5. Hii inashauriwa tu kwenye maeneo ambapo mtu ana hakika kwamba maji ya mvua hayakuchafuliwa
6. Al-Kafi, Jz. 6, Uk. 24 hadithi ya 4
7. Halliyatul Muttaqiin, Uk. 145-146
8. Biharul-Anwaar, Jz. 104, Uk. 114, hadithi ya 33
9. Halliyatul Muttaqiin, Uk. 126
10. Surat al-Shuraa (42:49)
11. al-Kafi, Jz. 6, Uk. 21
12. Biharul-Anwaar, Jz. 104, Uk. 98, hadithi ya 64
13. al-Kafi, Jz. 6, Uk. 6, hadithi ya 8
14. al-Kafi, Jz. 6, Uk. 24, hadithi ya 6
15. Halliyatul Muttaqiin, Uk. 126
16. Biharul-Anwaar, Jz. 104, Uk. 126, hadithi ya 86
17. Halliyatul Muttaqiin, Uk. 146
18. Halliyatul Muttaqiin, Uk. 130
19. Halliyatul Muttaqiin, Uk. 132
20. Halliyatul Muttaqiin, Uk. 120 - 133
21. Aqiqah itakuja kuelezewa kwa kirefu chini ya - Aqiqah: Uchunguzi makini katika mlango huu
22. Mustadrakul-Wasa’il, Jz. 15, Uk. 145, hadithi ya 17807
23. Halliyatul Muttaqiin, Uk. 134-135
24. Halliyatul Muttaqiin, Uk. 134
25. Kitabu, ‘A Mother’s Prayer’
26. Wasa’ilush-Shi’ah, Jz. 16, Uk. 455
27. Wasa’ilush-Shi’ah, Jz. 16, Uk. 134
28. Rayhaaney-e Behesht, Uk. 167
29. Hili limeelezwa kwa kina zaidi katika Mlango wa 9: Kunyonyesha
30. Hilliyatul-Muttaqin, Uk. 130 - 133
31. al-Kafi, Jz. 6, uk. 25, hadithi ya 3
32. Hilliyatul-Muttaqin, Uk. 150
33. Kitabu, ‘A Mother’s Prayer’
34. Hilliyatul-Muttaqin, Uk. 127
35. al-Kafi, Jz. 6, Uk. 17
36. Hilliyatul-Muttaqin, Uk. 128-130
37. Mustadrakul-Wasa’il, Jz. 15, Uk.128, hadithi ya 17748
38. Mustadrakul-Wasa’il, Jz. 15, Uk.166, hadithi ya 17876
39. al-Kafi, Jz. 6, Uk. 18, hadithi ya 4
40. Tahdhib al-Balaghah, Jz. 7, Uk. 438, hadithi ya 11
41. Mustadrakul-Wasa’il, Jz. 15, 129, hadithi ya 17751
42. al-Kafi, Jz. 6, Uk. 19, hadithi ya 8
43. al-Kafi, Jz. 6, Uk. 19, hadithi ya 7

Mlango Wa 9: Kunyonyesha

Chakula Kwa Ajili Ya Mtoto Aliyezaliwa Punde

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka chakula na maji kwa ajili ya mtoto katika mwili wa mama, na ameumba mfumo wa kushangaza wa kumlisha kichanga aliyezaliwa punde kwa njia ambayo ni kamilifu na yenye manufaa sana.

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Ewe mama wa Is’haaq, usimlishe mtoto kutoka kwenye titi moja tu, bali umlishe kutoka kwenye matiti yote mawili, kwani moja ni badala ya chakula na jingine ni badala ya maji.” 1

Katika riwaya nyingine, imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Allah (s.w.t.). ameweka riziki ya mtoto katika matiti mawili ya mama yake, ndani ya moja ni maji yake na katika jingine ni chakula chake.” 2

Kwa vile sasa tuko kwenye mas’ala ya ulishaji wa mtoto aliyezaliwa punde moja kwa moja kutoka kwa mama yake, ni lazima tena hapa kutaja na kusisitiza umuhimu wa kipato cha halali, ulipaji wa Khums na Zaka, matu- mizi ya chakula safi na halali kwa mama na athari zake kwa mtoto. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameeleza umuhimu wa kula chakula halali na kizuri mara nyingi ndani ya Qur’ani Tukufu3 na hadithi zimesisitiza wazi kwamba kukosa kulishikilia hili ni moja ya sababu za chanzo cha tabia (*akhlaq*) mbaya, ushari na uonevu. Vile vile imeelezwa kama ni chanzo cha kukosa utiifu kulikotolewa kwa Imam Husein (a.s.) kutoka kwa maadui zake na hivyo yakatokea masaibu ya Karbala.

Kufungamana na matokeo ya kula chakula haramu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesimulia: “Kila wakati tonge la chakula cha haramu linapoingia ndani ya tumbo la mtu, malaika wote wa mbingu na ardhi hutupa laana juu yake, na mpaka wakati ambapo lile tonge haramu limo ndani ya tumbo lake, Mwenyezi Mungu haangalii upande wake aliko. Kila mtu ambaye anakula tonge la chakula haramu anajikusanyia sababu za ghadhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu Halafu, iwapo akatubia, Mwenyezi Mungu huipokea toba yake na endapo atafariki dunia bila ya kutubia, basi anastahili moto wa Jahannam.4

Mifano Mitatu

Ili kuweza kusisitiza hayo hapo juu, na kadhalika baadhi ya njia zilizopendekezwa za unyonyeshaji na matokeo yake, mifano mitatu ya maisha ya maulamaa wetu imetajwa hapa chini:

1. Ilisemwa kwa mama yake Sheikh Ansaarii, mmoja wa Ulamaa wa Shi’ah wa kuheshimika: “Mashaallahu, mtoto mzuri kiasi gani uliyemleta kwenye jamii!” Huyo mama akajibu: “Nilikuwa na matumaini makubwa juu ya mwana wangu, kwa sababu nilimnyonyesha kwa miaka miwili na kamwe sikuwa bila ya Wudhuu. Wakati mwanangu alipolia katikati ya usiku na akataka maziwa, mimi niliamka, nikachukua Wudhuu, kisha ndipo nikamnyonyesha mwanangu.”5

2. Aliulizwa pia mama yake Muqaddas Ardabiili kwamba, ni nini chanzo cha hadhi ya hali ya juu ya mwanao? Yeye akajibu akisema: “Mimi sikuwahi kamwe kula kipande cha chakula chenye wasiwasi, na kabla ya kumpa mwanangu maziwa yangu kwanza nilichukua Wudhuu. Kamwe sikumtazama mtu ambaye sio maharim wangu (ambaye kuoana naye

kunaruhusiwa), na baada ya kumuachicha kwake kunyonya, nilichunga usafi na utakaso na kumfanya akae na kucheza na watoto wema.”6

3. Haj Sheikh Fadhkullah Nuuri, Mujitahidi anayeenziwa ambaye alinyongwa wakati wa uhai wake, alikuwa na kijana ambaye alikuwa ni aina ya mtu ambaye alijaribu kufanya baba yake anyongwe. Mmoja wa wanavyuoni mashuhuri anasimulia: Nilikwenda kukutana na marehemu Nuuri huko gerezani na nikamuuliza. “Huyu mtoto wako angepaswa kuwa mtoto wa mtu muungwana, na mrithi wako bora. Kwa nini yeye ni duni kiasi hicho kwamba anakuzungumzia vibaya na hata anadiriki kufurahia kuuliwa kwako?”

Marhum Nuuri alijibu: “Ndio, mimi nililijua hili na nilikuwa na hofu hiyo.” Kisha aliendelea akasema: “Mtoto huyu alizaliwa huko Najaf. Alipokuja kwenye ulimwengu huu, mama yake aliugua na hakuweza kum- nyonyesha maziwa yake. Tulilazimika kupata mama mnyonyeshaji wa kuajiriwa ili ampatie maziwa. Baada ya muda kitambo wa kunyonyesha, tuligundua kwamba mwanamke huyu ni dhalim (si mwenye tabia njema), na juu ya hayo, ni adui wa Imam Ali (a.s.) na Ahlul-Bayt wote (a.s.). Kwa wakati ule, kengele za tahadhari zilianza kulia kwa ajili yangu.”

Wakati wa kunyongwa kwa baba huyu, mtoto wake alisimama na kushangilia pamoja na wajinga wengine, na yeye pia hatimaye alitoa mtoto kwenye jamii ambaye si mwingine zaidi ya Nuuruddin Kianuri, kiongozi wa *Hizb-e Tude* (Chama cha Kikomunisti cha Irani);7 huyu ni mtoto wa kiume wa mtu yule yule aliyepiga makofi kushangilia wakati wa kuny- ongwa baba yake.8

Thawabu Za Kunyonyesha

Kuna hadithi nyingi sana zinazosimulia thawabu za kunyonyesha, kama zile ambazo zimesimuliwa katika sehemu ya Umuhimu wa Umama katika Mlango wa tano, ambapo mama anayenyonyesha amefananishwa na mtu anayepigana katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na endapo anafariki katika wakati huu, anapata thawabu za Shahidi.

Umuhimu Wa Maziwa Ya Kifuani

Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Kwa ajili ya mtoto, hakuna maziwa bora zaidi kuliko maziwa ya mama yake.”9 Mtume vile vile amesema kwamba hakuna kinachoweza kuchukua nafasi mbadala ya chakula na maji isipokuwa maziwa.10 Kadhalika, imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.) kwamba hakuna maziwa yenye baraka zaidi kwa mtoto kuliko yale maziwa ya mama.11

Kunyonyesha sio kumlisha mtoto tu, bali pia ni kubadilishana mapenzi na uimarishaji wa moyo. Wakati mtoto anaponyonya, anaweza kusikia sauti ya moyo wa mama yake na hili linasababisha uburudikaji na utulivu. Watoto walionyonyeshwa huelekea kuwa na afya zaidi na timamu zaidi katika masuala ya afya ya kimwili na kiroho na wanasaikolojia wanaamini kwamba kunyonyesha kunawaweka watoto wenye furaha na kuridhika na pia kuna athari katika Akhlaq zao.

Kunyonyeshwa ni moja ya haki za mtoto na pia inahesabiwa kama ni haki ya mama, na imekokotezwa sana ndani ya Qur’ani na hadithi. Kwa kweli, manufaa yake yanakubalika sana katika ulimwengu wa leo. Kwa hakika, inapasa kuzingatiwa akilini kwamba kunyonyesha kunashauriwa tu endapo kama hakutaleta hatari yoyote kwa mama au mtoto.

Faida Za Maziwa Ya Kifuani

Faida Za Maziwa Ya Kifuani 12

1. Maziwa ya kifuani yana virutubisho vyote muhimu ambavyo mtoto anavihitaji ndani ya miezi 4 – 6 ya mwanzo ya maisha.

2. Maziwa ya kifuani yanazo protini na mafuta yanayofaa kuridhisha mahitaji ya kawaida ya mtoto.

3. Kuna kiasi kikubwa cha laktosi katika maziwa ya kifuani kuliko kwenye aina nyingine za maziwa, kwani hii ndio inayohitajiwa na mtoto.

4. Kuna vitamini za kutosha ndani ya maziwa ya kifuani, zinazohakikisha kwamba hakuna vitamini za ziada ama maji ya matunda yanayohitajika.

5. Madini ya chuma ndani ya maziwa ya kifuani yanatosha kwa ajili ya mtoto. Hata kama viwango vikiwa sio vya juu sana, uwezo wa mtoto wa kunyonya kile kiasi cha lazima ni mzuri sana.

6. Maziwa ya kifuani yana maji ya kutosha kwa ajili ya mtoto, hata kama mtu anaishi katika tabia ya nchi iliyo kavu.

7. Maziwa ya kifuani yana chumvi ya kutosha, kalisi na fosfati kwa ajili ya mtoto.

8. Maziwa ya kifuani yana kimeng’enya kiitwacho *lipase* kinachomeng’enya mafuta.

9. Mtoto aliyenyonyeshwa sio mwepesi wa kuambukizwa kutokana na kinga iliyoongezeka.

10. Maziwa ya kifuani ndio kinga muhimu dhidi ya sababu mbili kuu za vifo miongoni mwa watoto: magonjwa ya kuhara na maambukizi kwa njia ya hewa.

11. Kunyonyeshwa kunapunguza magonjwa yanayotokana na mizio (aleji) kama vile pumu, ukurutu na kadhalika, na kunasaidia kukinga au kupunguza baadhi ya magonjwa wakati mtoto anapokuwa kwenye umri wa kijana na kuendelea juu zaidi.

12. Kisukari na baadhi ya matatizo ya mmeng’enyo yanakuwa machache kwa watoto walionyonyeshwa.

13. Kunyonyesha kunasaidia watoto wagonjwa kupona haraka zaidi; kwa hiyo ni muhimu sana kwamba kusisimamishwe katika wakati huu.

14. Maziwa ya kifuani ni rahisi na haraka kumeng’enya, kwa hiyo, watoto walionyonyeshwa wanaelekea kushikwa na njaa haraka kuliko watoto walionyonyeshwa maziwa ya aina nyingine.

15. Maziwa ya kifuani wakati wote yako tayari na hayana haja ya mata- yarisho yoyote.

16. Maziwa ya kifuani hayaharibiki kamwe na wala hayawi chachu, hata kama mtoto atakuwa hajanyonya kwa muda wa siku kadhaa chache.

17. Unyonyeshaji wa kawaida, na kunyonyesha wakati mtoto anapohitajia kunazuia ushikaji wa mimba.

18. Mawasiliano ya kawaida kati ya mama na mtoto katika siku za mwan- zoni za maisha yake kunaongeza fungamano la kiroho na la kimwili baina ya wawili hao, kuelekezea kwenye uhusiano mzito na wa upendo na mafunzo na malezi bora ya mtoto huyo.

19. Maziwa ya kifuani hayahitaji gharama yoyote ile.

20. Watoto walionyonyeshwa wanakuwa na umahiri wa uoni, uzungumzaji na utembeaji haraka sana.

21. Kule kunyonya kwa mtoto mara tu baada ya kuzaliwa kunasababisha muamsho wa oksitosini ambako kunaishia katika mnyweo wa tumbo la uzazi, na hivyo kupunguza utokaji wa damu kwa mama huyo.

22. Akina mama wanaonyonyesha wana uwezekano mdogo wa kupata saratani ya matiti au ya tumbo la uzazi.

23. Wanawake wanaonyonyesha wanarejea haraka sana kwenye miili yao ya wakati wa kabla hawajapata mimba kwa vile mafuta yao ya uzazi yanatumika haraka.

24. Maziwa ya kifuani ya mama hubadilika kulingana na mahitaji ya kila siku ya mtoto. Kuna tofauti vile vile kati ya akina mama kutegemeana na mahitaji ya watoto wao, kwa mfano, maziwa ya mama wa mtoto ambaye hajatimiza kipindi (cha ndani ya mimba – kabichi) na maziwa ya mama wa mtoto wa kipindi kamili aliyetimia.

25. Watoto walionyonyeshwa wana maarifa zaidi hata wanapokuwa wachanga kabisa (yaani, zile wiki nne za mwanzo za uhai wao). Utafiti umeonyesha kwamba watoto hawa wanacheza zaidi katika zile wiki mbili za mwanzo na waonyesha mishughuliko mingi kuliko watoto wengineo.

26. Watu wazima ambao waliwahi kunyonyeshwa huelekea kuwa madhubuti zaidi na wepesi kwa tabia.

Kipindi Cha Muda Uliopendekezwa Kwa Kunyonyesha

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Suratul-Baqarah, Aya ya 233 kama ifuatavyo:

وَالْوَالِدَاتُ يُرْضِعْنَ أَوْلادَهُنَّ حَوْلَيْنِ كَامِلَيْنِ لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يُتِمَّ الرَّضَاعَةَ {233}

"Na wanawake waliozaa wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kamili kwa anayetaka kukamilisha kunyonyesha ……" (Al- Baqarah; 2:233).

Na katika Surat al-Ahqaf, Aya ya 15, Mwenyezi Mungu anasema:

وَحَمْلُهُ وَفِصَالُهُ ثَلاثُونَ شَهْرًا {15}

"….. Na kumbeba na kumwachisha ziwa ni miezi thelathini …." (Al-Ahqaf; 46:15)

Kama ilivyoonyeshwa katika Aya hizo hapo juu, muda ulioshauriwa katika Uislam kwa ajili ya kunyonyesha ni takriban miaka miwili. Ni dhahiri vilevile kutoka kwenye hadithi kwamba muda wa kunyonya wa Imam Husein (a.s.) pia ulikuwa miezi ishirini na nne.[13]

Ahlul-Bayt (a.s.) wanayo mapendekezo kadhaa juu ya kipindi cha kunyonyesha. Katika baadhi ya hadithi, imesimuliwa kwamba kunyonyesha kwa muda chini ya miezi 21 kunahesabiwa kama ni uonevu na shari dhidi ya mtoto.14 Ndani ya riwaya nyinginezo, kunyonyesha kwa muda wa miezi 21 kunaonekana kama ni muhimu na ni lazima.15 Kadhalika, imesimuliwa katika hadithi kwamba kunyonyesha kwa zaidi ya miaka miwili pia kumekatazwa.16

Vitendo Vinavyoshauriwa

1. Mama anapaswa kuwa na uchamungu, na awe mwangalifu kwamba maziwa yasije yakachafuka kutokana na kukosa uchamungu na maadili. Hususan katika kipindi cha kunyonyesha, mtu anapaswa kujitenga na aina zote za dhambi. Matendo mema na ukaribu na Allah yana matokeo na athari njema kwa mtoto.

2. Usome "*Bismillah*" kabla ya kuanza kunyonyesha. Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Kila tendo la muhimu na la thamani ambalo linatendeka bila ya utajo wa "*Bismillahi Rahmani-Rahim*," litakuwa halikukamilika na halitakuwa na matokeo mema."

3. Mnyonyeshe mtoto pamoja na kumkumbuka Imam Husein (a.s.), kwani imesimuliwa kutoka kwa Imam huyo: "Enyi Shi'ah wangu, kila wakati mnapokunywa maji yenye siha basi nikumbukeni mimi."

4. Wakati wa kunyonyesha mwangalie mtoto huyo na uzungumze naye.

Hususan kuzungumza juu ya vifo vya kishahidi na kuzaliwa kwa Ma'asumin (a.s.) kunashauriwa sana; usijali kama mtoto anaelewa au laa. Mama anayetaka kupitisha (kurithisha) utamaduni na desturi ya Ahlul-Bayt (a.s.) kwa mtoto wake anahitajia kuwa na utamaduni wa kidini yeye mwenyewe na alitekeleze hili wakati anapomfundisha na kumnyonyesha mtoto wake.

5. Subira na utulivu, hasira na hali ya kukasirika mawazo mazuri na mabaya, tabia ya ukarimu na huruma na ukaidi na hali ya ulipizaji visasi vyote hivi vina athari kwa mtoto. Ni lazima na muhimu kukumbuka kwam- ba mustakabali wa mtoto uko mikononi mwa vitendo vyako wewe.

6. Kila siku ya wiki, tekeleza majukumu yako ya kila siku kama vile kupika, kufanya usafi, kula na kunyonyesha, huku ikiwa ni pamoja na kumkumbuka Ma'sumin wa siku hiyo, kama ilivyoainishwa katika *Mafatihul-Jinan*:

Jumamosi: Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.).
Jumapili: Imam Ali (a.s.) na Hadhrat Fatimah(a.s.).
Jumatatu: Imam Hasan na Imam Husein (a.s.).
Jumanne: Imam Zainul-Abidiin (a.s.), Imam Muhammad al-Baqir na Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.).
Jumatano: Imam Musa al-Kadhim, Imam Ali ar-Ridhaa, Imam Muhammad at-Taqii na Imam Ali an-Naqii (a.s.).
Alhamisi: Imam Hasan al-Askarii (a.s.).
Ijumaa: Imam Mahdi (a.s.).

7. Kama ilivyoshauriwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), uanze vitendo vyako kwa Qur'ani Tukufu, na kumdhukuru Mwenyezi Mungu na kuwakumbuka Ahlul-Bayt (a.s.) – (Pamoja na Duaul-Faraj kwa ajili ya Imam Mahdi a.s.).

8. Mshukuru na kumtukuza Mwenyezi Mungu Mtukufu baada ya kunyonyesha kwako.

9. Mwishowe kabisa, vifanye vitendo vyako, hususan kunyonyesha, kwa nia ya kutafuta radhi za
Mwenyezi Mungu Mtukufu na ukaribu Naye.

Kumuachisha Mtoto Ziwa (Kunyonya)

Ni17 muhimu kumkumbusha msomaji kwamba ingawa kuna njia nyingi sana za kumuachisha mtoto ziwa, kitabu hiki kinataja chache tu ambazo zimeelezwa katika vyanzo vya Kiislam na Ahlul-Bayt (a.s.):

1. Usiwe mkali kwa mtoto, na ujiepushe mbali na mbinu kama za kupaka viungo vikali kama pilipili,
na kadhalika.

2. Wakati mtoto anaposisitiza katika kunyonya, usimfukuzie mbali na wewe.

3. Kwa kuzingatia ukweli kwamba kunyonyesha sio kwamba ni chanza cha chakula tu, bali kwamba ni chanzo cha ukaribu na utulivu kwa ajili ya mtoto vilevile, ni muhimu kwamba, sambamba na vyakula vingi mbadala, upendo mwingi na wakati mzuri pamoja na mtoto hakikisha vinapatikana pia.

4. Kuchagua wakati muafaka na mahali pazuri kwa ajili ya kuanza na kumalizia kwa vitendo, hususan vile vyenye muhimu na thamani, ni moja ya mbinu za wanavyoni wa Kiislam.

Kwa hiyo, inastahili tu kwamba kwa ajili ya kumkatisha mtoto kutoka kwenye kitendo muhimu kama cha kunyonya, mahali na wakati mzuri vichaguliwe, na kutekelezwa kwa kutiliwa maanani ule utayari wa mtoto na uwasilishaji wa fursa nzuri.

5. Pale inapowezekana, mahali bora zaidi ni kwenye haraam (quba) za Maimam (a.s.) au Imamzade (maquba ya watoto wa Maimam).

6. Ushauri wa mwanachuoni ni kama ufuatao:

Katika miezi ya mwisho ya unyonyeshaji wakati uamuzi unapokuwa umefanyika wa kumsimamisha polepole mtoto kunyonya, chukua wudhuu na uingie kwenye haraam katika hali ya kutakasika. Mara unapoifikia kaburi tukufu (dariih), soma ziarat inayostahili na uombe tawasuli (uombezi mtukufu) wa mtu huyo mtukufu. Halafu chukua komamanga tamu lililomenywa na ukae ukielekea Qiblah. Wakati unaposoma Surat Yaasin, mnyonyeshe mtoto kutoka kwenye matiti yote hadi maziwa yanapokwisha, na upulize kwenye komamanga hilo mara kwa mara.

Mwishoni mwa kisomo hicho, wasilisha thawabu za kisomo hicho ziende kwa roho ya Ali Asghar, mtoto wa miezi sita, na kwa mama yake. Kisha muombe Mwenyezi Mungu akikubalie kipindi hicho cha unyonyeshaji kwa ukarimu Wake, na akujaalie na riziki yenye maana kwa watoto wako kwa kwisha kipindi cha kunyonyesha. Kisha mlishe mtoto hilo komamanga lote (au majimaji yake – juisi).

Angalizo: Utamu wa komamanga umetiliwa mkazo mahsusi hasa. Pia kwa kawaida, ulaji wa komamanga ni wenye manufaa sana, hususan katika siku za Ijumaa, na limehusishwa na utulivu uliozidi kiasi, na kuondoa fadhaa na wasiwasi.

Angalizo: Kama kwenda kwenye Haraam hakuwezekani kwa sababu za kijiogorafia au nyinginezo, inawezekana kufanya nia ya kutembelea Quba na kufanya vitendo vyote vilivyoshauriwa ukiwa nyumbani.

1. al-Kafi, Jz. 6, Uk. 40, hadithi ya 2
2. Wasa'ilush-Shi'ah, Jz. 21 Uk. 453
3. Surat al-Abasa; 80:24, na Surat al-Baqarah; 2:167 na 172
4. Thawab al-Amaal, Uk. 566
5. Rayhaaney-e Behesht, Uk. 177
6. Mafasid Maal wa Luqme Haraam.
7. Kianuri alikuwa aina ya mtu ambaye alitekeleza vitendo vya kukiri mwenyewe vya "kijasusi, udanganyifu na uhaini."
8. Tarbeat Farzand az Nazr Islam, Uk.89
9. Mustadrak al-Wasa'il, Jz. 15, Uk. 256
10. Tibb an-Nabii, Uk. 25
11. al-Kafi, Jz. 6, Uk. 40.
12. Rayhaaney-e Behesht, Uk. 184-187
13. Mustadrak al-Wasa'il, Jz. 15, Uk. 157, hadithi ya 17848
14. Tahdhib al-Balaghah, Jz. 8, Uk.106, hadithi ya 6
15. Tahdhib al-Balaghah, Jz. 8, Uk.106, hadithi ya 7
16. Tahdhib al-Balaghah, Jz. 8, Uk.105, hadithi ya 4
17. Rayhaaney-e Behesht, Uk. 212-213

Mlango Wa 10: Kanuni Muhimu Za Sheria (Fiqh)

Kwa Ajili Ya Akina Mama

Nifaas Ni Nini?

Kuanzia wakati pale kuzaliwa kwa mtoto kunapotokea, ile damu anayoiona mama mzazi ni Nifaas, madhali inasimama kabla au katika kukamilika kwa siku ya kumi. Ambapo katika hali ya *Nifaas*, mwanamke anaitwa *Nafsa*.

1. Ile damu ambayo mama anaiona kabla ya kutokeza kwa kiungo cha kwanza cha mtoto sio *Nifaas*.1

2. Inawezekana kwamba damu ya *Nifaas* inaweza ikatoka kwa muda mfupi tu, bali kamwe haizidi
siku kumi.2

3. Ni muhimu kwamba mtoto anakuwa kikamilifu. Hata kama mtoto mwenye upungufu (wa muda wa mimba yake) atazaliwa, ile damu anayoiona mama mzazi huyo kwa muda wa siku kumi itakuwa ni *Nifaas*. Maneno 'kuzaliwa mtoto' lazima yatumike kwake.3

4. Endapo mwanamke anakuwa na mashaka kwamba ameharibu chochote (mimba) au hapana, sio lazima kwa yeye kufanya uchunguzi, na ile damu ambayo inatoka katika hali

hiyo sio *Nifaas*. 4

Mambo ambayo ni wajibu na yale ambayo yamekatazwa au kuharamishwa kwa mtu aliyeko katika hali ya Nifaas.

Kwa msingi wa tahadhari, kukaa ndani ya Msikiti na vitendo vingine ambavyo vimeharamishwa kwa mwanamke mwenye hedhi vilevile vime- haramishwa kwa mwanamke Nafsa na vile vitendo ambavyo ni wajibu kwa mwanamke mwenye hedhi pia ni wajibu kwa Nafsa.5

Nifaas Inachukua Muda Gani?

Inawezekana kwamba damu ya Nifaas ikaweza kutoka kwa muda mfupi tu, lakini kamwe haizidi siku kumi. Kwa kutegemea tabia ya kawaida ya mwanamke mwenye hedhi, kanuni za urefu wa Nifaas zinatofautiana kama ifuatavyo:6

1. Kwa Mwanamke Mwenye Tabia Ya Kudumu Ya Hedhi:

a. Nifaas yake itakuwa sawa na kitambo cha muda wa hedhi.

b. Kama tabia yake ni chini ya siku kumi, baada ya muda huu anayo fursa ya kuacha swala yake hadi siku kumi, au afanye kama mustahadha (mwanamke aliyeko kwenye hali ya Istihaadha); hata hivyo, ni bora kuziacha swala kwa siku moja (zaidi ya idadi ya zile siku alizokuwa na kipindi kabla ya mimba).

c. Endapo hata hivyo, damu hiyo itaendelea kuonekana hata baada ya siku kumi, basi siku zote baada ya kipindi na kawaida cha hedhi, mpaka ile siku ya kumi, itakuwa ni istihaadha, na ni lazima afanye kadha ya kila kitendo cha ibada ambacho hakikufanyika katika wakati huu hadi siku ya kumi (kwani atakuwa amefuata kanuni za istihaadha baada ya siku ya kumi kwa vyovyote).

d. Anapokuwa kama mustahadha, ni lazima ajiepushe kutokana na vitendo haramu kwa mwanamke Nafsa vile vile mpaka siku ya kumi na nane.

Kwa mfano: Kama muda wa hedhi ya mwanamke wakati wote imekuwa ni siku sita na damu yake ikamtoka kwa zaidi ya siku sita, anapaswa kuzifanya siku sita kama Nifaas na ile siku ya 7, 8, 9, 10, (kama kutokwa na damu hakuzidi siku kumi) itakuwa ni fursa ya hiari yake ama kujizuia na vitendo vyote vya ibada au kutwaa kanuni za istihaadha.

Endapo hata hivyo, anaona damu kwa zaidi ya siku kumi, zile siku zote za ziada ya muda wake wa desturi wa hedhi utahesabiwa kama siku za istihaadha na itabidi kufanya kadha ya swala zilizokosekana kuswaliwa kama alichagua kujizuia na vitendo vyote vya ibada katika ile siku ya saba, ya nane, ya tisa na ya kumi.

2. Kwa Mwanamke Ambaye Hana Desturi Ya Kudumu Ya Hedhi

a. Nifaas yake itakuwa kwa siku kumi, na zinazobakia zitakuwa istihaadha.

b. Ni tahadhari inayoshauriwa kwamba pale unapojichukulia kama aliye mustahaadha, ujiepushe na vitendo vilivyoharamishwa kwa mwanamke Nafsa kuanzia ile siku ya 10 hadi siku ya 18. Wakati kipindi cha Nifaas kinapokuwa kimekwisha: 7

Pale mwanamke anapokuwa amesafika kitohara kutokana na Nifaas, ni lazima achukue

josho (ghusl) na afanye vitendo vya ibada. Endapo ataona damu tena mara moja au zaidi, kuna uwezekano namna mbili:

1. Jumla ya idadi ya siku ambamo damu inaonekana mara tu baada ya kujifungua na zile siku zinazoingilia kati wakati anapokuwa msafi kitohara ni siku kumi au chini yake, basi yote hiyo itakuwa ni Nifaas. Katika zile siku zinazoingilia kati, kama tahadhari, atachukua wudhuu na kuswali kama mwanamke mwenye tohara na kujiepusha vile vile na vitendo ambavyo ni haramu kwa mwanamke aliyeko kwenye Nifaas. Hivyo, endapo alifunga saumu, atazilipia kadha yake.

2. Endapo ile damu ambayo aliiona baadae itazidi siku kumi hapo tena, kanuni zinatofautika kutegemea juu ya tabia ya kawaida ya hedhi ya mwanamke huyo:

A. Kwa Mwanamke Mwenye Tabia Ya Kudumu Ya Hedhi:

Kama tahadhari, ni lazima aichukulie ile damu iliyoonekana baada ya kipindi cha hedhi cha kawaida kuwa ni istihaadha; kwa hiyo lazima afanye kama aliye mustahaadha, na vile vile ajiepushe na yale yote ambayo ni haramu kwa mwanamke nafsa.

B. Kwa Mwanamke Asiye Na Tabia Ya Kudumu Ya Hedhi:

Lazima azihesabu zile siku kumi za mwanzo kama Nifaas, na zinazobakia ziwe kama ni istihaadha. Kubainisha Hedhi. 8 Kanuni za kubainisha hedhi ya kwanza ya mwanamke baada ya kujifungua mtoto tena ni ya kutegemea juu ya tabia ya kawaida ya hedhi ya mwanamke huyo.

1. Kwa Mwanamke Mwenye Tabia Ya Kudumu Ya Hedhi:

a. Kama damu itaonekana mfululizo kwa mwezi mmoja au zaidi baada ya kumzaa mtoto, ile damu inayoonekana kwa zile siku zinazolingana na kawaidi yake ya hedhi itakuwa ni Nifaas, na ile damu inayoonekana baada ya hapo kwa muda wa siku kumi itakuwa ni istihaadha, hata kama itaangukia wakati mmoja na tarehe zake za hedhi ya kila mwezi.

b. Baada ya kupita kwa zile siku kumi za istihaadha, endapo kutokwa na damu kutaendelea, basi hiyo ni hedhi kama itaangukia kwenye siku za desturi ya kawaida, bila ya kujali kama inazo dalili za hedhi9 au hapana. Kama kuvuja damu hakutokei katika siku za hedhi ya kawaida, ni lazima asubiri mpaka zile siku za kawaida, hata kama itamaanisha kusubiri kwa mwezi au zaidi na hata kama damu ina dalili za hedhi.
Kwa mfano: Mwanamke ana tabia ya kudumu ya hedhi ya kuanzia tarehe 20 hadi 27 ya kila mwezi.

Anajifungua mnamo tarehe 10 ya mwezi, na anaendelea kuona damu kiasi cha mwezi au zaidi; Nifaas yake itakuwa siku saba, sawa na siku za hedhi yake, na itakuwa ni kuanzia tarehe 10 ya mwezi huo hadi tarehe 17; sasa, ile damu anayoendelea kuona kuanzia tarehe 17 hadi tarehe 27, yaani kwa muda wa siku kumi, hii itakuwa ni isti- haadha hata kama inaangukia katika siku za tabia yake ya hedhi.

c. Kama hana tabia maalum ya muda wa kuanza kwa hedhi, lazima afanye juhudi ya kutambua hedhi yake kwa dalili zake, na endapo hiyo itakuwa haiwezekani (kwa sababu damu inayoonekana baada ya Nifaas mara nyingi hubakia ya namna moja kwa mwezi mzima au zaidi), basi anapaswa kutwaa tabia iliyopo kwa wakati huo miongoni mwa ndugu zake wa damu (mama, dada zake, na kadhalika) ili kuamua siku za hedhi yake. Kama hilo nalo haliwezekani, basi anayo hiari ya kuchagua kupanga siku zake za hedhi.10

2. Kwa Mwanamke Asiye Na Tabia Ya Kudumu Ya Hedhi:

a. Kama ilivyoelezwa mapema, ile damu inayoonekana katika ule muda wa siku kumi za mwanzo itafanywa kuwa ni Nifaas, na kuhusu zile siku kumi zinazofuatia itakuwa ni istihaadha. Damu itakayoonekana baada ya hapo inaweza ikawa ama ni hedhi au istihaadha, na ili kuhakikisha kama ni hedhi, anapaswa kufuata kanuni kama hiyo hapo juu, yaani, kuitambua hedhi kwa dalili zake, kwa tabia iliyopo wakati huo miongoni mwa ndugu zake wa damu, au kupanga siku zake mwenyewe za hedhi.

Mikojo Ya Mtoto

Kuvifanya vitu kuwa safi kitohara kutokana na mikojo ya mtoto anayenyonya: Endapo kitu chochote kinakuwa najisi kutokana mikojo ya mtoto anayenyonya, ambaye bado hajaanza kula chakula chochote kigumu, na, kama tahadhari, yuko chini ya umri wa miaka miwili, kitu hicho kitakuwa tohara kama kitamwagiwa maji mara moja juu yake, yakifikia sehemu zake zote ambazo zimenajisika. Kama tahadhari inayoshauriwa, maji yanapaswa kumwagwa juu yake mara nyingine tena. Kama ni zulia au nguo na kadhalika, haitakuwa lazima kuikamua.[11]

1. Sheria za Kiislam, Kanuni ya 515
2. Sheria za Kiislam, Kanuni ya 517
3. Sheria za Kiislam, Kanuni ya 516
4. Sheria za Kiislam, Kanuni ya 518
5. Sheria za Kiislam, Kanuni ya 519
6. Sheria za Kiislam, Kanuni ya 523, 524, 525, 526
7. Sheria za Kiislam, Kanuni ya 520
8. Sheria za Kiislam, Kanuni ya 525
9. Dalili za hedhi: Kwa kawaida ni damu nzito na yenye joto na rangi yake ni ama nyeusi au nyekundu. Inatoka kwa nguvu na muwasho kidogo.
10. Tafadhali rejea kwenye mlango wa Hedhi wa kitabu Risalah kwa taarifa zaidi.
11. Sheria za Kiislam, Kanuni ya 162

Mlango Wa 11: Malezi Ya Mtoto

Mambo 40 Juu Ya Aklaq (Tabia) Katika Mahusiano Na Mtoto Wako

Mambo 40 Juu Ya Aklaq (Tabia) Katika Mahusiano Na Mtoto Wako:[1]

1. Utoe zawadi kwa mabinti zako kwanza.

2. Cheza na watoto wako.[2] Hili lina athari muhimu katika kumfundisha na malezi ya mtoto wako. Viongozi wetu katika Uislam wamesisitiza umuhimu wa jambo hili, na wamelipendekeza sana kwa Waislam.

Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba: “Mtu ambaye ana mtoto, anapaswa kuwa na tabia kama mtoto aapokuwa pamoja naye.”[3] Pia imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s) kwamba : “Yeyote ambaye anaye mtoto, anapaswa kwa ajili ya mafunzo

yake kujishusha mwenyewe mpaka kwenye kiwango chake cha utotoni.”4

3. Msiwapige watoto wenu wakati wakiwa wanalia, kwa sababu imes- imuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba: “Msiwapige watoto wenu wanapolia kwani kulia kwao kuna maana. Miezi minne ya kwanza ya kulia ni kukiri Upweke wa Allah, miezi minne ya pili ya kulia ni kumtakia rehma na amani Mtume na kizazi chake na miezi minne ya tatu ya kulia ni mtoto kuwaombea wazazi wake.”5
4. Busu watoto wako. Imesimuliwa kutoka kwa mmoja wa Maimam kwamba: “Mbusu sana mwanao kwa sababu kwa kila busu, utapewa cheo kitukufu cha kiungu ambacho vinginevyo itakuchukua miaka 500 kupata cheo hicho!” 6

Imesimuliwa pia kwamba mtu mmoja wakati mmoja alikuja kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akasema: “Mimi sijawahi kubusu mtoto wangu kamwe.” Mtukufu Mtume akasema: “Kwa kweli mtu kama huyu atakuja kuwa mkazi wa moto wa Jahannam.”

5. Kwa kutoa salaam kwa mwanao, kunajenga hisia yake ya nafsi na tabia. Kama vijana wakitoa salaam ni wajibu kwa wakubwa kujibu; hata hivyo, ilikuwa ni tabia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kutoa salam kwanza, ama kwa wakubwa au kwa wadogo**.**7

6. Usivikebehi vitendo vya mwanao, wala usiviite ni vya kijinga.

7. Usimwamrishe au kumkataza sana mwanao, kwani hili linawatia sana hamasa na kuwapelekea kuwa na tabia ya ukaidi watakapokuwa wakubwa.

8. Jenga tabia ya wanao kwa kuwaheshimu. Tunasoma katika hadithi kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alirefusha sajidah yake mpaka wajukuu zake waliposhuka kutoka mabegani mwake, na nyakati zingine aliswali swala za jamaa haraka sana wakati aliposikia watoto wa mama zao wanaoswali wakilia. Kadhalika, Imam Ali (a.s.) alikuwa akiwauliza wanawe maswali kuhusu mambo ya kidini mbele ya wengine, na hata kuy- atoa maswali ya watu kwao ili wapate kuyajibu.

Wakati wazazi wasipotosheleza shauku za asili na matamanio ya mtoto, basi mtoto anakimbilia kwenye njia potovu na mbinu (mara nyingi zinazofananishwa na makosa) ili kujaribu kujipa mwenyewe msukumo muhimu kujenga hisi za nafsi yake na umaarufu. Shaksia, uhuru, dhamira, kujiamini binafsi, na kadhalika udhaifu, uovu na kukosa kujiamini zote ni tabia na desturi ambazo misingi yake ipo mapajani mwa baba yake na kifua cha mama yake. Mtoto ambaye hakufanyiwa kama binadamu wengine au kama mwanafamilia mwenye thamani hawezi kutegemewa kuwa na shaksia iliyojengeka vyema katika utu uzima wake.

9. Timiza ahadi zako. Kutimiza ahadi katika Uislam ni alama ya imani yake mtu, na Mwenyezi Mungu Mtukufu anakutaja huku katika Qur’ani Tukufu:

وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ ۖ إِنَّ الْعَهْدَ كَانَ مَسْئُولًا {34}

“….. Na timizeni ahadi zenu, kwani ahadi ni yenye kuulizwa.” (Bani Israail; 17:34).

وَالَّذِينَ هُمْ لِلأَمَانَاتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ {8}

“Na wale ambao kwa amana zao na ahadi zao ni wenye kutekeleza.” (Al-Mu’minun; 23:8).

Kutimiza ahadi ni moja ya nguzo za ustawi wa mwanadamu na moja ya sifa bora kabisa za tabia za mtu, msingi wake ukiwa juu ya malezi na mafunzo yake mtu. Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba: “Wapende watoto wako na uwafanyie upendo na upole. Pale unapowaahidi, ni lazima utimize ahadi hizo, kwa sababu wanakuchukulia wewe kama mpaji wao.

10. Na kuhusu kuwafundisha watoto mambo ya kijinsia, wazazi ni lazima kwanza wawafundishe watoto wao kutoingia chumbani kwa wazazi wao bila ya kuomba ruhusa. Mwenyezi Mungu ameelekeza kwenye suala hili muhimu ndani ya Suratun-Nuur; Aya ya 58:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لِيَسْتَأْذِنْكُمُ الَّذِينَ مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ وَالَّذِينَ لَمْ يَبْلُغُوا الْحُلُمَ مِنْكُمْ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ ۚ مِنْ قَبْلِ صَلَاةِ الْفَجْرِ وَحِينَ تَضَعُونَ ثِيَابَكُمْ مِنَ الظَّهِيرَةِ وَمِنْ بَعْدِ صَلَاةِ الْعِشَاءِ ۚ ثَلَاثُ عَوْرَاتٍ لَكُمْ ۚ {58}

“Enyi mlioamini! Wakuombeni ruhusa wale iliyowamiliki mikono yenu, na wale wasiofikia balekhe miongoni mwenu mara tatu: Kabla ya swala ya Alfajiri na mnapovua nguo zenu wakati wa adhuhuri na baada ya Swala ya Isha; hizi ni nyakati tatu za faragha kwenu. …..”
(An-Nuur; 24:58).

Inashauriwa pia kuweka uangalizi wa karibu na udhibiti juu ya vitendo vyao pamoja wengine na kuzuia vile vitendo ambavyo vinaongeza hisia za kijinsia (kwa mfano, kwenda kwenye makundi yenye mchanganyiko). Ni muhimu kueleza hapa kwamba udadisi wao unakuwa mkubwa sana katika utoto wao. Kwa nyongeza, wanakuwa na hisia kali sana katika yale wanayoyaangalia na kuyaona, na bila ya woga wakataka kuyaweka katika vitendo na kuyajaribu wao wenyewe bila ya kujua au kufikiri kwamba kile wanachokifanya kinaweza kuwa sio sahihi.

Baadhi Ya Mambo Muhimu Ya Kuangaliwa

a. Akina mama ni lazima wawe waangalifu sana wakati wanapochunga usafi wa watoto wao (kwa mfano kuwaogesha), hata vile vichanga ambavyo ndio kwanza kuzaliwa, kwamba watoto wengine wanakuwa hawapo, hasa wale ambao ni wa jinsia tofauti.

b. Kutokea utotoni, wazazi wasicheze na viungo vya watoto vya uzazi, au hata vifua vyao na mapaja yao.

c. Kamwe usiwaache watoto peke yao au kwenye sehemu za faragha kwa vipindi virefu vya muda na wakati wanapokuwa wanapita kwenye awamu za udadisi. Pia si jambo linaloshauriwa kuwaacha bila kushughulikiwa wakiwa na mtu mwingine katika wakati huu, hasa kaka au dada.

d. Msiwaache wasichana wenye umri wa miaka sita wakae kwenye mapa- ja ya mwanaume

asiye maharimu au wapigwe mabusu na wanaume wasio maharimu wao.

e. Msiwaache wasichana wakae uchi mbele ya watu wengine. Hususan vifua vyao na mapaja ni lazima vifunikwe.

f. Jenga mapenzi ya Swala ndani ya watoto wako, kama Mwenyezi Mungu Mtukufu anavyosema ndani ya Qur'ani Tukufu kwamba Swala inamwepusha mbali mtu na vitendo viovu:

إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ {45}

"..... Hakika Swala huzuia mambo machafu na maovu ..... (Ankabuut; 29:45).

11. Kumharibu mtoto kunasababisha udhaifu, na ukosefu wa nia na dhamira. Watoto wa namna hii huwasumbua wazazi wao katika utoto wao, na huwafanya wapambane na matatizo mengi.

Watoto Walioharibika, Wao Binafsi Hukabiliwa Na Matatizo Mawili:

a. Wanayo matumaini yanayoegemea kwenye matakwa ya jamii, kama wazazi wao, kuwaliwaza na kuwaheshimu kwa hali yoyote ile iwayo, bila ya swali lolote lile. Pale wanapotambua kwamba watu sio tu kwamba hawatafanya hivyo, bali pia watayadhihaki matamaini hayo, wanachanganyikiwa na kujihisi wamefedheheshwa na kushushiwa hadhi yao.

b. Hali kama hizo huunda msingi wa dharau na kuwafanya wachukie, jeuri, wanaokosa subira na wanyonge. Wanakuwa aina ya watu wanaowafikiria wengine kwa uduni na wanawatendea vitendo na maneno makali.

12. Hakuna kinachoweza kuzima hisia za kujiamini binafsi kwa mtoto zaidi kuliko kumlazimisha kufanya mambo wanavyoweza kuwa hawana uwezo wa kuvifanya. Hii hasa ndio hali wakati endapo mtoto hana mafanikio, inafuatiwa na kauli za kukatisha tamaa: "Usijisumbue kujaribu, hutaweza, huna uwezo huo."

13. Swali kwa ajili ya watoto wako, tangu wakati wa mimba na baada ya kuzaliwa pia.8

14. Ukumbusho na maombi lazima vitolewe kwa upole na uangalifu ili visije vikasababisha kizuizi kati ya wazazi na mtoto. Siku moja, Imam Hasan (a.s.) aliwaita watoto wake na watoto wa ndugu yake pamoja na akawaambia: "Ninyi wote ni watoto wa jamii ya leo, na inategemewa kwamba ni viongozi wa jamii ya kesho. Kwa hiyo, someni, jifunzeni na fanyeni juhudi ya kupata elimu, na yeyote ambaye hana kum- bukumbu nzuri na hawezi kuyahifadhi masomo yanafundishwa na mwalimu wakati wa vipindi vya masomo, (anapaswa) ayaandike na ayaweke nyumbani." Hivyo tunaona kwamba Imam alisababisha mapenzi ya kupata elimu ndani yao bila kutumia mbinu kama kuwatishia au kuwalazimisha, bali kwa kuwafanya wao waelewe kwamba elimu ndio njia ya kwenye heshima na utukufu.

15. Endapo mtoto wako akiheshimiwa, anao mwelekeo mdogo sana wa kuasi kanuni za nyumbani humo. Heshima na maingiliano mazuri kati ya wazazi na mtoto ndio msingi katika kuunda tabia ya mtoto, imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Waheshimuni watoto wenu na zungumzeni nao kwa desturi nzuri na kwa namna inayopendeza."

16. Mfano mzuri wa maadili ni mtu ambaye anayerekebisha tamaa za watoto wake kwa hekima sana pamoja na mbinu sahihi.

17. Lea imani ya mtoto wako. Watoto ambao wamekuzwa tangu mwanzoni na imani ya Mwenyezi Mungu Mtukufu wanayo dhamira yenye nguvu na moyo shupavu, na kuanzia miaka yao ya awali kabisa wanakuwa wamekomaa na wajasiri; hili linaonekana kirahisi kwa vitendo na maneno yao. Utayari wa moyo wa mtoto kujifunza imani na akhlaq ni kama ardhi yenye rutuba ambamo aina yoyote ya mbegu inaweza kumea na kukua. Kwa hiyo wazazi ni lazima wawafundishe watoto wao mapenzi juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Ahlul-Bayt (a.s.) na viongozi wa Uislam kuanzia kwenye fursa zao za mapema kabisa.

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba: “Wafundisheni hadithi watoto wenu mapema sana iwezekanavyo, kabla wapingaji (wa imani zenu) hawajawafikia kabla yenu.”9

Katika hadithi, wazazi ambao hawazingatii maisha ya baadae (akhera) ya watoto wao wanaonywa vikali. Imesimuliwa kwamba macho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yaliangukia kwa watoto fulani na yeye akasema: “Ole kwa watoto wa zama za mwisho (kabla ya kudhihiri kwa Imam wa 12) kwa sababu ya taratibu zisizopendeza za baba zao.” Yeye akaulizwa: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni kwa sababu ya baba zao washirikina?” Yeye akajibu akasema: “Hapana, kwa sababu ya baba zao Waislam ambao hawakuwafundisha watoto wao wajibu wowote wa kidini. Wao waliridhika na mambo ya kimaada yasiyo na thamani kwa ajili yao. Nimechoshwa na watu kama hao na sina haja nao.” 10

Inasemekana kwamba katika Urusi ya kikomunisti, wao walikuwa waki- uondoa uwepo wa Mwenyezi Mungu kutoka kwenye kiwango cha chini kabisa; kwa mfano, wakati watoto walipokuwa na njaa au kiu, wazazi wao wangewaacha walie a kumwaambia, “Muombeni Mwenyezi Mungu aku- ruzukuni.”

Pale watoto walipofanya hivyo, na bado wakabakia na njaa na kiu, wao walikuwa wakiwaambia, “Mnaona, mmemlilia Mungu na hakukupeni chochote! Sasa muombeni Lenin (kiongozi wa Urusi) awape riziki!” Pale watoto walipofanya hivyo, ndipo hapo tu walipoweza kuwa- pa chakula na kinywaji. Matokeo ya hili ni kwamba, walipandikiza ndani ya watoto kuanzia utotoni mwao kwamba hakuna Mungu kupitia njia hii ya udanganyifu. Dhani hii hii inashutumiwa ndani ya Qur’ani Tukufu, Sura ya Yaasiin, Aya ya 47:

قَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ آمَنُوا أَنُطْعِمُ مَنْ لَوْ يَشَاءُ اللَّهُ أَطْعَمَهُ إِنْ أَنْتُمْ إِلَّا فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ {47}

“….. Wale waliokufuru huwaambia wale walioamini: Je, tumlishe ambaye Mwenyezi Mungu akipenda atamlisha? Ninyi hammo ila kati- ka upotevu dhahiri…..” (Surat Yaasiin; 36:47).

Hata hivyo, hili ni soma zuri sana kwetu sisi la jinsi Mwenyezi Mungu Mtukufu anavyopaswa kutambulishwa kwa watoto tangu umri wa utotoni. Wakati wowote watoto wanapofikia kwenye umri ule ambao kwamba wanaelewa kwamba wakati wowote wanapotamani kitu, wanahitajia kuwaomba wazazi wao, basi wazazi wao wanapaswa kuwataka kwanza waombe kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Kisha pale wanapowapatia kile kitu walichokihitaji, wazazi wanapaswa kusisitiza kwamba kimewafikia wao kupitia kwenye rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hivyo, jinsi wanavyoendelea kukua, watakuwa na uwezo wa kumuona Mwenyezi Mungu Mtukufu kama

ndiye msingi mkuu nyuma ya kila kitendo.

18. Kaa mbali na tabia ya kukamatana mikono na utawala juu ya watoto.

19. Moja ya wajibu wa wazazi ni kulea ile tabia ya asili ya kusema kweli ndani ya watoto. Tabia zao ndani ya nyumba zinapaswa kuwa za namna ambayo kwamba hii inakuwa ni desturi yao. Hata hivyo, hili ni moja ya maeneo magumu sana ya kumkuza mtoto na uangalifu kwenye elimu na vitendo ni muhimu sana.

Imesimuliwa katika hadithi kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Mwenyezi Mungu awe na huruma kwa mtu yule ambaye anawasaidia watoto wake katika kufanya wema.” Msimuliaji wa hadithi hii aliuliza: “Kwa vipi?” Katika jibu lake, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitoa maelekezo manne:

a. Chochote kile alichonacho mtoto katika uwezo wake na akawa amekifanya, basi kikubali.
b. Usitarajie kile ambacho ni kigumu kwake.
c. Mkinge kutokana na dhambi.
d. Usimuongopee wala kufanya mambo ya kijinga.

20. Usitumie hofu kama njia ya kumkuzia mtoto wako, kwani hili linasababisha madhara kwenye utu wao na kupelekea kwenye matatizo ya kisaikolojia. Hususan adhabu za kupindukia kutoka kwa mama zinadhoofisha uhusiano na thamani ambayo mtoto anakuwa nayo juu ya mama yake ndani ya moyo wake. Mara nyingi, kutazama au kukaa kimya kunaweza kuwa na nguvu zaidi katika kuwafanya watoto kuelewa makosa yao kuliko kuwapiga au kuwatishia.

21. Kumkumbatia na kumbusu mtoto ni moja ya chakula chao cha roho, na ni muhimu sana kwamba kiasi cha kutosha cha jambo hili kinatolewa kwao. Moja ya sababu ya kwa nini mtoto analia inaweza kuwa kwamba ana kiu juu ya huku kuonyeshwa upendo. Watoto wanaokua kwa upendo mwingi wanakuwa na utu wa kujiamini ambao hauyumbishwi na matatizo yanayojitokeza katika maisha.

Inasimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Kwa hakika Mwenyezi Mungu huonyesha huruma kwa mja Wake ambaye ana mapenzi makubwa kwa watoto wao.”[11]

Imesimuliwa vile vile kutoka kwa Imam huyo: “Nabii Musa alimwambia Mwenyezi Mungu yafuatayo wakati alipokuwa kwenye mlima Tuur: ‘Ewe Allah! Ni tendo gani lililo bora kwa mujibu Wako?’ Mwenyezi Mungu akamjibu: ‘Kuwapenda watoto ndio tendo bora.’”

22. Wazazi wanao wajibu wa kuwafanya watoto wao kuelewa ubaya wa dhambi na kujenga chuki kwa ajili ya watu wanaoshiriki katika hili, na kadhalika kukemea maovu na kuyatia moyo matendo mema ya mtoto. Hata hivyo, kukemea na kuvutiwa kuna wakati na mahali pake na kusi- fanywe kupita kiasi kwani hili lenyewa linaweza kumpotosha mtoto.

23. Vitanda vya watoto wa miaka sita na zaidi lazima vitengwe mbali na kila kimoja, hata kama wote ni wasichana au wote ni wavulana.[12]

24. Pamoja na tabia asilia ambazo mtoto anarithi kutoka kwa wazazi wake, mazingira na malezi ya mtoto yana athari kubwa. Ni kutowezekana kukubwa sana kwamba ndani ya familia ambayo haishughuliki sawa- sawa, mtoto wa desturi na kawaida anakuzwa. Hasa, yale maelekezo ya wazazi yanakuwa na matokeo tu kama wazazi hao wanaongoza kwa mfano. Hatua ya kwanza ya kumkuza mtoto ni malezi ya nafsi.

Mtu ambaye hana tabia nzuri hawezi kumuongoza mwingine kwenye akhlaq nzuri, na kadhalika, wazazi wenye hasira kali kwa kawaida hawawezi kukuza mtoto mtulivu na mwenye subira.

Watoto wanahitaji kufundishwa kwamba tabia kama vile kusema uongo, kusengenya, lugha chafu na kadhalika, ni sifa ambazo hazipendezi, na kwa kawaida, mtoto atajiepusha kutokana na mambo kama hayo pale tu wazazi watakapokuwa wameweka mifano kama hiyo.

25. Ni lazima pawe na tofauti katika taratibu na matarajio ya tabia ya mtoto ndani ya nyumba, na nje pia. Hapo nyumbani, mruhusu mtoto kucheza kwa uhuru.

26. Wakati wote zivumilie tabia zisizotegemewa za mtoto wako kwa kiwango cha ukomo, na usiyachukulie makosa ya mtoto wako wakati wote kuwa ni yasiyosameheka, ili kwamba uwe hulazimiki wakati wote kumuadhibu. Subira, kuvumilia na msamaha ni lazima wakati unapomkuza watoto. Kama mwanao anayo sifa ambayo huipendi, inapaswa kusahihishwa kwa njia ya busara bila kuonyesha kumdharau mtoto, na namna sahihi ya kufanya mambo inapaswa kuonyeshwa wakati uleule kama kumzuia na njia za kizamani.

Pale wazazi wakiwakaripia watoto wakati wote, wanawadhalilisha watoto hao na sio tu kwamba hawatakuwa na mafanikio katika kumrekebisha mtoto, bali pia watawasababishia tabia ya ukaidi. Imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.): “Makaripio yaliyozidi yanachochea moto wa kiburi. 13

27. Unapokuwa unamwelekeza mtoto, usitaje majina ya watoto wengine kila mara, au kuwalinganisha na wengine.

28. Simulizi za hadithi ni mbinu inayofaa na muhimu sana ya kuhimiza tabia na sifa njema na kukatisha zile mbaya, kama vile haki za marafi- ki, dini na kadhalika. Qur’ani Tukufu inatumia mbinu hii kufanyia hivyo kama ilivyoelezwa katika Surat Yusuf; Aya ya 111:

لَقَدْ كانَ فِي قَصَصِهِمْ عِبْرَةٌ لِلْأُولِي الْأَلْبَابِ {111}

“Bila shaka katika hadithi zao limo fundisho kwa wenye akili …..” (Yusuf; 12:111).

Ni muhimu kuzingatia akilini yafuatayo wakati unapochagua simulizi za hadithi:

a. Hadithi hizo lazima zimtaje Mwenyezi Mungu kwa namna moja au nyingine, na zisimuliwa kwa lengo la kulea utu na tabia za mtoto wako.
b. Umri, akili na hali ya maarifa ya mtoto lazima uzingatiwe wakati wa kuchagua hadithi.
c. Kusiwepo na uzidishaji kiasi, au uongo au uvumi mbali na ukweli ndani ya hadithi hizo.
d. Lazima ziwe na majibu ya maswali ya mtoto.
e. Zichaguliwe hadithi bora, kama vile alivyoeleza Mwenyezi Mungu ndani ya Surat Yusuf, Aya ya 3:
“Sisi tutakusimulieni hadithi zilizo bora zaidi.”
f. Ukweli na uadilifu ni lazima wakati wote viwepo katika hadithi hizo.
g. Mhusika mkuu (ambaye ndiye mfano wa maadili) wa hadithi hizo laz- ima awe hana mikengeuko au tabia mbaya.
h. Hadithi hizo lazima zisiwe ndefu sana au zenye kuchosha juu ya mtoto.

29. Utundu wa mwanao katika miaka ya mwanzoni ni ishara ya akili nyingi inayoongezeka katika miaka ya utu uzima, hivyo usije ukawa na wasiwasi sana au kumuadhibu sana.

30. Wafanye watoto wako waswali kuanzia umri wa miaka saba (7), na kufunga kuanzia miaka 9, ama nusu siku au kiasi kama hicho, kutegemea uwezo wao.

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Pale watoto wetu wanapofikia umri wa miaka 5, sisi tunawaambia waswali, kwa hiyo waambieni watoto wenu kufanya hivyo pale wanapofikia umri wa miaka 7; na sisi tunawaambia watoto wetu wafunge pale wanapofikia umri wa miaka 7 kwa kiasi chochote cha uwezo wanachoweza kuwa nacho, nusu siku, au zaidi, au pungufu kidogo, na wafunje saumu zao wanapokuwa na njaa au kiu ili waweze kuzoea kufunga na kuendeleza uwezo kwa ajili ya hilo, hivyo waambieni watoto wenu katika umri wa miaka 9 wafunge kwa kiasi chochote watakachoweza kuwa na uwezo nacho, na wakati kiu inapowazidia basi wavunje saumu zao.” 14 na 15

Imesimuliwa vilevile katika hadithi: “Tunawaamrisha watoto wetu kufanya tasbihi ya Hadhrat Fatimah (a.s.) kama vile tu tunavyowaamrisha kuswali. 16

Ni muhimu kukumbuka kwamba katika matendo ya ibada, kama katika jambo jingine lolote, lazima kuwe na kiasi cha wastani. Imesimuliwa kuto- ka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Uislam ndiyo dini madhubuti ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Endeleeni na kufanya wastani wa mambo na msifanye vitu ambavyo vitafanya nyoyo zenu kuona taabu kwenye ibada ya Mwenyezi Mungu.17

31. Usiwe mwepesi wa kuwashutumu watoto wako kwa kusema uongo kwa sababu hadi miaka 5, kudanganya halisi, au kudanganya kwa sababu ya faida binafsi ni adimu; bali ni kutokana na mawazo yao mashughuli, yanayohusiana na kucheza au kusababisha mshangao ndani ya wengine, au kwa ugunduzi wa mtoto wa kinafsi.

32. Msiwalaumu watoto ambao wamewachosha ninyi na maswali yao, kwa vile hili linadhoofisha hisia zao za udadisi.

33. Jaribuni kugombana, hususan mbele ya mtoto, kwani holi linawasum- bua sana na linaathiri utu wao.

34. Watoto wana hofu maalum juu ya neno kifo, hususan kifo cha mama au baba yao. Kwa hiyo, pale ambapo sio lazima, msizungumzie wakati wote juu ya kifo, au mfano wake. Hata hivyo, wafundisheni watoto wenu juu ya ukweli wa kifo, wazi wazi na kwa utulivu na bila ya kuvu- tia hofu.

35. Chunguza na kutambua juu ya vipaji vya mwanao na uviendeleze hivyo kiasi inavyowezekana.

36. Kuhusu mielekeo ya kidunia, usimkalifishe mwanao kupita kiasi ili asije akaenda kwenye njia ya upotovu, wala usifanye kwa kiwango cha chini mno, kwani njia zote hizo ni hatari.

37. Sababu moja muhimu ya furaha ya mtoto ni upole wa wazazi. Hakuna sifa nyingine inayoweza kusababisha furaha na utulivu kwa mtoto kama upendo, na kadhalika, hakuna sifa nyingine inayoweza kuvuruga na kutatiza mtoto kama kukosa upendo kutoka kwa wazazi.

Watoto wa wazazi ambao wamefanikiwa katika nyanja hii wanajaribu kiasi cha uwezo wao kuwaridhisha wazazi wao na kujiweka mbali na vitendo ambavyo vinawaudhi na

kuwasumbua, wakati wa utoto wao na pia pale wanapokuwa wakubwa. Kwa hiyo, mapenzi na upendo sio tu vinakidhi haja za watoto bali pia vinawahakikishia utiifu wao.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameelezea juu ya uzito wa upole huu ndani ya Qur’ani Tukufu, katika Surat al-Imraan; Aya ya 159:

فَبِمَا رَحْمَةٍ مِنَ اللّهِ لِنْتَ لَهُمْ وَلَوْ كُنْتَ فَظّا غَلِيظَ الْقَلْبِ {159}

“Basi kwa sababu ya rehema ya Mwenyezi Mungu umekuwa laini kwao na kama ungekuwa mkali mshupavu wa moyo, wangekukim- bia…..” (al-Imraan; 3:159).

Ni muhimu kutambua kwamba hapapaswi kuwa na kuzidi kiasi; mapenzi makubwa sana, kama vile tu madogo sana, ni uharibifu kwa mtoto; kwa hiyo, fuata njia ya kati na kati na uwakuze na kuwalea watoto kwa namna ambayo wanaweza kusimama wenyewe kwa miguu yao miwili (kujitegemea) wanapokuwa watu wazima.Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): “Akina baba wabaya sana ni wale ambao, katika wema na mapenzi yao kwa watoto wao, wanavuka mipaka na kuelekea kwenye kuzidisha kupita kiasi.” 18

38. Ni muhimu kwamba wazazi wawape watoto wao hiari na uhuru kulin- gana na uwezo wao, ili wabadili uzembe wao, na waendeleze uhuru wao wa ndani na kujiamini binafsi. Wakati huo huo, mtu lazima awe mwangal- ifu asivuke mipaka kiasi kwamba watoto wajiletee madhara wao wenyewe.

Baadhi ya wazazi, ama kujipa uhuru wao wenyewe au majukumu yao au kwa sababu ya mapenzi
yaliyopotea njia, wanawaacha kabisa watoto wao kwenye mipango yao wenyewe, hata hivyo, kabla ya
muda mrefu, watoto wanakua bila kujua kitu chochote cha majukumu yao ndani ya nyumba, au vinginevyo.
Ni kufikia hapa ambapo wazazi wanajaribu kuliingiza hili kwa watoto wao, bila kushangaza ikawa bila athari yoyote.

Wazazi wengine hata hivyo, wanafanya kinyume chake na hawawapi watoto wao fursa ya kutosha kuongoza vitendo vyao wenyewe, daima wakiingilia kati katika kile wanachofanya watoto wao na jinsi wanavyofanya. Vyote ni makosa na vina matokeo hasi.

39. Kuwalea watoto wako vizuri inavyostahili ni moja wa wajibu wa mzazi, na kukosa umakini katika wajibu huu ni sababu ya makemeo ya Maimam.19 Mtu anapaswa kujaribu kwa uwezo wake wote kupitia njia mbalimbali kujenga mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Ahlul-Bayt (a.s.), ili watoto wafuate njia ya haki. Kwa kiasi ambacho msingi wa mapenzi ni uzoefu na elimu, watu wajaribu kulipandikiza hili ndani ya watoto wao.20

40. Wafundishe watoto wako Qur’ani. Usomaji wa Qur’ani ndani ya nyumba unaeneza maneno bora ya haki na ukweli halisi wa Uislam. Kuwa katika mazingira ambayo mtu ana ufahamiano na Qur’ani, anasikiliza visomo vya Qur’ani Tukufu na anayafanyia kazi maelekezo ya Qur’ani, kunakuwa na athari kubwa kwenye maisha ya mtoto. Kila wakati wazazi wanaposoma Qur’ani, watoto wanashawishika kufanya vivyo na wanafuata katika

tabia hii. Hasa hasa, wale watoto ambao wana kumbukumbu nzuri ya asili na wana vipaji, wanaweza kwa urahisi kabisa kuhifadhi Qur'ani, ambayo itawanufaisha daima.21

Njia 14 Za Kudukiza Mapenzi Ya Ahlul-Bayt (A.S.) Ndani Ya Watoto Wako

Njia 14 Za Kudukiza Mapenzi Ya Ahlul-Bayt (A.S.) Ndani Ya Watoto Wako22

1. Utungaji mimba, na kile kipindi chote cha kuwa na mimba na tabia ya kiakili ya wazazi vyote vina athari juu ya mtoto katika eneo hili. Vilevile na kufuata yale mapendekezo yaliyotajwa katika kitabu hiki, kufuata mambo ambayo yamekokotezwa: kula tabaaruk (chakula kilichobarikiwa) ya Maimam, kuhudhuria kwenye Majalis na kusikiliza hotuba, kuwa mwangalifu juu ya yale mtu anayoyaangalia au kusikia, na kusikiliza Qur'ani, Nauha na Qasidah wakati wa kunyonyesha, na kadhalika.

2. Tumia kunywa maji ya mto Furati na Khakhe Shafaa (udongo kutoka kwenye eneo karibu na kaburi la Imam Husein (a.s.) huko Karbala).

3. Kuza mapenzi na hisia za upendo. Wafunze watoto wako kwamba mapenzi juu ya Ahlul-Bayt (a.s.) yanasababisha wao kupendwa na Mwenyezi Mungu na hao Ahlul-Bayt (a.s.), na kwamba mapenzi juu Allah na Ahlul-Bayt (a.s.) yanakwenda pamoja mkono kwa mkono.

4. Zingatia neema ya Ahlul-Bayt (a.s.) kwa wafuasi wao, Shi'ah.
Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): "Tunawajua Shi'ah wetu kwa namna ile ile mtu anavyoijua familia yake." Imesimuliwa vilevile kwamba katika Siku ya Kiyama, Shi'ah wa Imam Ali (a.s.) watatoshelezwa, kuokolewa na kufaulu.

5. Peleka ujumbe wa faida za urafiki na Ahlul-Bayt (a.s.), kama vile, "Fahamu kwamba yeyote anayekufa akiwa na mapenzi na dhuria wa Muhammad anakuwa amekufa shahidi," na "Fahamu kwamba, yeyote anayekufa na mapenzi juu ya kizazi cha Muhammad, milango miwili ya peponi itafunguka kutoka kaburini mwake."

Thamani ya mtu ni kulingana na kiasi gani cha mapenzi kilichomo mioy- oni mwao. Jinsi shabaha ya mapenzi ilivyo na thamani zaidi ndivyo anavyokuwa na thamani zaidi yule mwenye kupenda.

6. Fikisha haja ya mapenzi haya. Watu kwa kawaida wanavutiwa na vile vitu ambavyo vinatosheleza mahitaji yao, na sisi kwa kweli ni wahitaji zaidi sana wa hao Ahlul-Bayt (a.s). Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba: "Mapenzi juu yangu na mapenzi juu ya Ahlul-Bayt wangu yanamnufaisha mtu katika sehemu 7 ambako kuna wingi wa misukosuko: Wakati wa kukata roho, ndani ya kaburi, wakati wa kufufuliwa kutoka kaburini, wakati wa kupewa kitabu cha matendo, wakati wa hesabu, wakati wa kupimwa kwa vitendo, na wakati wa kuvuka lile daraja – Siraat."23

7. Onyesha kuthamini kwako, na matumaini yako juu ya vitendo maalum, ili kufanya mfano wa matendo hayo kwa ajili ya baadaye. Imesimuliwa kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alimpa Mwarabu mmoja kipande cha dhahabu ambacho yeye alikizawadiwa, kwa sababu Mwarabu huyo alijiweka kwa unyenyekevu mbele za Allah katika swala yake yenye makusudio mema na ukweli. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Nimekupa dhahabu hii kwa sababu mbele ya Allah, wewe ulimtukuza kwa wema na kwa kustahiki kwake." Hata hivyo, ni muhimu kwamba kumtia mtu moyo kusiwe katika namna ya kishawishi cha hongo.

8. Tekeleza yale unayoyalingania, kwani ile hali ya utu na vitendo vya mzazi ni walimu wasio wa moja kwa moja lakini muhimu sana kwa mtoto.

9. Sherehekea maadhimisho ya zile wiladat (kuzaliwa) na wafat (vifo) vya Ahlul-Bayt (a.s.), kama vile Muharram, Iddul-Ghadir, wiladat ya Imam wa 12, na kadhalika. Hii inajumuisha, sio tu kwenda msikitini, bali na maadhimisho nyumbani, kwenye Madrassa, na kadhalika. Panapaswa kuwepo na mafungamano baina ya furaha ya maisha ya mtoto na maisha ya Maimam (a.s.), kwa mfano, kufanya maadhimisho ya kuzaliwa kwao kuwa ni tukio la furaha katika kumbukumbu za watoto kwa kufanya tafrija, kutoa peremende, zawadi na hivyo kuwa na athari isiyo ya moja kwa moja juu ya mtoto.

10. Tamaa ya mtoto ya kutaka kukua na kufikia ukamilifu ni ya juu sana katika miaka ya ujana na mwanzoni mwa utu uzima, na hii inawasababishia, bila ya kufikiri, kutafuta (watu) vigezo vya mifano katika maisha. Tamaa hii ya kimaumbie lazima itumike vizuri sana na ombwe (nafasi tupu) hiyo ijazwe na Ahlul-Bayt (a.s.)

Kwa kweli, hao Ahlul-Bayt (a.s.) ndio udhihirisho wa ukamilifu wa uzuri wa Mwenyezi Mungu. Kupokezesha ujasiri wao, maadili, miujiza, ukarimu, uwezo wa kutibu watu na kutatua matatizo yao na daraja yao ya uombezi kwa Mwenyezi Mungu vyote vina matokeo mazuri katika kuleta mfungamano kati ya watoto na wao Ahlul-Bayt (a.s.).

Moja ya mbinu za Qur’ani Tukufu katika malezi na kuelekeza wanadamu pia ni katika kutumia vigezo bora ili kumuongoza mtu kwenye njia ya sawa iliyonyooka, kama ilivyoelezwa katika Surat al-Ahzab, Aya ya 21:

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِمَنْ كَانَ يَرْجُو اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا {21}

“Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na kumtaja Mwenyezi Mungu sana.” (al-Ahzaab; 33:21).

11. Jiepushe na vile vitendo ambavyo vinaondoa mapenzi ya Ahlul-Bayt (a.s.) kutoka kwa watoto; hili liende sambamba na vile vitendo vinavy- ochochea mapenzi. Kwa mfano, kama zile Majlisi nyingi zinazofanyika katika zile siku kumi za mwanzo za mwezi wa Muharram zikiwa zinachosha na kuwafanya watoto kuwa wachovu, au hali ya mazingira ikawa sio nzuri kwa watoto kwa kuwa wao hawatendewi vizuri, au watoto wanalazimishwa kufanya ibada nyingi, yote haya yanaweza kusababisha vikwazo kwenye uhusiano wa karibu na wa mapenzi kwa Ahlul-Bayt (a.s.).

12 Jenga mazingira ya kiroho na ya makusudi. Hata kama watoto wataachwa zaidi kwenye mipango yao wenyewe na hawakuvutwa huku na huko, kama wanawekwa kwa utaratibu maalum katika mazingira hayo, huo mvuto kwa Ahlul-Bayt (a.s.) bila kusukumwa utajitokeza. Kambi za kitamaduni na kiislam, ziyara, kwenda kwenye haraam, kukutana na watu wa maana, kuwa na marafiki wa Ahlul-Bayt wakati wote, shughuli za kijamii na kushiriki kwenye majlisi, yote haya yanaweza kuchangia katika kujenga mazingira kama hayo.

13. Wazoeshe watoto wako vitabu, majarida, michoro ya picha za rangi na mashairi kuhusiana na Ahlul-Bayt (a.s.). Hili linaweza kufanyika kwa idadi kadhaa ya njia kama vile mashindano, majadiliano, kusoma, uan- dishi wa makala, kubadilishana mawazo na kadhalika.

14. Himiza uanzishwaji wa vikundi vya vijana hasa kwa kuadhimisha matukio katika maisha ya Ahlul-Bayt (a.s.) kujumuisha shughuli kama vile azadari, michezo, hotuba, na kadhalika.

Uhifadhi Wa Qur'ani Tukufu

Hapa24 chini na baadhi ya mambo ya kuwasaidia wote, wazazi na watoto kuhifadhi Qur'ani, ili kwamba kitendo hiki kitukufu kiweze kuleta manu- faa mfululizo daima, Insha'allah.

1. Anzisha uhifadhi wa Qur'ani kwa watoto katika umri mdogo, kama inavyosemekana kwamba kile kinachojifunzwa katika siku za mapema hakisauliki kamwe.

Kwa kweli, imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.): "Nyoyo za vijana ni kama ardhi isiyolimwa, inakubali chochote kila kinachopandwa juu yake."25 Imesimuliwa pia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Elimu utotoni ni kama kuichonga juu ya jiwe."

2. Hifadhi Qur'ani kwa uaminifu. Vitendo vyote lazima viwe ni kwa kutafuta ukaribu na ujamaa na Mwenyezi Mungu peke Yake. Kwa vile hili sio jambo rahisi kulihamishia kwa watoto, ni lazima waangaliwe kuona kwamba ni nini motisha yao au hamasa juu ya kuhifadhi Qur'ani. Hakuna ubaya katika kuwapa watoto zawadi ili kuwatia moyo pale mwanzoni, na kisha, jinsi vile wanavyokua wakubwa, taratibu na kwa kufaa sana kuwafanya watambue lile lengo halisi nyuma ya vitendo vyao.

3. Hifadhi kila Aya, kifungu au Sura kwa nia ya Ma'sumin (r.a.) au shahidi, na muwasilishie mtu huyo hizo thawabu baada ya kuhifadhi. Sio tu kwamba kufanya hivyo kunamuongezea mtu malipo bali watu hawa vilevile watakuwa waombezi wetu. Hivyo mtu Insha'allah atakuwa mwenye kupokea rehema za ziada, neema na tawfiiq ya Allah Azza wa Jallah, na Aya hizo zitahifadhika haraka na kwa ubora zaidi.

4. Amini katika uwezo wa milele wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

5. Kamwe usikadirie kwa upungufu nguvu ya Dua na maombi. Kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Suratul-Furqaan; Aya ya 77:

قُلْ مَا يَعْبَأُ بِكُمْ رَبِّي لَوْلَا دُعَاؤُكُمْ {77}

"Sema: Mola Wangu asingekujalini kama sio kule kuomba kwenu ….." (al-Furqaan; 25:77).

6. Kuwa shupavu, mwenye lengo, uvumilivu na matumaini. Kufanikisha lengo hili, na vilevile tamaa na shauku, jitihada na dhamiri ni lazima viwepo.
7. Kula vyakula rahisi, halali na halisi kwani hivi ni venye athari sana katika kuiandaa akili na kumbukumbu.

8. Kuwa na ratiba sahihi. Bila ya ratiba sahihi, itakuwa nihatua ndefu na ngumu, na pengine

hata isiyowezekana kulifikia lengo hilo tukufu.

Kwa ajili ya kuhifadhi, ainisha muda maalum kila siku, kipindi maalum cha muda na vile vile kiwango maalum (kwa mfano idadi ya kurasa kwa siku). Usingojee fursa zijitokeze, bali weka kwa bidii sana masharti muhimu yanayotakikana, na jaribu kutokosa hata siku moja ya kutekeleza ratiba hiyo.

9. Tumia Qur'ani ambayo ni rahisi, yenye maandisi ya wazi, ambayo ni rahisi kusomeka na yenye kanuni za tajwiid ndani yake. Kama huna ufahamu wa tafsiri ya Qur'ani Tukufu, ni bora kutumia nakala yenye tafsiri chini yake (au pembeni mwake), ambayo ni fasaha na nyepesi kusomeka, kwani kule kusoma na tafsiri yake pia kutasaidia kuhifadhi. Ni lazima kwamba uwekwaji wa namba za aya ndani ya Qur'ani ni sahihi na wakuaminika. Upande wa nyuma wa kurasa hizo zisije zikawa nyeupe kabisa kwani hilo linapelekea uchovu wa macho.

10. Sahihisha matamshi yako kwa kujifunza chini ya usimamizi wa mso- maji hodari mwenye uwezo, au kumsikiliza msomaji mzuri. Matumizi ya mikanda ya sauti, video na CD yanafaa kwa kazi hii vile vile.[26]

11. Rudia kile ulichokwisha kujifunza, kwa kughani na mara kwa mara.

Usiende kwenye fungu jingine la Aya au Surah mpaka lile fungu la nyuma liwe limekamilishwa. Soma mbele ya watu wengine ili kisahi- hisha na kujaribu ule uhifadhi, na wakati wote rudi kwenye kile kilichohifadhiwa ili kukidumisha.

12. Wakati wa kuhifadhi, kuwa na umakini kamili na akili huru kutokana na mawazo ya aina zote. Hiki ni kimoja cha vipengele kinachoongezea kwenye hifadhi yenye mafanikio. Kuondoa aina zote za vivurugaji, kama vile njaa, kiu, wasiwasi, uchovu ni muhimu sana, kama kulivyo kuchagua kwa muda na mahali panapofaa.

Imesimuliwa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.): "Msomaji wa Qur'ani tukufu anahitaji mambo matatu: moyo mnyenyekevu, mwili huru (kutokana na usumbufu) na mahali pa faragha."

13. Kuwa na udhuu wakati wa kuhifadhi Qur'ani tukufu na elekea Qibla kwa kiasi kinachowezekana.

14. Himiza ushiriki katika mashindano na programu za kuhifadhi na kuso- ma.

15. Soma Dua ifuatayo kabla ya kuanza:

"Ewe Allah! Nipe rehma Zako kwa kuniwezesha mimi kuacha vitendo visivyo vya utii Kwako daima kwa kiasi utakachonibakisha kuwa hai, na unirehemu kwa (kunikinga) kujikalifu na yale ambayo hayanihusu.

Na uniruzuku na mawazo mazuri juu ya yale yote ambayo ni lazima niyafanye ili kukufanye uwe radhi nami. Na uufanye moyo wangu ugandamane kati- ka kukifadhi Kitabu Chako kama ulivyonifundisha, na uniruzuku niweze kukisoma katika namna itakayokufany uridhike nami. Ee Mungu! Nitie nuru katika kuona kwangu kupitia Kitabu Chako, nikunjulie kifua changu, ufurahishe moyo wangu, ufanye ulimi wangu kuwa fasaha na mwili wangu kushughulika. Nitie nguvu kwa Kitabu hiki, unisaidie mimi ndani yake. Hakika hakuna msaidizi kwa ajili yake hicho ila Wewe; hakuna mungu ila Wewe."[27]

Maneno Ya Hekima Kutoka Kwa Imam Ali Ibnul-Husein; Zainul-Abidiin (A.S.)

“Haki ya mama yako ni kwamba, utambue kwamba alikubeba wewe mahali ambapo hakuna mtu anayembeba mtu mwingine, alikupa wewe lile tunda la moyo wake ambalo hakuna mtu anayempa mwingine, na alikulinda wewe kwa viungo vyake vyote. Hakuwa akijali kama ana njaa alimradi wewe ulipata kula, wala kama alikuwa na kiu alimradi wewe ulikunywa, kama hakuvaa ilimradi wewe ulivaa, kama alikuwa juani ilimradi wewe ulikuwa kivulini. Alisamehe usingizi wake kwa ajili yako na alikukinga kutokana na joto na baridi, yote hayo ili uweze kuwa wake.

Hutaweza kumuonyesha yeye shukurani, isipokuwa kupitia msaada wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na Yeye kukupa mafanikio.”

“Haki ya baba yako ni kwamba, unajua kwamba yeye ndiye mzizi wako. Bila ya yeye, wewe usingekuwepo. Wakati wowote unapoona jambo lolote ndani yako ambalo linakufurahisha, ujue kwamba baba yako ndie chanzo cha neema hiyo juu yako. Hivyo mtukuze Mwenyezi Munguna umshuku- ru Yeye kwa kiwango hicho. Na hakuna nguvu ila kwa Mwenyezi Mungu.”

“Haki ya mwanao ni kwamba, unapaswa kujua kwamba yeye anatokana na wewe na atahusishwa na wewe – kupitia vitendo vyake vyote, vizuri na vibaya – katika mambo ya karibuni ya dunia hii. Unawajibika kwa kile ambacho kimedhaminiwa kwako, kama vile kumsomesha katika tabia njema, kumwonyesha kwenye mwelekeo kwa Mola Wake.

Hivyo fanya vitendo kuelekea Kwake kwa vitendo vya mtu anayejua kwamba atalipwa thawabu kwa kufanya mema kuelekea Kwake, na ataadhibiwa kwa kufanya makosa au dhambi.”

Yamechukuliwa kutoka – **Makala ya Haki** – (*ar-Risalatul-Huquq*)

Maneno Ya Hekima Kutoka Kwa Imam Ali Ibnul-Husein; Zainul-Abidiin (A.S.)

“Ewe Mungu! kuwa na huruma juu yangu kupitia kuendelea kuishi kwa wanangu, uwaongoze kwenye haki kwa ajili yangu, na kuniruhusu mimi kuwafaidi wao!”

“Mola Wangu, yafanye maisha yao kuwa marefu kwa ajili yangu, ongeza vipindi vyao, unikuzie yule mdogo kabisa kwa ajili yangu, mpe nguvu yule dhaifu kwa ajili yangu; rekebisha miili yao kwa ajili yangu, kujitolea kwao katika dini, na tabia zao za kimaadili, wafanye wazuri katika nyoyo zao, viungo vyao, na kila kitu ambacho kinanihusu mimi katika mambo yao, mimina kwa ajili yangu na juu ya mikono yangu riziki zao!

Wafanye kuwa wachamungu, wenye kuhofia, wenye utambuzi, wasikivu, na watiifu Kwako, wenye upendo na mwelekeo mwema kwa marafiki Zako, na wap- inzani shupavu na wenye chuki kwa maadui Zako wote! Amiin!

“Ewe Allah, imarisha mkono wangu kupitia kwao, unyooshe mgongo wangu uliolemewa; nizidishie idadi yangu; pendezesha mahudhurio yangu, dumisha utajo wangu, nitosheleze ninapokuwa sipo nyumbani; nisaidie katika mahitaji yangu; na wafanye wenye mapenzi kwangu, upendo, walio karibu, waadilifu, watiifu, wasiwe wakaidi kamwe, wasio na hes-

hima, wapinzani au wakosaji!

“Nisaidie katika kuwalea kwao, kuwaelimisha kwao, na upendo wangu kwao, nipatie miongoni mwao, kutoka Kwako, watoto wanaume, lifanye hilo liwe wema kwa ajili yangu, na wafanye wawe msaada kwa ajili yangu katika kile ninachoomba kutoka Kwako!

“Nipatie mimi pamoja na kizazi changu kinga kutokana na Shetani aliye- laaniwa, kwani Wewe umetuumba sisi, umetuamuru sisi, na umetukataza sisi, na umetufanya sisi kutamani malipo ya kile ulichoamrisha, na kuhofia adhabu yake!

Umetuwekea adui anayepanga dhidi yetu, ukampa mamlaka juu yetu kwa namna ambayo kwamba hukutupa sisi mamlaka juu yake, ukamruhusu yeye kukaa katika vifua vyetu na ukamfanye atembee katika mishipa yetu ya damu; yeye hajali kitu, ingawaje sisi tunajali, yeye hasau, ingawaje sisi tunasahau, anatufanya sisi tujihisi kuwa salama kutokana na adhabu Yako na anatujaza hofu kwa wengine wasiokuwa Wewe.”

Dua kwa ajili ya watoto wema na waadilifu,
as-Safinatul-Kamilatul Sajjadiyah.

1. Mengi yamechukuliwa kutoka Rayhaaneye Beheshti, Uk. 221 – 241
2. Mustadrakul-Wasa’il, Jz. 15, Uk. 171
3. Wasa’ilush-Shi’ah, Jz. 21, Uk. 386, hadithi ya 27659
4. Wasa’ilush-Shi’ah, Jz. 21, Uk. 386, hadithi ya 27658
5. Biharul-Anwaar, Jz. 60, Uk. 381
6. Rawdhatul-Waaidhin.
7. Mustadrakul-Wasa’il, Jz. 2, Uk. 69
8. Dua zinazopendekezwa kwa ajili ya mtoto wa halali zimeelezewa kwa kirefu katika Mlango wa 6 – Mimba: Dua zinazopendekezwa.
9. al-Kafi, Jz. 6, Uk. 47
10. Mustadrakul-Wasa’il, Jz. 2, Uk. 625
11. Biharul-Anwaar, Jz. 103, Uk. 7
12. Mustadrakul-Wasa’il, Jz. 2. Uk. 558
13. Tuhafal-Uquul, Uk. 84
14. al-Kafi, Jz. 3, Uk. 409 hadithi ya 1
15. Hadithi hii inawahusu hasa vijana wavulana; maana ya jumla hata hivyo ni kwamba watoto wanapaswa kufundishwa kuswali na kufunga, miaka michache kabla hawajafikia kipindi cha baleghe, ili kwamba waweze kukuza uwezo kwa ajili ya hilo.
16. al-Kafi, Jz. 3, Uk. 343
17. al-Kafi, Jz. 2, Uk. 86-87
18. Ta’rikh Ya’quubi, Jz. 3, Uk. 53
19. Mustadrakul-Wasa’il, Jz. 15, Uk. 164
20. Hili linaelezewa kwa kina zaidi katika: Njia 14 za kudukiza Mapenzi ya Ahlul-Bayt (a.s.) ndani ya watoto wako katika Mlango huu.
21. Hili linaelezewa kwa kina zaidi katika: Uhifadhi wa Qur’ani, katika Mlango huu.
22. Nyingi zimepatikana kutoka Rayhaaneye Beheshtii, Uk. 244-247
23. Mizan al-Hikmah, Jz. 2, Uk. 237
24. Nyingi zimechukuliwa kutoka kwenye Rayhaaneye Beheshti, Uk. 235-238
25. Nahjul-Balaghah, Barua ya 31
26. Wasomaji wanaopendekezwa ni pamoja na Muhammad Siddiq Menshawi, Khaleel Hussari, Muhammad Jibrail, Abu Bakr Shaatri, hawa pamoja na wengineo wanaweza kupatikana katika mtandao http://www.hidayahonline.org/7page=audio [18].
27. al-Kafi, Jz. 2, uk. 577

Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al-Itrah Foundation:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Ishirini na Nne
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n’amavuko by’ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur’ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya

46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur’an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju’l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju’l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Tujifunze Misingi Ya Dini
68. Sala ni Nguzo ya Dini
69. Mikesha Ya Peshawar
70. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
71. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliy onyooka
72. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
73. Liqaa-u-llaah
74. Muhammad (s) Mtume wa Allah
75. Amani na Jihadi Katika Uislamu
76. Uislamu Ulienea Vipi?
77. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
78. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
79. Urejeo (al-Raja’a)
80. Shahidi kwa ajili ya Ubinadamu
81. Utokezo (al - Badau)
82. Kuanzia ndoa hadi kuwa wazazi
83. Myahudi wa Kimataifa
84. Uislamu na dhana
85. Mtoto mwema
86. Adabu za Sokoni
84. Johari za hekima kwa vijana
85. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
86. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
87. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
88. Tawasali
89. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
90. Maana ya laana na kutukana katika Qur’ani Tukufu
91. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
92. Swala ya maiti na kumlilia maiti
93. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)

94. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
95. Hadithi ya Thaqalain
96. Fatima al-Zahra
97. Tabaruku
98. Sunan an-Nabii
99. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
100. Idil Ghadiri
101. Mahdi katika sunna
102. Kusalia Nabii (s.a.w)
103. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
104. Ujumbe - Sehemu ya Pili
105. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
106. Ujumbe - Sehemu ya Nne
107. Shiya N'abasahaba
108. Iduwa ya Kumayili
109. Maarifa ya Kiislamu.
110. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
111. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
112. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
113. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
114. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
115. Johari zenye hekima kwa vijana
116. Safari ya kuifuata Nuru
117. Historia na sera ya vijana wema
118. Myahudi wa Kimataifa
119. Shahidi kwa ajili ya ubinadamu
120. Visa vya kweli

Back Cover

Kitabu hiki kinazungumzia masuala yote yanayohusu wanandoa: kuanzia kufunga kwao ndoa - waishi vipi, mpaka watakapopata watoto - wawalee vipi - kwa mujibu wa mafundisho ya Kiislamu. Kama ambavyo inafa- hamika kwamba Uislamu ni dini na ni mfumo wa maisha, basi kwa haki- ka haukuacha hata kitu kimoja kinachohusu maisha ya mwanadamu, pamoja na kumhudumia kiroho.

Ndoa ni taasisi ambayo iliasisiwa na Allah '*Azza wa Jallah* Mwenyewe pale alipowaunganisha baba yetu Adam na mama yetu Hawa kuishi pamo- ja kama mume na mke.

Kwa hiyo, Uislamu kama dini na mfumo wa maisha, umeweka kanuni, sheria na hukumu za kufuatwa ndani ya taasisi hii tukufu (ya ndoa). Waandishi wa kitabu hiki wamefanya juhudi kubwa ya kukusanya mafundisho yote muhimu yenye kuhusu taasisi hii kutoka katika vyanzo vikubwa na chimbuko la sheria na mafundisho ya Uislamu, ambavyo ni Qur'ani na Sunna.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com [19]
Tovuti: www.ibn-tv.com [20]

Source URL:
http://www.al-islam.org/sw/kuanzia-ndoa-hadi-kuwa-wazazi-abbas-na-shaheen-merali

Links
[1] http://www.al-islam.org/sw/user/login?destination=node/25378%23comment-form
[2] http://www.al-islam.org/sw/user/register?destination=node/25378%23comment-form
[3] http://www.al-islam.org/sw/person/abbas-na-shaheen-merali
[4] http://www.al-islam.org/sw/person/ramadhani-kanju-shemahimbo
[5] http://www.al-islam.org/sw/organization/alitrah-foundation
[6] http://www.al-islam.org/sw/library/marriage
[7] http://www.al-islam.org/sw/tags/ndoa
[8] http://www.al-islam.org/sw/tags/watoto
[9] http://www.al-islam.org/sw/tags/wazazi
[10] http://www.al-islam.org/sw/tags/familia
[11] http://www.al-islam.org/sw/person/imam-ali-1
[12] http://www.al-islam.org/sw/person/bibi-fatimah
[13] http://www.al-islam.org/sw/person/imam-zainul-abideen
[14] http://www.al-haqq.com
[15] mailto:tph@tph.ca
[16] http://alIslam.org/masoom/writings/duas/arafah.html
[17] http://al-Islam.org/sahifa/dua32.html
[18] http://www.hidayahonline.org/7page=audio
[19] mailto:alitrah@raha.com
[20] http://www.ibn-tv.com